Ufalme Wake Ulikamatwa
Lakini Anaurudisha

# Mfalme wa Utukufu



Kutoka Kwenye
Maandiko Matakatifu

Mwandishi Na
P. D. Bramsen

Picha Zimechorwa Na
Arminda San Martín

Relief Opportunity & Care for Kids
ROCK International
Resources Of Crucial Knowledge

**Mfalme wa Utukufu**
Na P. D. Bramsen
Picha zimechorwa na Arminda San Martín
Copyright @ 2022 ROCK International. All rights reserved.
**www.rockintl.org | www.king-of-glory.com**

**ISBN 978-1-62041-035-6**

Swahili edition of **KING of GLORY** (Picture Book)
Copyright @ 2011, 2025, **ROCK International**
• Relief, Opportunity & Care for Kids
• Resources Of Crucial Knowledge
P.O. Box 4766, Greenville, SC 29608, USA
www.rockintl.org • resources@rockintl.org
**www.king-of-glory.com**

Nukuu za Maandiko zilizotumiwa kwenye kitabu hiki zimechukuliwa kutoka kwenye Maandiko Matakatifu, *Union Version* © Bible Societies of Tanzania and Kenya 1994.

Mirahaba ya kitabu imewekezwa kwenye miradi ya ROCK International. Kutafsiri Mfalme wa Utukufuau uchapishaji na utangazaji mwingine wa ROCK, wasiliana na: resources@rockintl.org

**Kuhusu mwandishi:** Paul Dan Bramsen alizaliwa California. Yeye na mke wake waliwalelea watoto wao watatu huko Senegal, Afrika ya Magharibi, taifa la walio wengi Waislamu kwenye ukingo wa jangwa la Sahara. Bramsen anauandikia umma wa kimataifa, akiunda vyanzo vinavyosimulia kuhusu manabii wa kibiblia kwa mpangilio wa nyakati. Maandishi yake ni pamoja na *The Way of Righteousness* (mfululizo wa matukio 100 ya matangazo kwa njia ya redio, ulioandikwa kwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiwolof ya Senegal, sasa katika lugha nyingi), na *One God One Message* (kitabu kilichoandaliwa kiwasaidie wenye mashaka juu ya vipingamizi vyao na wanaoitafuta kweli na waweze kuielewa vizuri habari kuhusu Mungu na ujumbe wake), na filamu ya MFALME WA UTUKUFU (safari ya kuvutia ya dakika 222 kupitia Maandiko ya manabii, katika lugha nyingi). www.king-of-glory.com

**Kuhusu Mchoraji:** Arminda San Martín wa Argentina anaandika: "Tangu wakati ninaoweza kuukumbuka, nimekuwa nikichora. Baada ya mapumziko ya kujiweka wakfu nikawa mke na nikalea watoto wangu, nilianza tena amali yangu kwa kupata shahada ya Sanaa. Nilifanya kazi kwa bidii, nikivumbua mbinu tofauti kwenye nchi yangu mwenyewe na pia huko New York, ambako niliishi miaka michache miaka ya '90. Baada ya kurudi Argentina nilipata nafasi ya kuendeleza kazi ya kitaalamu nikitengeneza vielelezo kwa ajili ya vitabu vingi, hasa vinavyohusu asili na mambo ya kiroho. Ujuzi wangu wote niliopewa na Mungu umemwagwa kwenye uchoraji wa *Mfalme wa Utukufu*. Kwangu mimi, mradi huu ni ndoto iliyotimia, nafasi ya kutokea mara moja katika maisha. Shukurani zangu kwa Bwana hazitoshi kwa fursa hii. Pia ninamshukuru sana Paul Bramsen, ambaye siye tu mwandishi mwenye upako, bali pia ni mhariri aliyejitokeza. Ninamshukuru Mungu kwa ufahamu na mwongozo wake thabiti hadi kufanikisha matokeo haya ya mwisho." Hivi sasa Arminda anafanya kazi kama mchoraji wa vielelezo kwenye nyumba nyingi za uchapishaji.

*Kimechapishwa nchini Kenya*
*Printed in Kenya*








**KWA UTUKUFU WA MFALME NA BARAKA YA WATOTO WA VIZAZI VYOTE KWENYE KILA TAIFA**







*"Salama? Nani Aliyesema lo lote kuhusu salama? Bila shaka hayuko salama. Lakini yu mwema. Yeye ndiye Mfalme, nakwambia."*

—*Kutoka The Lion, the Witch, and the Wardrobe kilichoandikwa na C.S. Lewis*









# Orodha ya matukio


**Nyuma ya majukwaa** . . . . . . . . . . 8

**Ufunguzi** . . . . . . . . . . 11

1 • Mfalme Na Ufalme Wake

2 • Mfalme Na Manabii Wake

3 • Mfalme Na Ulimwengu Wake

**Sehemu ya 1 – Mfalme Atabiri Mpango Wake** . . . . . . . . . . 19

| | |
|---|---|
| 4 • Siku Ya Kwanza | Mwanzo 1 |
| 5 • Ulimwengu Mkamilifu | Mwanzo 1-2 |
| 6 • Mwanadamu Wa Kwanza | Mwanzo 1-2 |
| 7 • Makazi Kamilifu | Mwanzo 2 |
| 8 • Sheria Ya Dhambi Na Mauti | Mwanzo 2 |
| 9 • Mwanamke Wa Kwanza | Mwanzo 2 |
| 10 • Ufalme Wa Nuru | Ufunuo 4-5 |
| 11 • Ufalme Wa Giza | Isaya 14; Ezekieli 28 |
| 12 • Nyoka | Mwanzo 3 |
| 13 • Uchaguzi | Mwanzo 3 |
| 14 • Dhambi Na Aibu | Mwanzo 3 |
| 15 • Wamekufa Kiroho | Mwanzo 3 |
| 16 • Laana | Mwanzo 3 |
| 17 • Ahadi | Mwanzo 3 |
| 18 • Sadaka Ya Kwanza | Mwanzo 3 |
| 19 • Wamefukuzwa | Mwanzo 3 |
| 20 • Watoto Wa Kwanza | Mwanzo 4 |
| 21 • Wenye Dhambi Wanaabudu | Mwanzo 4 |
| 22 • Sheria Ya Sadaka Ya Dhambi | Mwanzo 4 |
| 23 • Kukubaliwa Na Kukataliwa | Mwanzo 4 |
| 24 • Mauaji Ya Kwanza | Mwanzo 4-5 |

25 • Uvumilivu Na Hukumu Mwanzo 6-7
26 • Mwanzo Mpya Mwanzo 8-9
27 • Mnara Wa Majivuno Mwanzo 11
28 • Mungu Anamwita Ibrahimu Mwanzo 12
29 • Mtunza Ahadi Mwanzo 15
30 • Jaribu Kuu Mwanzo 22
31 • Mwana Aliyehukumiwa Mwanzo 22
32 • Mifano Na Unabii Mwanzo 22
33 • Mungu Mwaminifu Na Mtakatifu Kutoka 19-20
34 • Amri Kumi Kutoka 20
35 • Mifano Zaidi Kutoka 20, 24
36 • Unabii Zaidi Zaburi & Manabii

**Sehemu ya 2 – Mfalme Atimiza Mpango Wake ........................ 87**

37 • Habari za Mfalme Zinaendelea Mathayo 1
38 • Habari Za Mariamu Luka 1
39 • Habari Za Yusufu Mathayo 1
40 • Ujio Luka 2
41 • Habari Za Wachungaji Luka 2
42 • Habari Za Mamajusi Mathayo 2
43 • Mtoto Mkamilifu Luka 2
44 • Mwana-Kondoo Wa Mungu Yohana 1
45 • Mwana Mkamilifu Mathayo 3
46 • Mwanadamu Wa Pili Mathayo 4
47 • Mfalme-Masihi Luka 4
48 • Mamlaka Juu Ya Mapepo Na Magonjwa Luka 4
49 • Mamlaka Juu Ya Upepo Na Mawimbi Marko 4
50 • Mamlaka Juu Ya Dhambi Marko 2
51 • Mamlaka Juu Ya Kifo Luka 7; Yohana 11
52 • Mpaji Yohana 6
53 • Mwalimu Mathayo 5-7
54 • Fahari Yake Mathayo 17
55 • Utume Wake Mathayo 16, 20
56 • Mfalme Anaingia Yerusalemu Marko 11
57 • Mfalme Anahojiwa Luka 20
58 • Mfalme Anakamatwa Marko 14
59 • Mfalme Anahukumiwa Yohana 18
60 • Mfalme Anavikwa Taji Mathayo 27
61 • Mfalme Anasulubiwa Luka 23
62 • Mfalme-Mwokozi Luka 23
63 • Sadaka Ya Mwisho Mathayo 27
64 • Mfalme Amezikwa Mathayo 27
65 • Kaburi Tupu Mathayo 28
66 • Ujumbe Wa Manabii Luka 24
67 • Mwili Wa Utukufu Yohana 20
68 • Kuondoka Matendo 1
69 • Sherehe Ya Ushindi Zaburi 24; Ufunuo 5
70 • Mfalme Atakuja Tena Ufunuo 19-22

**Kufunga........................................................157**

• Kwa Furaha Milele Baadaye?
• Habari Mbaya
• Habari Njema
• Mwitikio Wako Kwa Mfalme

**Mambo Ya Ziada..............................................167**

• Maswali Ya Mapitio • Sehemu ya 1 • Agano La Kale
• Maswali Ya Mapitio • Sehemu ya 2 • Agano Jipya
• Ukumbusho Wa Mwisho
• Kwenda Ndani Zaidi
• Mwongozo wa matukio ya filamu

# NYUMA YA MAJUKWAA

*"Alice alianza kuchoka sana kukaa karibu na dada yake ufukoni, na bila lo lote la kufanya; mara moja au mbili alikuwa amechungulia kwenye kitabu alichokuwa akisoma dada yake, lakini hakikuwa na picha wala mazungumzo ndani yake, Alice alifikiria, "kina faida gani kitabu ambacho hakina picha wala mazungumzo?"*

—Mistari ya mwanzo kwenye kitabu *Alice's Adventures in Wonderland* alichoandika Lewis Caroll , 1865

Kitabu unachotaka kusoma kimejaa picha na mazungumzo, lakini tofauti na habari maarufu za kubuni za *Alice kwenye nchi ya ajabu*,[1] picha na mazungumzo kwenye kitabu *Mfalme wa Utukufu* hutiririka kutoka kwenye simulizi la kweli lililowahi kutokea.[2]

Niliamua kwa wasiwasi kutoa kitabu chenye picha kuhusu simulizi kuu kati ya yote yaliyowahi kutolewa.

Miaka iliyopita, nilipokuwa nikiishi Afrika ya Magharibi, nilijifunza masomo yanayohusu utoaji wa kipindi kwa njia ya redio. Siku ya kwanza darasani mkufunzi aliuliza, "Ni nini moja ya faida kubwa ya redio kuizidi televisheni?" Jibu lake lilitushangaza.

"Inatoa picha bora zaidi."

Ni kweli.

Hata sinema za hali ya juu huhangaika kuufikia uwezo wa akili ya mwanadamu kutafsiri maneno rahisi yaweze kuwa mifano dhahiri ya kiakili. Maandiko ya kale ya manabii huchora mamia ya picha za maneno ambazo sinema haziwezi kuonyesha kwa hali ya kuridhisha, ambazo mwanadamu na usanii wake anaweza kuzifafanua kikamilifu.

Hivyo ninakubali. Haupo usanii unaoweza kuyaonyesha kikamilifu masimulizi yaliyo bora kuzidi yote yaliyowahi kusimuliwa. Hata hivyo, imekuwa burudani kujaribu.







Arminda San Martín, msanii wetu mwenye karama na neema kutoka Argentina, amefanya kazi ya kushangaza na sahihi ya kutafsiri habari za kibiblia kutoka maneno hadi picha za rangi. Kwa kalamu ya kidigitali na brashi, Arminda alikamilisha michoro ya mwanzo na upakaji rangi wa mwisho ndani ya miezi kumi na minne tu. Ninatumaini kazi yake itakusisimua kama ilivyofanya kwangu.

Sasa lifikirie hili.

Tukisoma simulizi la kitabu, tunaanzia wapi? Katikati? La, tunaanzia mwanzoni. Ndipo tu tutakapolielewa simulizi. Kadhalika, kuyaelewa Maandiko, lazima tuanzie mwanzo na tulifuatilie simulizi hadi kwenye hitimisho lake lenye mantiki na kuridhisha.

Maandishi ya manabii yana mamia ya simuliizi fupi zinazopatana na kufanya simulizi moja. Katika kuandika *Mfalme wa Utukufu*, ni mejisikia kama muuza maua niliyeagizwa kwenda kwenye bustani kubwa mno lenye maua yasiyo na kikomo, nikachague dazeni chache, na nizipange ziwe shada moja linaloonyesha utukufu wa bustani nzima. Kwa kitabu hiki, nimechagua dazeni chache za masimulizi ya msingi kutoka kwenye Maandiko na kuyapanga yawe tamthiliya yenye matukio 70 katika jitihada ya kuuonyesha utukufu wa Mfalme wa milele aliyejidhihirisha Mwenyewe kwenye historia ya wanadamu.

Maombi yangu kwa Mungu ni kuwa kuonyesha na kusimulia kwa simulizi hili la kweli kutavutia watu wa kila rika wayafurahie maandishi ya manabii, wampende wanayemzungumzia, na wajiunge na huo ufalme wenye furaha ambao hautakuwa na mwisho.

Kwa picha inayoeleweka,

Paul D. Bramsen

# Ufunguzi

Moyo wangu umefurika kwa neno jema,
Mimi nasema niliyomfanyizia Mfalme;
Ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi mstadi.

Katika fahari yako usitawi uendelee
Kwa ajili ya kweli na upole na haki;
Na mkono wako wa kuume utakufundisha
mambo ya kutisha.

— Kutoka kwenye Maandiko ya Manabii (Zaburi 45:1,4)

## Tukio la 1

# Mfalme Na Ufalme Wake

Zamani za kale, kabla kabisa ya ulimwengu kuwako, alikuwako mfalme, Mfalme wa utukufu.

Mfalme huyu alikuwa mbali, juu sana na ng'ambo ya cho chote na ye yote tunayeweza kumfikiria. Kwenye kutokuwa na mwisho kwa umilele yeye pekee alikuwa Mfalme, na ufalme wake ndio uliokuwa ufalme pekee, enzi yenye hekima, upendo, furaha, na amani kikamilifu. Ufalme huo haukuwa na haja ya jua wala nyota, maana Mfalme Mwenyewe alikuwa nuru yake.

Huku ufalme huo ukiwa bila mipaka kiukubwa, ulikuwa na mipaka kwa waliokuwa chini yake. Baadhi husema Mfalme hakuwa kabisa na wa chini yake.

Au hakuwa nao?

Moja ya siri za mwanzo za Mfalme huyu ilikuwa kwamba pamoja na kuwa ni Yeye pekee aliyekuwako, kamwe Yeye hakuwa peke yake.

Isitoshe, Yeye alitaka ashiriki maisha na viumbe wengine wenye akili.

Hivyo Mfalme huyu mwema na mwenye hekima alifanya jimbo la mbinguni lenye mamilioni ya viumbe wa kiroho wanaong'aa, wenye akili kupita kiasi walioitwa malaika. Aliwajua wote kwa majina na alitaka nao wamjue Yeye. Maisha na Mfalme huyo lilikuwa tukio la ajabu lisilo na kikomo.

Lakini Mfalme alitaka zaidi ya malaika. Hivyo Aliumba ufalme wa wakati, anga, na vitu — ulimwengu wa kustaajabisha wenye sayari ya kumeremeta ambayo yangekuwa makao ya jamii ya viumbe wa ajabu wanaoitwa wanadamu.

Tofauti na malaika, familia ya wanadamu ilianza na viumbe wawili tu, wa kiume na wa kike. Kama ilivyokuwa kwa malaika, Mfalme alitaka ashiriki pia na wanadamu. Kisha lilitokea jambo, jambo la kutisha. Uasi ulitokea kwenye ufalme, kwanza mbinguni, kisha kwenye dunia.

Malaika mwasi aliuchukua ufalme wa dunia kwa kuwateka wanadamu wake. Lakini Mfalme hakushituka.

Ndani kabisa ya moyo wa Mfalme ulikuwamo mpango wa kuokoa wa ajabu, wa kimiujiza, wa kupita kiasi, wenye athari mno, kiasi kwamba angechukua maelfu ya miaka kuutimiza.

Ungetarajia jambo gani lingine kutoka kwa Mfalme wa umilele?

Anaishi juu ya wakati.







# Tukio la 2
## Mfalme Na Manabii Wake

Kumjua Mfalme na mpango Wake, lazima ukijue kitabu Chake. Kwa zaidi ya miaka 1500 Mfalme alichagua watu kama 40 waandike habari zake na ujumbe wake. Waliitwa manabii. Mfalme aliwapa maneno Yake, waliyoyaandika kwenye magombo ili yanakiliwe, yaenezwe, na yatunzwe kwa ajili ya vizazi vijavyo. Ingawa manabii wengi hawakujuana hata kidogo, maandishi yao husimulia simulizi moja na ujumbe mmoja ulio thabiti.

Maandishi ya manabii hao huitwa Maandiko Matakatifu. Bila ya Maandiko hayo tungeweza kubashiri tu ni wapi tumetoka, kwa nini tuko hapa, na ni wapi tunakokwenda. Ili tujue majibu sahihi tunakihitaji kitabu cha Mfalme.

Kama miaka 3500 iliyopita, Mfalme alimvuvia nabii aliyeitwa Musa akaandika,

> Mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha BWANA. (Kumbukumbu 8:3)

Leo maneno ya Mfalme yamekusanywa kikawa kitabu kimoja, *Biblia Takatifu*. Takatifu maana yake ni *safi* au *kilichotengwa tofauti na vingine vyote*. Biblia maana yake ni *kitabu* au *mkusanyiko wa vitabu*. Biblia imeuzwa na kutafsiriwa kwa wingi zaidi ya kitabu kingine cho chote. Maelfu ya karatasi za mavunjo na magombo ya ngozi huonyesha kuwa ni maandiko ya kale yaliyohifadhiwa vizuri zaidi.[3]

Hayo Maandiko Matakatifu yana sehemu mbili kuu.

Sehemu ya mwanzo ni lile Agano la Kale (Torati, Zaburi, nk.) ambapo Mfalme anatabiri mpango Wake.

Sehemu ya pili ni lile Agano Jipya (Injili, Matendo, nk.) ambapo Mfalme anatimiza mpango Wake.

Agano maana yake ni *mkataba,* au *makubaliano*. Agano la Kale hutabiri alichopanga Mungu kufanya. Agano Jipya lina kumbukumbu ya kutimia kwa mpango wake. Ni Mungu pekee anayeweza kuiandika historia kabla haijatokea.

Tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya ni tofauti kati ya Mfalme mkuu kukutumia barua na picha — na kuja Yeye mwenyewe kukutembelea.

Maandiko yalikuja kwanza huko Mashariki ya Kati, Afrika, Asia, na Ulaya, kisha baadaye huko Amerika na ng'ambo yake. Manabii walitokea Mashariki ya Kati, lakini simulizi na ujumbe walioandika ni kwa ajili ya kila taifa. Kwa ajili ya kila familia, Kwa ajili ya kila mtu. Kwa ajili yako.







## TUKIO LA 3
# MFALME NA ULIMWENGU WAKE

Tungeweza kurudi nyuma kuvuka wakati na anga,
nyuma,
nyuma,
nyuma sana,
kabla ya kuwako watu, sayari, au nyota, tungeshuhudia uwezo na utukufu nyuma ya maneno ya kwanza ya Andiko:

> Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. (Mwanzo 1:1)

Leo, watu wengi hufikiri ulimwengu na maajabu yake vilitokea bila ya Muumbaji mwenye hekima yote. Lakini nadharia zao haziuelezi vya kutosha usanifu huu usioelezeka na mpangilio Unaoonekana wa ulimwengu.

Kwenye kitabu Chake, Mfalme anasema,

> Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake. (Zaburi 19:1)

Ukizungumzia mikono, iangalie ya kwako mwenyewe. Chezesha vidole gumba vyako. Jaribu kukamata kitabu, mfagio, au nyundo bila ya vidole gumba. Angalia kwenye kucha, maungio, na ngozi. Fikiria baadhi ya mambo muhimu unayofanya kwa kutumia mikono yako. Nani kama si fundi stadi mkuu ambaye anaweza kubuni nyenzo kama hizo?

Ni hekima ya aina gani na uwezo wa aina gani vilivyohitajika kuumba bilioni nzima ya makundi ya nyota? Au kuumba chembe hai na mamilioni ya sehemu zake mchanganyiko? Au kuzifuma pamoja nyuzi za seli pamoja na mkusanyiko wa vinasaba vinavyokufanya uwe *wewe?*

Miaka elfu tatu iliyopita, nabii na mfalme aliyeitwa Daudi aliandika,

> Uliniumba tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. (Zaburi 139:13-14)

Ungependa kukutana na yule aliyekuumba? Ungependa kuishi milele na Muumbaji na Bwana wa makundi ya nyota? Unaweza. Amejifunua Mwenyewe. Anataka umjue. Anataka familia na jamii yako nao wamjue. Anakukaribisha uufahamu mpango wake, uone upendo wake, uutazame utukufu wake, ujikabidhi kwenye utawala wake, na uishi kwa ajili ya utukufu wake. Lakini hatakulazimisha kuwa raia wake.

Hata hivyo, Yeye si mfalme fulani tu. Yeye *ndiye* Mfalme. *Mfalme wa utukufu.*

Hizi ndizo habari Zake.





# Sehemu Ya 1

## Mfalme Atabiri Mpango wake

— Agano La Kale —



## TUKIO LA 4
# SIKU YA KWANZA

Kitabu cha Mungu kinaanza kwa namna anayostahili mfalme. Anatueleza anachotaka tukijue na si zaidi.

> Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. (Mwanzo 1:1)

Kila tunachoweza kukiona na kukigusa kina mwanzo, lakini Muumbaji na Mmiliki wa ulimwengu hana mwanzo wala mwisho. Yeye ni Roho asiyeonekana, wa milele anayeweza kuwa pote wakati ule ule. Anaona na anajua kila jambo.

Unalijua Jina lake? Mungu ana majina mengi, lakini Jina lake lililovuma zaidi ni BWANA. Kwenye lugha ya asili ya kitabu cha Mungu, jina lake ni *Yahweh*, yaani *ALIYEKO*, au tu *MIMI NIKO*.

Simulizi la uumbaji linaendelea kwa maelezo ya dunia ya asili ya Mfalme.

> Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji. (Mwanzo 1:2)

Ulikuwa wakati wa kuiandaa sayari kwa ajili ya watu.

> Mungu akasema, "Iwe nuru; ikawa nuru."
>
> Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza. Mungu akaiita nuru Mchana, na giza akaliita Usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja. (Mwanzo 1:3-5)

Mungu alifanya nini siku ya kwanza ya uumbaji? Aliamuru nuru ilichome giza. Baadaye jua liliiangazia nchi, lakini si kwenye siku ya kwanza. Mungu anataka tujue kuwa Yeye ndiye chanzo cha nuru.

> Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake. (1 Yohana 1:5)

Mungu ni msafi, kama nuru. Hawezi kuchafuliwa. Nuru hata ikiangaza kwenye vitu vichafu sana, iko safi. Mungu ni mkamilifu. Mungu ni mtakatifu.


Ulimtambua aliyekuwako pamoja na Mungu kwenye eneo la uumbaji? Roho wake alikuwako, akitulia juu ya uso wa maji. Neno Wake naye alikuwako, akizungumza.

> Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vifanyika kwa huyo … (Yohana 1:1-3)

Roho Mtakatifu wa Mungu Na Neno wamekuwa wakati wote pamoja na Mungu mmoja wa kweli. Ndiyo maana inaweza kusemwa kuhusu Mfalme huyo:

*Hata kama ni Yeye pekee aliyekuwako, kamwe Hakuwa peke yake.*







# Tukio la 5
## Ulimwengu Mkamilifu

Kwa siku sita zenye utaratibu, Mfalme aliumba ulimwengu mzuri ajabu. Mungu alisema tu, na maajabu yaliyobuniwa kikamilifu yakatokea.

Siku ya kwanza Mungu alisema, "Na iwe nuru!" na ikawako nuru.

Siku ya pili Mungu aliumba Mazingira ya dunia na mbingu ya bluu tunayoiona na hewa isiyoonekana tunayovuta. Mungu akalibuni anga likiwa na mchanganyiko thabiti wa gesi zinazolinda uhai, kama vile oksijeni na naitrojeni.

Siku ya tatu Mungu alisema, "Nchi kavu na ionekane!" Na ndicho kilichotokea. Kisha Mungu akasema, "Nchi na itoe majani!" Hapo hapo, nyasi, mimea, maua, na matunda yalianza kumea, kila moja na mbegu zake lenyewe.

Siku ya nne Mungu aliamuru jua na mwezi viangaze na viwe dalili ya miaka, miezi na siku duniani. Aliumba na nyota.

Siku ya tano Mungu alisema, "Maji na yajawe na samaki na vingine vyenye uhai! Anga na lijawe na ndege wa kila aina!" Na ndicho kilichotokea.

Siku ya sita Mungu akasema, "Nchi na izae kila aina ya mnyama – mifugo, wanyama wadogo wadogo, na wanyama wa porini!" Mungu aliwezesha kila kiumbe hai kuzaana kwa aina yake na kutunza vichanga vyake.

> Mungu akaona ya kuwa ni vyema. (Mwanzo 1:25)

Amani ilitawala. Hapo mwanzo wanyama wote walikuwa marafiki. Hawakuuana na kulana. Mimea ilitoa chakula chake.


Utaratibu ulitawala. Kama kazi ya saa, jua lilitunza umbali sahihi kutoka duniani. Mwezi ulibadilika kutoka mwezi mchanga hadi mwezi mpevu. Dunia iliitengeneza upya hewa, na maji yake, na uchafu wake. Ungetawaliwa vema, ufalme wa dunia haungepungukiwa na cho chote chema. Ungekuwa makao ya kuwafaa wanadamu.

Kila siku ya uumbaji hutupa dokezo la vile Mungu alivyo.[4]

- Siku ya 1. Huonyesha kuwa Mungu ni *mtakatifu*. Mkamilifu na msafi kama nuru.
- Siku ya 2. Mungu *anaweza yote*. Aliyaumba, na anayathibiti mazingira.
- Siku ya 3. Mungu ni *mwema*. Aliumba mimea na vyakula vingi kwa ajili yetu.
- Siku ya 4. Mungu ni *mwaminifu*. Jua na mwezi hukaa kwenye mizunguko yake.
- Siku ya 5. Mungu ni *uhai*. Aliweka samaki baharini na ndege angani.
- Siku ya 6. Mungu ni *upendo*. Baada ya Mungu kuwaumba wanyama, ulifika wakati aumbe viumbe wa kuwamwagia upendo wake.

Ulifika wakati wa kuumba viumbe maalum wa kuweza kuuonyesha utakatifu, uwezo, wema, uaminifu, uhai, na upendo Wake.







# Tukio la 6
## Mwanadamu Wa Kwanza

Siku ya sita ya uumbaji, Mfalme alisemezana ndani yake mwenyewe (Mungu, Roho Wake Mtakatifu, na Neno Wake), akisema,

> "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu;[5] wakatawale … nchi yote, na kila chenye uhai …"
>
> Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. (Mwanzo 1:26-27)

Andiko linaposema kuwa Mungu aliwaumba watu kwa mfano wake, haina maana kuwa Mungu yu kama tulivyo sisi. Ina maana kuwa inatubidi tuonyeshe asili yake na utu wake. Kama sarafu za Kirumi baadaye zilivyowekewa mhuri wa mfano wa mfalme, na wanadamu waliwekewa mhuri wa mfano wa Mungu. Mwanamume na mwanamke wa kwanza waliumbwa wakiwa na uwezo wa kufikiri, kupenda, na kuzungumza kama Muumbaji wao waweze kufurahia uhusiano wa karibu naye. Watu hawakuumbwa wawe watumwa wa Mungu, bali wawe marafiki wa Mungu.

Katika kuwaumba wanadamu kwa mfano wake, Mungu aliwapa umiliki. Waitunze na kuitawala nchi kwa ajili ya Mungu, wazigundue siri za nchi na kuzitumia rasilimali zake kwa hekima. Uwezo kama huo uliwatenganisha wanadamu na ufalme wa wanyama.

Kwa wanyama, Mungu alitoa vipimo viwili: mwili na nafsi. Kwa wanadamu, Mungu alitoa vipimo vitatu: mwili, nafsi, na roho.

> BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi[6] ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. (Mwanzo 2:7)

Mwili ulikuwa nyumba tu, au hema, ambamo Mungu alipulizia nafsi na roho ya mtu.

Nafsi ilikuwa akili, hisia, na utashi binafsi ndani ya mwanadamu, vilivyomwezesha mwanadamu kufikiri, kuhisi, na kuchagua.

Roho ilimuunganisha mwanadamu kwa Mungu. Huku mwili ukimwezesha mwanadamu kuunganika na ulimwengu unaoonekana, roho ilimwezesha mwanadamu kuungana na Mungu asiyeonekana. BWANA alitaka wanadamu wamjue.

Wanadamu walikuwa hazina maalum ya Mungu. Kwa kuwa Mungu aliwaumba, hakuwa tu Muumbaji wao, bali pia Mmiliki wao.

BWANA Mungu alimwita mwanadamu wa kwanza Adamu, yaani *Wa udongo,* au tu *Mwanadamu*. Baadaye Mungu alimuumba mwanamke wa kwanza, lakini kwanza yalikuwako maandalizi fulani ya kufanya.

Adamu alihitaji makao na kazi.







## Tukio la 7
# Makazi Kamilifu

Baada ya kuufanya mwili wa kwanza wa mwanadamu kwa mavumbi[6] na kuupulizia uhai, Mungu alipanda bustani huko Eden, mahali fulani huko Mashariki ya Kati.

Mto mzuri ulitiririka katikati ya bustani.

> BWANA Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.
>
> BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. (Mwanzo 2:9,15)

BWANA Mungu hakumwuliza Adamu kama alitaka kuishi katika Edeni. Mungu alikuwa Muumbaji na Mmiliki wa Adamu. Alijua kilicho bora zaidi kwa mwanadamu.

Makao ya Adamu ya bustanini yalijaa vitu vya kufurahisha visivyo na ukomo—vya kuona, kusikia, kunusa, kugusa, na kuonja. Vijito vya kumeremeta. Ndege wa kuimba. Maua ya kunukia. Viumbe wenye manyoya. Matunda yenye maji mengi. Maboga mazuri. Matunda matamu madogo madogo. Misitu ya ajabu. Miamba yenye rangi. Wadudu wa kuvutia. Na trilioni nzima ya maajabu mengine yaliyosubiri kugunduliwa.

Lakini mwanadamu aliumbwa si tu kwa ajili ya kuvumbua na kula. Mungu alimwumba Adamu awe mkuu wa uzao wa wanadamu. Mungu alitaka Adamu na familia yake watawale Naye milele. Lakini ni waaminifu tu kwa kazi ndogo wanaoweza kupewa kazi kubwa.

Hivyo Mungu alimpa Adamu kazi yake ya kwanza: Kuitunza bustani.

Bustani hii ilikuwa eneo lisilo na kasoro. Halikuwa na miiba wala magugu wala wadudu wabaya. Hali ya hewa ilikuwa njema na ardhi ilikuwa na rutuba, hata hivyo haikunyesha mvua. Badala yake, umande ulitokea ardhini ukaimwagilia ardhi.

Mungu pia alimpa Adamu kazi nyingine: Kuwapa wanyama majina.


BWANA alivileta kwake viumbe aone ataviitaje. Lifikirie tukio hilo. Jozi ya wanyama na manyoya yao shingoni na miguu yenye nguvu wakija na mwendo wao. Adamu anawachunguza, anapapasa migongo yao, anawapa jina *farasi*. Muumbaji anaita, ndege mkubwa mwenye mdomo wa kindoano na mbawa pana anashuka. Adamu anasema, “Tai!” anayefuata, mnyama mwenye rangi ya chungwa na milia mweusi anapita. Unadhani Adamu alimwitaje?

> Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni. (Mwanzo 2:20)

Edeni ilikuwa mahali tosha kwa mwanadamu kumjua Muumba wake.

Ulifika wakati wa kumjaribu Adamu.







## Tukio la 8
# Sheria Ya Dhambi Na Mauti

Tangu mwanzo, Mungu na mwanadamu walikuwa marafiki, lakini urafiki huo ulihitaji kujaribiwa. Mfalme wa ulimwengu hangeujaza ufalme wake na raia waliolazimishwa kumtii.

Mungu alimpenda Adamu na alikuwa na mipango ya heshima kwa ajili yake na familia yake ya baadaye. Kwa kuwa Mungu alitaka watu na si vikaragosi, Alimpa Adamu amri moja aitii.

> Bwana Mungu akamwambia huyo mtu, akisema, "Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula; walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."
> (Mwanzo 2:16-17)

Hili halikuwa agizo gumu. Adamu angeweza kula tunda lo lote kwenye bustani *isipokuwa moja*. Kwa kutii agizo hili rahisi, Adamu angeonyesha kuwa aliamini kuwa Muumba wake alijua kilichokuwa bora zaidi kwa ajili yake.

Mungu alisema lingetokea jambo gani kwa Adamu akivunja agizo lake?

Mungu alimwambia Adamu kuwa akila tunda lilokatazwa lazima aanze kutimiza desturi za kidini, atumie shanga za sala, afunge, atoe sadaka, aende kwenye kanisa, sinagogi, au msikiti, na ajaribu kutenda mema ya kutosha kuwianisha kwenye matendo yake mabaya? Ndicho alichosema Mungu?

La, Mungu hakusema hivyo.

Mungu alimwambia Adamu, "Utakapokula matunda ya mti huo *utakufa hakika*."

Kutotii agizo la Mungu huitwa *dhambi*.
Adhabu ya kuvunja agizo la Mungu ilikuwa *kifo*.
Kwenye kitabu chake, Mfalme huiita hii "sheria ya dhambi na mauti" (Warumi 8:2).

Sheria ya Mfalme inasema kuwa dhambi lazima iadhibiwe kwa kifo.


Maana ya kifo ni *kutengwa*. Kama Adamu hakutii agizo moja la Mungu, alikuwa kama tawi lililovunjika linaloanza kunyauka na kufa likitenganishwa tu na chanzo cha uhai.

Kama Adamu aliamua kufanya alichotaka badala ya kile alichoagizwa na Mfalme wa ulimwengu, hicho kilikuwa kitendo cha uasi; hiyo ilikuwa *dhambi*.

Dhambi iliukomesha urafiki wa mwanadamu na Mungu.
Dhambi ilisababisha mwili wa mwanadamu kuzeeka na kufa.
Dhambi iliitenganisha roho, na nafsi ya mwanadamu, na mwili wa mwanadamu, mwanadamu akatengana na Mungu milele.

Dhambi husababisha kifo.







## Tukio la 9
# Mwanamke Wa Kwanza

Baada ya Mungu kumpa mwanaume wa kwanza kazi ya kufanya na agizo la kutii, ulifika wakati wa kumuumba mwanamke wa kwanza.

> Bwana Mungu akasema, "Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."
>
> Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.
>
> Adamu akasema, "Sasa huyu ni mifupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume." (Mwanzo 2:18, 21-23)

Umeona aliyefanya upasuaji wa kwanza — na aliyeipanga ndoa ya kwanza? Ndiyo, alikuwa Mungu.

Mwanamke maana yake ni *Ametwaliwa katika Mwanamume*. Baadaye, Adamu alimwita mkewe jina lake Hawa, yaani *Mama wa wote*. Huku Mungu akiwapa majukumu tofauti, aliwafanya mwanaume na mwanamke kuwa na thamani inayolingana. Kama Adamu, Hawa aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Naye aliumbwa amjue Muumba na Mmiliki wake, aionyeshe tabia yake, na afurahie uhusiano naye wenye furaha milele.

> Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya sita.
>
> Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba. (Mwanzo 1:31; 2:2)

Kwa nini Mungu alistarehe siku ya saba? Kwa sababu alikuwa amemaliza kazi yake. Na kwa kuuumba ulimwengu wetu ndani ya siku sita na kustarehe siku ya saba, Mungu alianzisha wiki yenye siku saba — mzunguko wa kufanya kazi na kupumzika unaofanya kazi hata leo duniani kote.


BWANA Mungu aliwatunza Adamu na Hawa kama baba mwenye hekima na upendo. Kila jioni, alikuja bustanini kutembea na kuzungumza nao. Walifurahi na kustarehe kwenye uwepo wake.

> Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya. (Mwanzo 2:25)

Fikiria ulimwengu mkamilifu umekaliwa na familia kamilifu katika urafiki wa karibu na Muumbaji wao aliye mkamilifu. Mambo yalikuwa hivyo hapo mwanzoni.

Ni nini kilichoharibika?







# TUKIO LA 10
# UFALME WA NURU

Kabla hatujagundua kilichoharibika duniani, tunahitaji kufahamu mambo fulani ya mbinguni.

Ulimwengu huu mwingine, unaoitwa pia Paradizo, ni mahali penye nuru safi, rangi za kupendeza, muziki wa kuburudisha, mazungumzo ya kuridhisha, na siri zinazofichuka. Shughuli ndogo zaidi za mbinguni huzidi sana raha kuu za duniani. Mbinguni ni eneo jingine.

Mbinguni ni makao ya Mfalme.

Kivutio kizuri zaidi cha eneo hili la furaha ni Mfalme Mwenyewe. Kila pembe ya hilo jiji la mbinguni imesanifiwa kuonyesha fahari yake.

> Mji ule ulikuwa wa dhahabu safi, mfano wa kioo safi. (Ufunuo 21:18)

Maelezo ya mbinguni yaliyofafanuliwa zaidi yamo kwenye kitabu cha mwisho cha Maandiko yaani *Ufunuo*. Mungu alimpa nabii Yohana ufunuo wa mbinguni na akamwambia aandike alichokiona.

> … Na tazama, kiti cha enzi kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi juu ya kile kiti; … na upinde wa mvua ulikizunguka kile kiti cha enzi … Na katika kile kiti cha enzi kunatoka umeme na sauti na ngurumo … Mbele ya kile kiti cha enzi kulikuwa na mfano wa bahari ya kioo, kama bilauri.
>
> Nikaona nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi, … na hesabu yao ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu … hawapumziki …, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja.
> (Ufunuo 4:2-3, 5-6; 5:11; 4:8)

Maana ya malaika ni *mjumbe* au *mtumishi*. Malaika ni roho. Kama alivyo Muumbaji wao, malaika hawawezi kuonwa na mwanadamu, isipokuwa wakitumwa na ujumbe wanakohitajika kuonwa.

Mfalme wa mbinguni aliumba malaika kabla ya kuumba wanadamu. Kwenye kitabu chake, anatuambia kuwa, "wana wote wa Mungu walipiga kelele kwa furaha" (Ayubu 38:7) walipomwangalia akiuumba ulimwengu.

Mungu aliwapa malaika zake uwezo wa kumjua, kumtii, kumsifu, na kumtumikia milele. Malaika hawakuwa watumwa wa Mungu. Kama ilivyokuwa kwa wanadamu, Mungu hakuwalazimisha wamsujudie. Alitaka watumishi wenye furaha na utayari.

Maandiko husimulia ya malaika mmoja mwenye cheo cha juu ambaye Mungu alimpa akili, uzuri na uwezo wa kiwango cha juu.

Kama unazijua habari za malaika huyu, basi unajua uovu ulitoka wapi.







## Tukio la 11

# Ufalme Wa Giza

Lusiferi alikuwa mmoja wa malaika wakuu wa Mungu. Jina lake lina maana ya *Anayeng'aa*. Maandiko ya manabii humwelezea Lusiferi "wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri." (Ezekieli 28:12).[7]

Kisha Lusiferi alianza kujiangalia mwenyewe badala ya kumwangalia Muumbaji na Mfalme wake mkuu. Kwa mara ya kwanza kutokea, kilichoumbwa kikajivuna! Akipofushwa na uzuri na hekima yake mwenyewe, na kumsahau aliyemuumba, Lusiferi alisema moyoni mwake,

> "Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nitapanda mpaka mbinguni, Nitafanana na yeye Aliye juu." (Isaya 14:13-14)

Lusiferi alitaka awe mfalme. Alitaka *mapenzi yake* yafanyike badala ya mapenzi ya Mungu.

Dhambi iliuingia ulimwengu.

Lusiferi alishawishi theluthi ya malaika kuungana na uasi wake, lakini Mungu, asiyevumilia dhambi, aliwatupa nje ya makao yake ya mbinguni.

Jina la Lusiferi lilibadilika akawa Ibilisi, yaani, *mshitaki*. Anaitwa pia Shetani, yaani *mdanganyaji*. Malaika waovu huitwa mapepo.

Mahali pa siri penye giza, Mungu ameandaa jela ya shetani na mapepo yake. Sehemu ile inaitwa Jahanamu na Ziwa la Moto. Ni mahali pa kutengwa milele na Mungu, ambapo waasi hawatasumbua tena. Siku moja Shetani na mapepo yake yote watafungiwa milele kwenye jela hiyo, lakini bado hawajafungiwa.

Hivyo walikwenda wapi hawa roho wachafu baada ya Mungu kuwatupa nje?

Waliingia kwenye mazingira ya dunia. Huko shetani aliwapanga malaika zake kwa madaraja. *Kama hakuweza kutawala mbinguni aliweza kutawala duniani!* Ndiyo maana Andiko humwita Shetani "mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi" (Waefeso 2:2).

Shetani na mapepo yake hayaonekani kwetu, lakini yako kweli. Hata kama hatujui walivyo, tunalijua kusudi lao lenye giza na uovu. Watatumia namna zote za udanganyifu kuwafanya watu wajiunge na ufalme wao wa giza na maangamizi. Hawatakuacha hadi wamekuangamiza.

> Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. (2 Wakorintho 11:14)

> Mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. (1 Petro 5:8)

Sasa turudi nyuma kwenye simulizi la wazazi wetu wa kwanza.







# Tukio la 12

## Nyoka

Maisha ya Adamu na Hawa yalijawa na matukio na kusudi. Kila siku ilikuwa na la ajabu walipokuwa kwenye bustani yao kubwa, wakitunza viumbe na mimea yake, na kuonja vyakula vyake.

Kila jioni ilikuwa hata ya ajabu zaidi Muumbaji na Mmiliki wao alipowaheshimu kwa kuwatembelea yeye binafsi. Walifurahia mno kutembea na kuzungumza naye! Mwanaume huyo na mkewe walikuwa na furaha kwenye makao yao bustanini.

Lakini Shetani hakufurahi. Alimchukia Mungu na aliwachukia viumbe hawa wawili walioakisi mfano wa Mungu!

Kwa hiyo Shetani, aliyeshindwa kuutwaa ufalme wa mbinguni, alipanga kuutwaa ufalme wa dunia. *Akiweza tu kumsababisha Adamu, mkuu wa uzao wa wanadamu, achague kulivunja agizo la Mungu. Lakini hakumjaribu Adamu moja kwa moja …*

Siku moja Hawa alisikia sauti.

Hakuwa Adamu. Hakuwa Mungu.

Alikuwa nyoka!

Kwa Hawa, mtambaazi wa kuzungumza alikuwa tu uvumbuzi mwingine. Hakuwa na wazo kuwa adui wa Mungu alikuwa anamtumia nyoka. Wala hakujua kuwa Shetani alitaka kumtumia kumjaribu Adamu avunje agizo la Mungu.

Nyoka alikuwa amestahimili akingoja, macho yake yakimfuatia mwanamke kwa mahesabu. Kisha, kwenye wakati mzuri, alimfanyia ishara ya kumwita mwanamke na kusema,

> "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustani?"
> (Mwanzo 3:1)

Shetani alitaka Hawa alitilie mashaka neno la Mungu. Alimtaka pia afikiri kuwa Mungu alikuwa akiwazuilia yeye na mume wake kitu chema.

> "Mwanamke akamwambia nyoka, 'Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula, lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.'"
>
> Nyoka akamwambia mwanamke, "Hakika hamtakufa, kwa maana Mumgu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."
> (Mwanzo 3:2-5)

Hawa angelifanya nini?







# Tukio la 13
## Uchaguzi

Mungu alikuwa amewapa Adamu na Hawa uhuru wa kuchagua kati ya kufanya mapenzi yake au mapenzi yao.

BWANA alijua kilichokuwa bora zaidi kwa hawa viumbe maalum aliowaumba kwa mfano wake mwenyewe. Aliwataka Adamu na Hawa wamwamini, hata kama hawakuelewa sababu za agizo lake.

Ni Mungu pekee aliyeweza kuyatambua matokeo ya kutisha ya uovu huko mbeleni, ndiyo maana alimwambia Adamu mapema,

> "Matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." (Mwanzo 2:16-17)

Lakini sasa nyoka alikuwa amemwambia Hawa,

> "Hakika *hamtakufa*." (Mwanzo 3:4)

Hawa alipaswa kumtii nani — Muumbaji wake, au kiumbe?

Hili ndilo lililotokea:

> Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala,
>
> Akampa na mumewe, naye akala. (Mwanzo 3:6)


Mwanamke alikula! Mwanamume alikula!

Hawa alikula tunda walilokatazwa kwa sababu alidanganywa na udanganyifu wa Shetani. Adamu alikula kwa sababu alichagua kwa makusudi kufuata njia yake mwenyewe kuliko njia ya Mungu.

Badala ya kunyenyekea kwa Muumbaji wao mtakatifu na mwenye upendo, mwanadamu akasalimu amri kwa adui.

Wazazi wetu wa kwanza walitenda dhambi.







# Tukio la 14
## Dhambi Na Aibu

Adamu aliteuliwa kuwa mkuu wa wanadamu. Ni yeye aliyeagizwa na Mungu asile tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Adamu alipokula tunda alilokatazwa ndipo yeye na mke wake walipoanza kuyaona madhara ya uchaguzi wao.

> Wakafumbuliwa macho wote wawili, wakajijua kuwa wa uchi; wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo. (Mwanzo 3:7)

Aibu kubwa na hatia iliyochoma mioyoni mwao vilifurika kwenye nafsi zao. Walijisikia kuwa ni wachafu ndani na nje.

Dhambi ilileta aibu.

Kabla ya Adamu na Hawa kuvunja agizo la Mungu, walimtambua Mungu na, "wala hawakuona haya" (Mwanzo 2:25). Waliheshimika kuwa na Muumbaji wao, kuakisi mfano wake, na kuwa rafiki Zake.

Lakini walipokula matunda mti wa ujuzi wa mema na mabaya, walijitambua na kuaibika.

Aibu ilisimama badala ya heshima.

Walijaribu kuifunika aibu yao kwa majani ya mtini, lakini juhudi zao wenyewe hazikumaliza tatizo. Hawakuwa na msaada wa kuiondoa dhambi iliyovamia nafsi zao. Hawakuwa na msaada wa kuirudisha heshima waliyokuwa wamepoteza.


Ilikuwa mchana.

Hautapita muda Muumbaji wao aliye mtakatifu na mwenye upendo aje kwa matembezi yake ya jioni. Wazo la kumwona lilituma mawimbi ya mshituko wenye kitisho yakifukuzana miilini mwao.

Atasema nini kwao?

Watasema nini Kwake?







# Tukio la 15
## Wamekufa Kiroho

Kabla ya kumwasi Mungu, Adamu na Hawa walifurahia kumwona Mfalme na Rafiki yao kila alipokuja kuwatembelea.

Sasa wakawa wameogopa.

> Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone. (Mwanzo 3:8)

Kama watoto wasiotii wanaojaribu kujificha wazazi wao wasiwaone, Adamu na Hawa walijaribu kujificha Muumbaji wao asiwaone.

> BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia, "Uko wapi?"
>
> Akasema, "Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha."
>
> Akasema, "Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?"
>
> Adamu akasema, "Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala."
>
> BWANA Mungu akamwambia mwanamke, "Nini hili ulilolifanya?"
>
> Mwanamke akasema, "Nyoka alinidanganya, nikala." (Mwanzo 3:9-13)

Kwa nini Adamu na Hawa walitaka kujificha Mungu asiwaone? Kwa sababu walikuwa wametenda dhambi. Kwa nini waliwalaumu wengine kwa dhambi yao? Kwa sababu waliona aibu.

Adamu na Hawa hawakuuonyesha tena mfano mtakatifu wa Mungu. Badala ya kuakisi utakatifu na upendo wa Muumbaji wao, sasa waliakisi uasi wa shetani na majivuno yake.

Hao wawili wa kwanza walikuwa kama tawi lililovunjika kwenye mti ulio hai. Dhambi yao iliuvunja uhusiano wao na Mfalme wa ulimwengu.

Kiroho, walikuwa wamekufa. Dhambi yao ilikuwa imewatenga na chanzo cha uzima wa milele.

Kimwili, walikuwa bado hai, lakini mchakato wa kuzeeka ulikuwa umeanza. Nguvu ya mauti ilikuwa imevamia miili yao.

Na chanzo cha hivi vifo na uharibifu kilikuwa nini?

Dhambi.







## Tukio la 16

# Laana

Mwanzoni mwa historia ya wanadamu Mungu na wanadamu walikuwa pamoja. Amani na furaha vilitawala. Kisha mwanadamu alivunja agizo la Mungu.

Siku ile ile Adamu na Hawa walipotenda dhambi, Mungu alitangaza baadhi ya matokeo ya dhambi yenye athari nyingi.

Akamwambia mwanamke,

> "Kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala." (Mwanzo 3:16)

Kabla ya dhambi kuingia kwenye tukio, Hawa alifurahia upendo na uangalizi wa mumewe usio na choyo, lakini sasa asili zao zilizoathiriwa na dhambi zilileta machafuko na uchungu kwenye furaha ya ndoa.

Akamwambia Adamu,

> "Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako. Michongoma na miiba itakuzalia … Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi." (Mwanzo 3:17-19)

Kwa sababu ya dhambi yao, Adamu na Hawa waliipoteza miliki juu ya nchi. Sasa ulimwengu wao ukajumuisha miiba, uchungu, huzuni, magonjwa , na kifo.

Baadhi yetu tumelizoea sana balaa hili hata tunalikubali kama jambo la kawaida. Lakini huo ulikuwa mpango wa Mungu tangu asili maua kuwa na miiba? Au furaha ya kuzaliwa mtoto kuwa uchungu mkali? Au walioumbwa kwa mfano wa Mungu kuzeeka na kufa? La. Mungu hakuusanifu uumbaji wa asili upigane wenyewe. Dhambi ya mwanadamu ndiyo iliyosababisha dunia kuwa chini ya laana ya Mungu.

Mwanadamu alifanya dhambi hivyo lazima afe. Sheria ya dhambi na mauti iliamuru hilo.


Kifo ni kutengwa. Dhambi huleta kutengwa aina tatu:

1. Kifo cha Kiroho: Roho ya mwanadamu imetengwa na Mungu.
2. Kifo cha Kimwili: Roho na nafsi ya mwanadamu kutengwa na mwili wake (kadhalika kutengwa na wapendwa wake).
3. Kifo cha Milele: Roho, nafsi na mwili wa Mwanadamu kutengwa milele na Mungu kwa kutupwa kwenye ziwa la moto.[8]

Mwanadamu hakuwa na njia ya kujiokoa mwenyewe kutoka kwenye laana ya dhambi.

Lilikuwako tumaini lo lote?







# Tukio la 17
## Ahadi

Shetani alikuwa ameiba tunu maalum ya Mfalme, lakini Mfalme alikuwa na mpango wa siri wa kuirudisha kwa gharama. Kwa kuwa gharama ya kukombolea aliyopanga Mfalme kulipa ingekuwa ya juu isivyowazika, si mapepo wala wanadamu ambao wangeweza kuuelewa mpango wake hadi utakapotimizwa.

Siku ile ile Shetani aliwateka nyara wanadamu, Mungu alimwambia nyoka,

> "Kwa sababu umefanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako." (Mwanzo 3:14)

Mungu alipowaumba nyoka walikuwa na miguu. Kwa kuwa nyoka alitumiwa na Shetani kusababisha wanadamu watende dhambi, Mungu alimlaani aende kwa tumbo. (Ulijua kuwa majoka yana alama ndogo chini ya ngozi ambapo wakati fulani ilikuwa wawe na miguu?) Kwa kuwafanya nyoka wawe chini ya hayawani wote, Mungu aliwapa jamii ya wanadamu ukumbusho kuwa, kwa wakati wake atamponda kichwa yule "nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote" (Ufunuo 12:9).

Kisha Mungu akamwambia Shetani aliyemtumia nyoka,

> "Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino." (Mwanzo 3:15)

Huu ulikuwa wa kwanza kati ya unabii mwingi ambamo Mungu, hatua kwa hatua, alifunua mpango wake wa siri wa kuwaokoa watu kutoka kwa Shetani, dhambi, na kifo. Shetani na wafuasi wake hawakuujua mpango huo, maana Mfalme aliuweka unabii huo kifumbo.

Mungu aliahidi kutuma Mwokozi duniani — *uzao wa mwanamke*. Mwokozi awe na mama mwanadamu, lakini baba si mwanadamu. Ajulikane kama Masihi, kwa maana ya *Mteule*. Shetani amponde Kisigino Masihi, lakini Masihi amponde kichwa Shetani.


Haya yote yalikuwa na maana gani? Baadaye Mfalme aliweka wazi, lakini wakati huo Mungu alikuwa amewapa Adamu na Hawa tumaini.

Maelfu ya miaka baadaye mmoja wa manabii wa Mfalme aliandika,

> Watu wale waliokwenda katika giza wameona nuru kuu … Bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli — 'Mungu pamoja nasi'. (Isaiah 9:2; 7:14; Mathayo 1:23)

Mfalme ataikomboa tunu yake maalum.[9]
Lakini itagharimu kiasi gani?







## Tukio la 18
## Sadaka Ya Kwanza

Unakumbuka walichofanya Adamu na Hawa baada ya kula tunda walilokatazwa? Walijifanyia nguo za majani ya mti.

Nguo zao hizo ziliwafanya wajisikie vizuri mbele ya Muumba na Mhukumu wao? La! Walijisikia kuwa na aibu na hatia. Hawakuwa na njia ya kujiweka sawa kwa Mungu.

Hivyo Mungu alifanya jambo kwa ajili yao.

> BWANA Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.
> (Mwanzo 3:21)

Ni nani aliyeanza kutoa sadaka ya mnyama? Ni Mungu.

BWANA alichinja wanyama, akafanya nguo na kuwavika Adamu na Hawa. Kwa kufanya hivi, Mungu alikuwa akiwafundisha masomo ya msingi kuhusu haki, huruma na neema.

Hebu tuyafikirie haya maneno matatu muhimu.

> *Haki*. Waangalie wanyama waliouawa, Kwa nini Mungu aliwatoa sadaka? Hakuwaonyesha Adamu na Hawa kuwa lazima sheria ya dhambi na mauti isitishwe. Dhambi yao lazima iadhibiwe kwa kifo. Hiyo ndiyo haki.
>
> *Huruma. Waangalie Adamu na Hawa. Mungu aliwaua?* La. Mungu alitoa wanyama wafe badala yao. Hii ilikuwa njia ya Mungu ya kuadhibu dhambi yao bila ya kuwaadhibu wao wenyewe. Hiyo ndiyo huruma.
>
> *Neema. Sasa angalia nguo nzuri za Adamu na Hawa.* Wavunja maagizo hawa walistahili zawadi hi? La, lakini Mungu aliwaonyesha wema kwa kuwavika ngozi za wanyama waliotolewa sadaka. Hiyo ndiyo neema.
>
> Kwa sababu ya kile alichowafanyia BWANA, Adamu na Hawa walifurahia kuwa tena na Mungu!

Damu ya wanyama wale ilifunika *dhambi* yao. Adamu na Hawa walistahili kufa siku ile, lakini wanyama wasio na hatia walikufa badala yao.


Nguo za ngozi za wanyama hao zilifunika *aibu* yao. Mara nyingine tena Adamu na Hawa walijisikia vizuri kwenye uwepo wa Mungu.

Maelfu ya miaka baadaye mmoja wa manabii wa Mungu aliandika,

> Nitafurahi sana katika BWANA, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki.
> (Isaya 61:10)

Ni Mungu pekee mwenye njia ya kumweka sawa tena mwenye dhambi.







## Tukio la 19
# Wamefukuzwa

Mungu alipowafukuza malaika waasi kutoka mbinguni, maangamizi yao yalitiwa muhuri. Roho hizi zilizowahi kuishi kwenye nuru ya mbinguni hazikuwa na udhuru kwa dhambi yao. Lakini kwa wanadamu walioathiriwa na dhambi, BWANA alikuwa na mpango wa kuwarudisha wakimtumaini.

Pamoja na hayo, dhambi ina matokeo yake. Kama Mungu alivyowafukuza Lusiferi na malaika zake waovu nje ya paradizo ya mbinguni, kadhalika Mungu aliwafukuza Adamu na mkewe kutoka kwenye paradizo ya duniani.

> Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima. (Mwanzo 3:24)

Mti wa uzima ulikuwa mti mwingine maalumu katikati ya bustani. Ni wakamilifu tu walioweza kula matunda yake. Adamu na Hawa hawakuwa tena wakamilifu. Walifanya dhambi na lazima wazeeke na kufa.

Mungu wetu Muumbaji mkuu ni mtakatifu. Hivyo yeye ni mkamilifu, msafi, thabiti, na mwenye haki. Kwa sababu ya utakatifu na sheria zake takatifu, lazima aiadhibu dhambi kwa kifo — kutengwa na chanzo cha uzima.

Baadhi ya watu hufikiri kuwa Mungu ni mkuu kiasi cha kuweza kupuuza baadhi ya sheria alizoziamua mwenyewe. Fikiria mahakama ambapo hakimu anakataa kuzitiisha sheria za nchi. Utasema huyo ni hakimu *mkuu?* Fikiria mchezo wa mpira wa miguu ambapo mwamuzil mkuu hazifuati sheria za mchezo. Utamwita ni mwamuzi *mkuu?*

Shetani alitaka Hawa aamini kuwa Muumbaji wake hatayatiisha maagizo yake, kuwa hatawaadhibu kifo wavunjaji wa sheria. Lakini Mfalme na Mhukumu wa ulimwengu mwenye haki wakati wote hutimiza neno lake.

Mungu ni mkuu. Unaweza kumtumaini.

> Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako, Fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako. (Zaburi 89:14)

Ona kama unaweza kutegua kitendawili hiki: *Shetani na wanadamu wanaweza kufanya nini ambacho Mungu hawezi?*

Hapa kuna jibu la Mungu mwenyewe:

> "Mimi sitalihalifu agano langu; Sitabadili neno … Kwa utakatifu wangu hakika sitamwambia Daudi uongo." (Zaburi 89:34-35)

Mfalme wa ulimwengu hawezi kurudi nyuma kuhusu neno lake.







## Tukio la 20
# Watoto Wa Kwanza

Nje ya bustani, ulimwengu ulikuwa bado mzuri, ingawa ulijumuisha pia mambo mabaya kama miiba, wadudu wabaya na mwili wenye kuchakaa. Wanyama wengi tayari hawakuwa na urafiki tena. Haikuwa rahisi kupata chakula. Iliwabidi Adamu na Hawa watoke jasho ili waweze kujaza matumbo yao.

Walikuwa na nyakati za furaha pia.

> Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, "Nimepata mtoto mwanamume kwa BWANA." (Mwanzo 4:1)

Hawa akampa jina la Kaini lenye maana ya *miliki* mtoto wa kwanza duniani. Tunu kubwa kutoka kwa Mungu! Huenda alifikiri mtoto wake atakuwa Mwokozi aliyeahidiwa, lakini baadaye aligundua kuwa mtoto wake alikuwa mkorofi na mchoyo — kama wazazi wake tu!

Baadaye, mtoto wao wa pili alipozaliwa, Hawa alimwita jina lake Habili, yaani *ubatili*. Ni wazi kuwa Adamu na Hawa hawakuweza kuuleta *uzao wa mwanamke* wa kuwaokoa watu kutoka kwenye dhambi zao.

Badala ya kuakisi mfano mtakatifu wa Mungu, Uzao wa Adamu na Hawa unaakisi au kuonyesha asili zao zilizoelekea kwenye dhambi.

> Adamu … akazaa wana, waume na wake … kwa sura yake, kwa mfano wake. (Mwanzo 5:4,3)

Iangalie picha. Unamwona Kaini akimpokonya mdogo wake tikitimaji? Anatenda kama wazazi wake, waliochukua tunda lisilokuwa lao. Kama ugonjwa wa kuambukiza, dhambi ya Adamu na Hawa iliwaambukiza watoto wao.

> Adamu alipotenda dhambi, dhambi iliingia duniani. Dhambi ya Adamu ilileta kifo, hivyo kifo kilienea kwa kila mtu, "kwa sababu wote wamefanya dhambi". (Warumi 5:12 )

Methali ya Kiafrika inasema, *Uzao wa panya huchimba*. Methali ya Kiarabu hutamka ukweli ule ule: *Mtoto wa bata ni mwogeleaji*.


Wazazi wetu wa mwanzo walipotenda dhambi, walikuwa kama tawi lililovunjika kwenye mti. Kama kila kijiti na jani kwenye tawi lililovunjika vinavyoathirika, na kila uzao wa familia ya Adamu huathiriwa na dhambi ya Adamu.

Muda mrefu baada ya Adamu kufa, nabii Mfalme Daudi aliandika,

> Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu, Mama yangu alinichukua mimba hatiani. (Zaburi 51:5)

Tunaweza tusilifurahie hili, lakini tunajua kuwa ni la kweli.







## Tukio la 21
# Wenye Dhambi Wanaabudu

Adamu na Hawa walikuwa na watoto wengi wa kiume na wa kike, lakini Maandiko huwalenga vijana wao wawili wa mwanzo.

> Habili alikuwa mchunga kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi. (Mwanzo 4:2)

Wote Kaini na Habili walikuwa wachapa kazi.
Wote walijua kuhusu Muumba wao.
Wote walitaka Mungu awakubali wao na ibada yao.
Wote walikuwa na tatizo lile lile: *dhambi*.

Si tu walizaliwa wakiwa na dhambi, waliishi kama wenye dhambi. Kila siku walifikiri, walizungumza, na kutenda kwa njia zisizoonyesha asili ya Mungu ya usafi na upendo. Kwenye kitabu chake, Mfalme wa ulimwengu hali hii huiita *dhambi*.

> Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. (Warumi 3:23)

Ilikuwako njia ya Mungu kuwasamehe Kaini na Habili na kuwatangaza kuwa ni wenye haki mbele zake? Ndiyo, lakini iwe ya gharama sana.

> Pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo (la dhambi). (Waebrania 9:22)

Sheria hiyo ya ulimwengu isiyoweza kuvunjika—sheria ya dhambi na mauti—lazima itekelezwe. Dhambi lazima iadhibiwe kwa kifo. Ndiyo maana njia ya Mfalme ya msamaha ilitaka malipo ya kifo. Huku mwenye dhambi akistahili kufa, Mungu aliikubali damu ya wanyama fulani, kama vile mwana-kondoo.

Alitakiwa mwana-kondoo asiye na ugonjwa au mikwaruzo au uchafu. Awe mwenye afya na msafi. Asiwe na kasoro.


Mwana-kondoo huyo alichinjwa na kuteketezwa kwa moto. Alikufa badala ya mwenye hatia. Mwana-kondoo yule alikuwa badala ya mwenye dhambi.

Siku moja ndugu hao wote wawili walileta matoleo kwa Mungu, lakini ni mmoja tu aliyeleta matoleo sahihi.

> Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, kama sadaka kwa BWANA.
>
> Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. (Mwanzo 4:3-4)

Unadhani ni sadaka gani aliyoikubali Mungu?







# Tukio la 22
## Sheria Ya Sadaka Ya Dhambi

Watazame hao ndugu. Kitazame wanachotaka kumtolea Mungu. Yatazame madhabahu.

Dhabahu lilikuwa jukwaa lililoinuliwa, kwa kawaida lilitengenezwa kwa mawe au udongo. Palikuwa mahali pa kifo. Madhabahu iliibeba sadaka juu kati ya mbingu na nchi, kati ya Mungu na mwanadamu. Kila kilichotolewa kiliteketezwa kwa moto.

Wakati wote Mungu hutetea haki lakini hutaka kuonyesha huruma. Atawezaje kuyafanya yote? Atawezaje kuiadhibu dhambi bila ya kumwadhibu mwenye dhambi?

Muda mwingi baada ya wakati wa Kaini na Habili, Mungu alimwambia nabii Musa:

> Uhai wa mwili u katika hiyo damu; nami nimewapa ninyi hiyo damu juu ya madhabahu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwani ni hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi. (Mambo ya Walawi 17:11)

> Kisha ataweka mkono wake juu ya kichwa cha hiyo sadaka ya kuteketezwa; nayo itakubaliwa kwa ajili yake, ili kufanya upatanisho kwa ajili yake. (Mambo ya Walawi 1:4)

Maana ya *upatanisho* ni nini? Unahusisha kulipa gharama ya fidia inayotakiwa ili dhambi ziweze kufunikwa, kuoshwa, na kusamehewa. Nyakati za Agano la Kale, Mungu aliwaambia watu kuwa ataikubali damu iliyomwagika ya mwana-kondoo, kondoo dume, mbuzi, fahali, na njiwa wasio na kasoro kama malipo kwa ajili ya dhambi zao. Damu hiyo italeta upatanisho — kuifunika dhambi — lakini tu hadi siku ile Mungu atakapotoa sadaka iliyo kamilifu kuilipa gharama halisi inayotakiwa na sheria ya dhambi na mauti.

Sasa mwangalie Kaini na kile anachotaka kumtolea Mungu. Amechagua matunda na maboga mazuri! Alitoka jasho hasa kuipata sadaka hii! Lakini haikuweza kufunika dhambi zake kwa sababu haikuwa na damu, haikuwa na malipo ya kifo.


Mwangalie Habili na sadaka yake. Tukio la kusikitisha! Mwana-kondoo amefungwa na anataka kuuawa. Unamwona Habili akiweka mkono wake kwenye kichwa cha mwana-kondoo? Kwa sababu Habili aliuamini mpango wa Mungu, Mungu alizichukua dhambi zote za Habili na kuziweka juu ya mwana-kondoo. Habili anamshukuru BWANA kuwa ingawa yeye anaistahili hukumu ya kifo, Mungu ataikubali damu ya mwana-kondoo ifunike dhambi.

Sheria ya dhambi iliwataka wenye dhambi wote wahukumiwe kifo, lakini Mungu, kwa haki na huruma yake, alikubali kifo cha mwana-kondoo badala yao. Mungu huiita hii "amri ya sadaka ya dhambi" (Mambo ya Walawi 6:25).

Hiyo amri ya sadaka ya dhambi ilimweka Habili huru kutoka kwenye sheria ya dhambi na mauti.

Lakini vipi kuhusu Kaini?







## Tukio la 23
## Kukubaliwa Na Kukataliwa

Unayaona madhabahu ya Kaini? Kuna nini juu yake? Mazao yanayonyauka. Sasa yaangalie madhabahu ya Habili. Kuna nini juu yake? Damu na majivu. Mungu aliwafikiriaje hawa ndugu wawili na ibada zao?

> BWANA akamtakabali Habili na sadaka yake, bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. (Mwanzo 4:4-5)

Hatuambiwi Mungu alivyoonyesha kibali chake kwa sadaka ya Habili na alivyoikataa sadaka ya Kaini.[10] Andiko linasema tu:

> Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake. (Waebrania 11:4)

Kwa sababu alimwamini BWANA na mpango wake, Habili alisamehewa na kushuhudiwa kuwa ana haki. Hii ilikuwa zawadi ya Mungu kwa Habili.

Mungu alimtwika mwana-kondoo dhambi za Habili. Mwana-kondoo alikufa badala ya Habili. Damu ya mwana-kondoo ilimwagwa na mwili wake ukateketezwa ukawa majivu. Hasira ya Mungu ya haki juu ya dhambi ilimwangukia mwana-kondoo badala ya kumwangukia Habili. Kwa nini Mungu alipendezwa na mwana-kondoo wa Habili aliyetolewa sadaka? Kwa sababu alimlenga Mwokozi ajaye ambaye siku moja atalilipa deni la dhambi ya ulimwengu.

Kwa sababu ya imani yake kwenye mpango wa Mungu Habili sasa alikuwa kwenye uhusiano mzuri na Mungu. Baadaye Habili, badala ya kutengwa milele na Mungu, alikwenda kuwa na Mungu ambaye sasa ni rafiki yake. Amri ya sadaka ya dhambi iliishinda sheria ya dhambi na mauti.


Kaini alimkaribia Mungu na maombi yake, lakini hakulitii agizo la Mungu linalosema kuwa dhambi lazima iadhibiwe kwa kifo. Kaini alikuwa mshika dini, lakini hakuwa na uhusiano sahihi na Mungu. Sheria ya dhambi na mauti iliendelea kuning'inia juu yake kama wingu lenye giza. Kama hakumwamini Mungu na mpango wake, hangeweza kamwe kumjua Mungu kama rafiki yake. Angemkaribia Mungu kama Mhukumu wake.

Baadhi ya watu hujaribu kumtetea Kaini kwa kusema, "Kaini alikuwa mkulima. Alileta alichokuwa nacho." Lakini Mungu hakutaka alichokuwa nacho. Kaini angeuza kiasi cha mazao kwa mmoja wa wana-kondoo wa Habili, au angeweka mkono wake juu ya mwana-kondoo wa Habili na kuabudu kwenye madhabahu yake.

Kaini alifanya nini?

Alitubu na kuja kwa Mungu na sadaka inayofaa?







# Tukio la 24
## Mauaji Ya Kwanza

BWANA aliikataa sadaka ya Kaini. Hata hivyo Mungu bado alimpenda na kumhimiza atubu.

Nini maana ya kutubu?

Tuseme unataka kusafiri hadi mji fulani. Ukiingia kwenye gari, unatambua umeingia kwenye gari usilokusudia. Unafanya nini? Unalikubali kosa lako, unatelemka kwenye gari hilo, na kupanda kwenye gari sahihi. Hiyo ndiyo maana ya kutubu.

Maana ya kutubu ni *kubadili mawazo yako; kuondoka kwenye kosa na kunyenyekea kwenye kweli*. Kutubu mbele za Mungu hakuna maana kuwa lazima nijiadhibu kwa dhambi zangu. Ni kuiona dhambi yangu kama anavyoiona Mungu.

Mungu alitaka Kaini atubu—aache kuamini njia yake mwenyewe na aamini na kufuata njia ya Mungu.

> Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana.
>
> BWANA akamwambia Kaini, Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde. (Mwanzo 4:5-7)

Kaini alikuwa na kiburi mno hakuweza kutubu. *Alikuwa ameaibishwa na nduguye! Alitaka aondoe aibu hii na arudishe heshima kwa njia yake mwenyewe!*

> Kaini akamwambia Habili nduguye, [Twende uwandani]. Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua.
>
> BWANA akamwambia Kaini, Yuko wapi Habili ndugu yako?
>
> Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?
>
> BWANA akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. (Mwanzo 4:8-10)

Nafsi na roho ya Habili ilikuwa pamoja na BWANA, lakini mwili wake ulirudi mavumbini hadi siku ya baadaye Mungu atakapoyabadilisha hayo mavumbi yawe mwili wa utukufu unaofaa kwa umilele.


Lakini kwa Kaini, Mungu alimpa nafasi nyingine ya kutubu, lakini alikataa.


> Kaini akatoka mbele za uso wa BWANA. (Mwanzo 4:16)

Akiwa na roho ya kuasi na kiburi, Kaini alikwenda mashariki akajenga mji. Yeye na mkewe walizaa watoto wengi. Wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wao ndio waliotengeneza vifaa vya chuma na vya muziki.

Uzao wa Kaini ulikuwa na akili nyingi, lakini hawakumjua BWANA.







## Tukio la 25
# Uvumilivu Na Hukumu

Vizazi kumi baada ya Adamu kutenda dhambi ya kwanza, Mungu alitoa taarifa hii ya kusikitisha kwenye familia ya wanadamu:

> Maovu ya wanadamu ni makubwa duniani na … kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote. (Mwanzo 6:5)

Lakini familia moja duniani bado ilimwamini Mungu.

> Lakini Nuhu alipata neema machoni pa BWANA.
>
> Mungu akamwambia Nuhu, "Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. Hivi ndivyo utakavyoifanya." (Mwanzo 6:8,13-15)

Safina hii kubwa yenye sakafu tatu, yenye urefu wa mara moja na nusu ya uwanja wa mpira wa miguu, ilikuwa na nafasi ya kutosha jozi moja ya kila myama na jozi saba za kila mnyama anayefaa kwa kutoa sadaka ya dhambi. Safina hiyo ilikuwa na nafasi ya kuingizia hewa na mlango mmoja mkubwa.

Kwa karne nzima, Nuhu aliijenga safina akiwa na mke wake, wana wake watatu na wake zao. Wakati akiijenga, Nuhu aliionya dunia kuhusu hukumu ya Mungu inayokuja, lakini watu walimdhihaki tu.

Mwishowe safina ilikamilika. Familia ya Nuhu iliisheheneza safina mahitaji. Mungu aliwaleta wanyama, reptilia, wadudu, na ndege. Ukawa mwonekano wa ajabu kuingia na kutulia maelfu ya viumbe kila kimoja kwenye sehemu yake!

Nuhu na familia yake nao waliingia. Kuna mwingine yeyote aliyeingia kwenye eneo hilo la usalama? La. Mungu aliufunga mlango. Mawingu yenye hasira yaliifunika dunia, radi zilipiga, na ngurumo ziligongana.

> Siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka. Mvua ikanyesha juu ya nchi, siku arobaini mchana na usiku. (Mwanzo 7:11-12)

Lilikuwa janga la asili baya zaidi katika historia. Isipokuwa nafsi nane zilizohifadhiwa kwenye safina, wanadamu wote waliangamia. Ulimwengu wenye kiburi, usioamini, uliitambua kweli ukiwa umechelewa.

Kumbukumbu za kijiolojia na watu wa kale huithibitisha taarifa hiyo ya kibiblia. Kuanzia kwenye jangwa la sahara hadi kwenye milima ya Himalaya, visukusuku vya meli viliweza kuchimbuliwa kwenye majangwa makuu na milima mikuu ya dunia.

Katika huruma yake Mungu ni mvumilivu, lakini katika haki yake ataihukumu dhambi.







## Tukio la 26
# Mwanzo Mpya

Kwa hiyo ilitokea nini kwa Nuhu na familia yake, na wanyama katika safina? Waliokoka kutoka kwenye hukumu ya Mungu.

> Mungu akamkumbuka Nuhu, na kila kilicho hai, na wanyama wote waliokuwamo pamoja naye katika safina; Mungu akavumisha upepo juu ya nchi, maji yakapungua. (Mwanzo 8:1)

Safina ile kubwa ilielea ikishuka, hatimaye ilitua kwenye mlima wa Ararati, mlima mkubwa wenye vilele viwili ulio Mashariki mwa Uturuki.

Mara tatu Nuhu alimtuma njiwa aone kama kuna nchi kavu. Mara ya kwanza njiwa yule alirudi tu. Mara ya pili alirudi kwa Nuhu akiwa na jani la mzeituni mdomoni. Mara ya tatu njiwa yule hakurudi. Alipata makao! Nuhu akajua ni wakati wa kutoka kwenye safina. Mwaka mzima ulikuwa umepita tangu kuanza kwa gharika.

Unajua jambo la kwanza alilofanya Nuhu baada ya familia yake na wanyama kutoka kwenye safina?

> Nuhu akamjengea BWANA madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. BWANA akasikia harufu ya kumridhisha … (Mwanzo 8:20-21)

Haki na huruma ya Mungu haikubadilika. Dhambi iliendelea kutaka malipo ya kifo. Ndiyo maana Nuhu alimwaga damu ya viumbe wasio na hatia na kuteketeza miili yao madhabahuni, imetundikwa kati ya mbingu na nchi, kati ya Mungu na wanadamu. Sadaka kama hizo zililmlenga Masihi asiye na dhambi ambaye angekuja siku moja duniani ayatoe malipo halisi kwa ajili ya dhambi.

Kisha, Mungu alitoa agizo kwa Nuhu na familia yake:

> "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi." (Mwanzo 9:1)

BWANA Mungu pia alifanya agano na dunia:


> "Mimi nauweka upinde wangu winguni, nao utakuwa ni ishara ya agano kati yangu na nchi … Wala maji hayatakuwa gharika tena kuwaharibu wote wenye mwili." (Mwanzo 9:13,15)

Kama ishara ya agano lake, Mungu aliuweka upinde wake wenye utukufu ulioenda juu kwenye anga lenye mawingu. Mungu aliahidi kuwa hataleta tena gharika la kuangamiza dunia nzima.

Upinde huo hutukumbusha kuwa, kama ni kuadhibu au kulinda, Wakati wote Mungu hutimiza ahadi zake.

Wakati wote.







## Tukio la 27
# Mnara Wa Majivuno

Hata wakiwa wamebarikiwa kuanza upya, ndani ya vizazi vichache walio wengi walimwacha BWANA na kugeukia njia yao wenyewe. Kwa mfano, Mungu aliwaagiza watu wasambae na wa "ijaze nchi" (Mwanzo 1:28; 9:1). Basi mwanadamu alifanya nini?

Andiko linatueleza.

> Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja.
>
> Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi tambarare katika nchi ya Shinari [Iraki ya leo]; wakakaa huko. Wakaambiana, "Haya, na tufanye matofali tukayachome moto."
>
> Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa.
>
> Wakasema, "Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote."
> (Mwanzo 11:1-4)

Badala ya kulitukuza jina kuu la BWANA, wajenzi wa mji huu walitaka watu wawasifu wao. Kama Shetani, walitawaliwa na roho ya majivuno na uasi.

Kwa kutaka kujenga mnara, "na kilele chake kifike mbinguni," walikuwa kama watu wa dini leo wanaotumaini kufika mbinguni kwa juhudi zao wenyewe. Kama Kaini, watu hawa walikuwa na dini, lakini waliipuuza njia ya Mungu ya msamaha na haki. Hawakumwamini Mungu na mpango wake.


Basi BWANA Mungu alisema,

> "Haya, na tushuke huko, tukawachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao."
>
> Basi BWANA akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; wakaacha kuujenga ule mji. Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo BWANA alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko BWANA akawatawanya waende usoni pa nchi yote. Mwanzo 11:7-9)

Kwa kuwapa kila familia au ukoo lugha tofauti, BWANA aliukomesha mradi wao wa ujenzi. Watu hawakuwa na la kufanya ila kuondoka Babeli na kuijaza nchi, kama Mungu alivyoagiza.

Watu hawakuumaliza mnara wao,
lakini mipango ya Mungu iliendelea kama ilivyopangwa.







# Tukio la 28
## Mungu Anamwita Ibrahimu

Vizazi kumi vilipita tangu wakati wa nabii Nuhu. Shetani alikuwa ameyakamata mataifa, au ilielekea hivyo.

Badala ya kumwamini BWANA watu waliamini dini zao. Baadhi ya mataifa waliliabudu jua badala ya yule aliyeliumba. Wengine waliabudu mwezi.

Ilikuwa kama mwaka wa 1925 k.K.

Kwenye nchi moja kaskazini mashariki ya Arabia aliishi mzee aliyeitwa Abramu. Baadaye Mungu alilibadilisha jina akamwita Ibrahimu, yaani *Baba wa mataifa mengi*.

Umri wa Ibrahimu ulikuwa miaka 75 na wa Sara mkewe ulikuwa 65, bila ya mtoto. Wazazi na majirani wao walikuwa waabudu miungu, waliabudu viumbe badala ya Muumba.

Siku moja BWANA alimwambia Ibrahimu,

> “Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha.
>
> “Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki na kulikuza jina lako; na uwe Baraka; nami niitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.”
>
> (Mwanzo 12:1-3)

BWANA alitaka afanye agano na Ibrahimu. Akiiacha nyumba ya baba yake aende kwenye nchi isiyojulikana, basi BWANA amfanyie Ibrahimu mambo makuu mawili:

1. Mungu amfanye Ibrahimu kuwa baba wa taifa kubwa.
2. Kupitia hilo taifa jipya Mungu awabariki watu wa kila taifa.

Ibrahimu akimwamini na kumfuata BWANA, awe baba wa taifa ambamo watakuwamo manabii, yatakuwamo Maandiko, na atakuuwamo Mwokozi wa ulimwengu.


Ibrahimu alifanya nini?

> Kwa imani alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. (Waebrania 11:8)

Haikuwa rahisi kwa Ibrahimu na mkewe kuacha jamaa zao na kuiacha dini ya familia. Lakini walichagua kustahimili kukosolewa na jamii wakamfuata Mungu mmoja wa kweli.

Kumwamini na kumtii Mungu si rahisi wakati wote, lakini ni bora zaidi wakati wote.







# Tukio la 29
## Mtunza Ahadi

Ibrahimu na mkewe walikuwa wazee na bila ya mtoto. Hata hivyo BWANA alimwahidi Ibrahimu kuwa atakuwa baba wa taifa kubwa .

Ibrahimu alijibuje kuhusu ahadi ya Mungu ambayo "haiwezekani"?

> Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu. (Yakobo 2:23; Mwanzo 15:6)

Kama uzao wote wa Adamu, Ibrahimu alikuwa mwenye dhambi, lakini kama Habili na Nuhu, Ibrahimu alitoa sadaka ya dhambi kwa Mungu. Kwa kuwa Ibrahimu alimwamini Mungu na ahadi zake, Mungu alimhesabia Ibrahimu kuwa ana haki mbinguni, na akampa zawadi ya uzima wa milele. Sara naye alimwamini BWANA, na Mungu alimhesabu naye kuwa mwenye haki.

Lakini ni vigumu kusubiri.

Baada ya kuwa kwenye nchi ya Kanaani miaka kumi, wakitumaini na kuomba Sara apate mimba, waliamua "kumsaidia" Mungu kutimiza ahadi yake ya kumpa Ibrahimu mwana. Akifuata mila ya kwao, Sara alimpa Ibrahimu mjakazi wake Mmisri Hajiri. Alilala na Hajiri, naye akapata mimba na kuzaa mwana. Walimwita Ishmael.

Kama miaka 13 baadaye, Ibrahimu alipokuwa wa miaka 99 na Sara 89, Mungu Mwenyezi aliwatokea tena. Aliwaambia kuwa watapata mwana na watamwita jina lake Isaka. BWANA alimwambia pia Ibrahimu,

> "Na kwa habari za Ishmaeli …. nimembariki … Bali agano langu nitalifanya imara kwa Isaka, ambaye Sara atakuzalia majira kama haya mwaka ujao." (Mwanzo 17:20-21)

Mwaka mmoja baadaye, Sara alimzaa Isaka, yule mwana wa ahadi.


Iangalie picha. Unamwona Ibrahimu na mkewe wakiangalia angani usiku? Wanamshukuru BWANA kwa uaminifu wake. Baadaye, Hajiri na Ishmaeli walifukuzwa, lakini Mungu alikuwa mwema kwao pia.

> Mungu akawa pamoja na huyo kijana, naye akakua, akakaa katika jangwa, akawa mpiga upinde. Akakaa katika jangwa la Parani; mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri. (Mwanzo 21:20-21)

Ishmaeli akawa baba wa Waarabu wenye nguvu, ambao Mungu amewabariki kwa namna nyingi sana.

Na Isaka alibaki nyumbani, akiangalia mifugo ya baba yake. Wakati mwingine Isaka alimsaidia baba yake kuchagua mwana-kondoo mwenye afya njema, kumchinja, na kumteketeza kwenye madhabahu kwa ajili ya dhambi zao. Lakini si Isaka wala baba yake, hakuna aliyefikiria ni sadaka gani Mungu alikuwa anakaribia kuagiza.







## Tukio la 30
# Jaribu Kuu

Mungu alipanga kumtumia Ibrahimu na mwanawe kuuonyesha ulimwengu unabii na picha za mpango wake wa kuwakomboa wanadamu kutoka kwenye dhambi na mauti. Mungu pia alipanga kujaribu imani ya Ibrahimu kwa namna ya kupita kiasi akimtaka afanye jambo la kutia hofu, ambalo halikuleta maana hadi lilipopita.

Kwenye hatua hii Ibrahimu alikuwa na imani kamili kwa BWANA. Ibrahimu alimjua Mungu. Ibrahimu alitambua kuwa Mungu ni mwema na mwenye haki. Hata hivyo, Ibrahimu aliweza kumwamini na kumtii Mungu, hata kama alichomtaka afanye kimeonekana kuwa si sawa?

Hapa kuna habari za moja kwa moja kutoka kwenye Maandiko:

> Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu.
>
> Akamwambia, “Ee Ibrahimu!” Naye akasema, “Mimi hapa.”
>
> [Kisha Mungu] Akasema, “Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria,[11] ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia.”
>
> Ibrahimu akaondoka alfajiri, akatandika punda wake, akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Mungu.
>
> Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake, akapaona mahali pakali mbali. Ibrahimu akawaambia vijana wake, “Kaeni ninyi hapa pamoja na punda, na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena.”
>
> Basi ibrahimu akazitwaa kuni za hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe; akatwaa moto na kisu mkononi mwake, wakaenda wote wawili pamoja.
>
> Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, “Babangu!”
>
> Naye akasema, “Mimi hapa, mwanangu.”
>
> Akasema, “Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo wa sadaka ya kuteketezwa?”
>
> Ibrahimu akasema, “Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu.”
>
> Basi wakaenda wote wawili pamoja. (Mwanzo 22:1-8)







## Tukio la 31
# Mwana Aliyehukumiwa

Ulisikia kile Ibrahimu aliwaambia watumishi wake, kabla yeye na mwanawe kuupanda mlima wa kutolea sadaka?

> "Tukaabudu, na kuwarudia tena."

Mwana wa Ibrahimu angewezaje *kuwarudia* kama anakwenda kuuawa na mwili wake uteketezwe kwa moto? Andiko linasema,

> Akihesabu ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kuzimu.
> (Waebrania 11:19)

Mungu aliahidi kumfanya Isaka awe baba wa taifa jipya (kupitia hilo aje Mwokozi aliyeahidiwa). Mungu hawezi kusema uongo. Kwa Ibrahimu, hilo lilitosha.

Wakati huo huo, Isaka alikuwa akifikiri nini? Alijua ni mwenye dhambi na kuwa anastahili kufa kwa dhambi zake. Alijua pia kuwa Mungu atakubali kipatanisho. *Lakini leo wanakwenda kwenye eneo la kutolea sadaka bila ya kondoo wala mwana-kondoo? Haikuleta maana!* Hivyo Isaka akamwambia baba yake,

> "Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?"
>
> Ibrahimu akasema, "Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu."

Sasa tuendelee na simulizi.

> Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.
>
> Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe.
>
> Ndipo malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni, akasema, "Ibrahimu! Ibrahimu!"
>
> Naye akasema, "Mimi hapa."
>
> "Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee."
> (Mwanzo 22:9-12)


Ibrahimu na mwanawe walifurahi, lakini vipi kuhusu sadaka inayotakiwa?

> Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka.
> (Mwanzo 22:13)

Mwana wa Ibrahimu aliepushwa ile hukumu ya kifo.

Mungu alitoa mbadala!







TUKIO LA 32

## MIFANO NA UNABII

Mungu alimwokoaje mwana wa Ibrahimu aliyehukumiwa? Alitoa mnyama asiye na kasoro, asiye na hatia, afe badala yake.

> Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. (Mwanzo 22:13)

Matukio haya yote yalionyesha mfano wa mpango wa Mungu wa kumtuma duniani Mwokozi mtakatifu atakayekidhi matakwa ya sheria ya dhambi na mauti, na kuwaokoa wenye dhambi wa kila taifa duniani.

> Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama watu wasemavyo hata leo, "katika mlima wa BWANA itapatikana." (Mwanzo 22:14)

Kwa nini Ibrahimu aliuita mlima ule *BWANA* ***Atatoa*** badala ya *BWANA* ***Ametoa****?*

Mungu hakutoa komboleo?

Kwa kuuita mlima *BWANA* ***Atatoa***, nabii Ibrahimu alikuwa akiitabiri siku ambapo kwenye mlima huu huu, Mungu mwenyewe atatoa sadaka kwa damu ya thamani sana kiasi cha yeye kuikubali kama malipo kamili kwa deni la dhambi ya ulimwengu, ili kila anayeiamini sadaka hiyo asipotee bali awe na uzima wa milele.

Miaka 1,900 baada ya nabii Ibrahimu kutoa kondoo madhabahuni, Mwokozi mwenye aliyetabiriwa aliangalia nyuma kwenye tukio hili la kihistoria na kusema,

> "Ibrahimu baba yenu alishangilia kwa vile atakavyoiona siku yangu; naye akaiona, akafurahi." (Yohana 8:56)

Moshi wa yule kondoo ulipopanda kuelekea mbinguni, Mungu alimpa kidokezo cha sadaka ya kuteketezwa itakayotolewa kwenye mgongo wa mlima huu huu. Ghafla jibu la Ibrahimu kwa swali la mwanawe "yuko wapi mwana-kondoo?" lilichukua maana yenye kina zaidi.

> "Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu." (Mwanzo 22:8)

Kwa Ibrahimu na mwanawe, Mungu alikuwa hajatoa bado mwana-kondoo. Alitoa kondoo mume.

Alikuwa wapi *mwana-kondoo?*

Wakati ufaao Mungu atatoa jibu.







## Tukio la 33
# Mungu Mwaminifu Na Mtakatifu

Unazikumbuka ahadi kuu mbili ambazo BWANA alimpa Ibrahimu? Kwanza Mungu alisema:

> "Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa." (Mwanzo 12:2)

Mungu alitunza neno lake. Ibrahimu alimzaa Isaka, Isaka alimzaa Yakobo, na Yakobo aliwazaa wana12 ambao familia zao zilikuwa yale makabila 12 ya Israeli. Mungu pia alisema:

> "Katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa." (Mwanzo 12:3)

Mungu aliitunza pia sehemu hiyo ya ahadi yake. Kwa kufanya kazi na taifa hili maalumu — na linaloasi mara nyingi, Mungu alitaka awaonyeshe watu wote duniani alivyo, na wenye dhambi watakavyoweza kuja kwake. Mungu alipokuwa akilinda taifa hili, Alikuwa akilinda mipango yake ya kutubariki mimi na wewe — maana manabii, Maandiko Matakatifu, na Mwokozi aliyeahidiwa angekuja kutokea kwenye taifa hili.

Mpango wa Mungu wa siri ulikuwa ukisonga mbele.

Kama mwaka wa 1500k.K., Mungu alimwita Musa, wa uzao wa Ibrahimu, awe nabii wake. Musa aliandika vitabu vitano vya mwanzo vya Biblia. Mungu pia alimtumia Musa kuwaongoza wana milioni tatu wa Ibrahimu kutoka kwenye karne nne za utumwa. Mungu mwenyewe aliwaongoza wakalivuka jangwa hatari kwa nguzo ya wingu ya kuleta kivuli wakati wa mchana, na nguzo ya moto kutoa nuru wakati wa usiku. Kwa mkono wake ulio hodari, aliwafungulia njia awaokoe kwenye Bahari ya Shamu, aliwapa mana kutoka mbinguni na maji kutoka kwenye mwamba, na akawaleta kwenye mlima Sinai.

Chini ya huo mlima Mungu aliwaambia watu,

> "Nanyi mtakuwa kwangu ufalme … na taifa takatifu!" (Kutoka 19:6)

Mungu alitaka taifa hili liwe takatifu: lililotengwa kwa ajili yake na tofauti na mataifa yanayolizunguka. Lakini watu hawakuelewa ni nini kuwa watakatifu. Hawakujiona kuwa ni wenye dhambi wasio na msaada. Walidhani kwa namna fulani wangeweza kuutwaa upendeleo wa Mungu. Ili awafundishe somo kuhusu hasira yake inayowaka juu ya dhambi, BWANA alishuka kwa kitisho na moto uwakao na baragumu iliayo.

> Mlima wa Sinai wote pia ukatoa moshi, kwa sababu BWANA alishuka katika moto; na ule moshi wake ukapanda juu kama moshi wa tanuu, mlima wote ukatetemeka sana. Na hapo sauti ya baragumu ilipozidi kulia sana, Musa akasema, naye Mungu akamwitikia kwa sauti." (Kutoka 19:18-19)

Mungu alimpa Adamu amri moja.

Aliandaa kuwapa amri kumi taifa hili jipya.





## Tukio la 34
## Amri Kumi

Walio wengi kwenye taifa walidhani walikuwa wema vya kutosha kuwa watu wa Mungu. Hivyo BWANA aliwapa amri kumi, kwanza kwenye sauti yenye ngurumo kutoka kwenye mlima Sinai, kisha kwenye mbao za mawe.

Tuzisome amri hizo kumi (kwa kulia, zimefupishwa kutoka Kutoka 20).

Mungu alimwambia Musa kuwa lazima wazitii amri zote kumi kikamilifu.

> "Na alaaniwe asiyeyaweka imara maneno ya torati hii." (Kumbukumbu 27:26)

Unadhani watu walijisikiaje baada ya kuzisikia hizi amri kumi? Unafikiri bado walidhani walikuwa wema vya kutosha? Na wewe? Unadhani u mwema wa kutosha kuishi kwenye ufalme wa Mungu ulio mkamilifu?

Soma tena *amri namba moja*. Wakati wote unamweka Mungu kwanza? Kama sivyo, umeshindwa kuitimiza sheria hii. Isome *namba tano*. Kama umewahi kushindwa kumtii baba yako au mama yako, una hatia kwa Mungu. Sasa iangalie *amri ya nane*. Kama umewahi kuchukua kitu kisicho chako au umewahi kudanganya kwenye mtihani, umeivunja amri hii. Umewahi kusema uongo? Basi umeshindwa kutii *amri ya tisa. Amri ya mwisho* inatuambia ni makosa hata kutamani kuwa na kitu cha mwingine. Mungu huiona dhambi iliyomo mioyoni mwetu.

Ni dhambi ngapi zilizoharibu uhusiano wa Adamu na Hawa na Mungu? *Moja tu.* Kiwango kikamilifu cha Mungu hakijabadilika.

> Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. (Yakobo 2:10)

Mungu ni mtakatifu na hawezi kuiridhia dhambi. Utapendaje kushiri chumba kimoja na mzoga wa nguruwe uliooza? Ndivyo ilivyo dhambi yetu kwa Mungu. Kama kupulizia manukato kwenye mwili unaonuka kusivyoweza kusafisha chumba, kadhalika hakuna juhudi za kidini zinazoweza kusafisha mioyo yetu.


Kama kioo kinavyonionyesha uchafu usoni kwangu, ndivyo sheria ya Mungu inavyonionyesha dhambi moyoni mwangu. Kama vile kioo kisivyoweza kusafisha uso wangu, kadhalika amri kumi haziwezi kusafisha moyo wangu.

> Hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria. (Warumi 3:20)

Haijalishi tunavyoweza kudhani sisi ni wema, si wema wa kutosha kuishi na Mungu mbinguni.

Tunahitaji Mwokozi.







## Tukio la 35
# Mifano Zaidi

Amri Kumi zililipatia taifa hilo jipya kiwango dhahiri cha kuwa sahihi na kutokuwa sahihi. Hilo lilikuwa jambo jema. Lakini sheria ya Mungu pia ilileta habari mbaya. Iliwaonyesha watu kuwa walikuwa kwenye tatizo kubwa. Kwa sababu ya dhambi zao lazima wote wafe na kutengwa na Mungu.

Habari njema ni kuwa BWANA bado aliikubali damu iliyomwagika ya wana-kondoo, fahali, mbuzi, na njiwa kufunika dhambi zao. Hivyo, siku ile ile Mungu alipozitoa hizo amri zake kumi, Mungu alimwambia Musa,

> "Utanifanyia madhabahu … Nawe utatoa dhabihu zako juu yake."
> (Kutoka 20:24)

Unamwona Musa na mkono wake ukiwa kwenye kichwa cha mwana-kondoo? Unawaona watu wakielekeza mikono yao kwa mwana-kondoo? Kwa sababu wanamwamini Mungu na njia yake ya msamaha, dhambi zao zinawekwa juu ya mwana-kondoo asiye na hatia. Kisha mwana-kondoo yule alichinjwa madhabahuni. Damu iliyomwagika ilizifunika dhambi za watu. Kisha, mnyama huyo aliteketezwa kwa moto akawa majivu. Majivu yaliwaonyesha watu alichofanya Mungu kuhusu dhambi zao. Walikuwa wamesamehewa!

Lakini mtindo huu wa kutoa damu ya wanyama kwa ajili ya msamaha wa dhambi ulikuwa mfano tu wa alichotaka hasa Mungu.

> Basi torati … kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao. Kama ndivyo, je! dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?
>
> Lakini katika dhabihu hizo, liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka. Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.
> (Waebrania 10:1-4)


Wanyama hawakuumbwa kwa mfano wa Mungu.

Thamani ya mwana-kondoo haifanani na thamani ya mwanadamu. Kama vile ambavyo huwezi kupeleka gari ya bandia ya kuchezea watoto kwa muuza magari ukaitoe kama malipo ya gari halisi, kadhalika, damu ya mwana-kondoo haingeweza kulipia gharama inayotakiwa na sheria ya dhambi na mauti.

Ilihitajika sadaka iliyo bora zaidi.

Sadaka za wanyama hazikuweza kuondoa deni la dhambi ya ulimwengu, lakini ziliwapa wenye dhambi mfano wa yule anayeweza.







## Tukio la 36
# Unabii Zaidi

Ulipokuwa ukikaribia ujio wa Mwokozi, BWANA aliwaambia manabii wake waandike unabii zaidi[12] kuhusu Masihi-Mfalme. Hapa kuna baadhi ya huo unabii wa kale:

*Bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume …* — *Nabii Isaya 7:14*

*"Bali wewe, Bethlehemu … kutoka kwako atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala … matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele."* — *Nabii Mika 5:2*

*Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume … naye ataitwa jina lake Mshauri wa ajabu … Mungu mwenye nguvu … Mfalme wa amani.* — *Nabii Isaya 9:6*

*Mungu wenu atakuja … kuwaokoa. Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kurungu …* — *Nabii Isaya 35:4-6*

*Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjioni …* — *Nabii Isaya 53:7*

*"Wamenizua mikono na miguu."* — *Nabii Daudi. Zaburi 22:16*

Mwokozi aliyeahidiwa alikuwa anakuja!
Lakini lini? Na alikuwa nani?
Unabii huu ulitimia vipi?





# Sehemu Ya 2

## Mfalme atimiza mpango wake

— AGANO JIPYA —

## Tukio la 37
# Habari za Mfalme Zinaendelea

Uliifurahiaje sehemu ya kwanza ya kitabu cha Mfalme? Umejifunza nini kwenye Agano la Kale?

Maana ya agano ni *makubaliano*. Huko nyuma kabla ya Mungu kutoa Maandiko ya Agano Jipya, alisema,

> "Siku zinakuja … Nitakapofanya agano jipya." (Yeremia 31:31)

Kwenye agano la mwanzo na watu wake, Mungu aliiwapa maagizo mengi kuwaonyesha utakatifu wake na uovu wao. Aliwapa pia mifano mingi na unabii mwingi kuhusu Mwokozi ajaye. Kwenye agano la mwanzo manabii walitabiri: Masihi-Mfalme ata kuja. Lakini kwenye agano jipya tunasoma: Masihi-Mfalme *ame* kuja!

Agano Jipya lina *Injili*. Kwenye lugha ya Kiarabu inaitwa *Injil*. Maneno hayo yote yana maana ya *Habari Njema*. Injili huanza kwa maneno haya:

> Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu: Ibrahimu alimzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo … (Mathayo 1:1-2)

Jina kwa jina, Maandiko huorodhesha msurur wa majina usiokatika wa uzao kutoka kwa Ibrahimu hadi kwa Yesu. Mungu aliitunza ahadi yake ya kuyabariki mataifa yote kwa kumtuma Mwokozi kupitia uzao wa Ibrahimu.

Agano Jipya lina vitabu vinne vya injili. Kwa nini vinne? Kwa nini kisiwe kimoja tu? Kwenye Agano la Kale, Mungu alimwambia Musa,


> "Jambo na lithibitishwe kwa vinywa vya mashahidi wawili, au watatu." (Kumbukumbu 19:15 )

Kuzithibitisha habari zake na ujumbe wake, Mungu alichagua watu wanne, siyo tu wawili au watatu, waandike taarifa nne tofauti kuhusu maisha ya Masihi. Majina yao ni Mathayo, Marko, Luka, na Yohana. Kama waandishi wa habari wanne wanaoshughulikia tukio moja, kila mmoja anaelezea habari ile ile lakini kwa mitazamo tofauti.

Agano Jipya lina jumla ya vitabu 27. Kitabu cha Matendo, kilichoandikwa na Luka, kinaeleza kilichotokea baada ya Masihi kumaliza kazi aliyotumwa kuja kuifanya. Mungu aliwavuvia Paulo (aliyekuwa gaidi), Yakobo na Yuda (Ndugu wa Yesu kwa upande mmoja), na Petro na Yohana (wavuvi) kuiandika sehemu ya Agano Jipya iliyobaki. Kila kitabu hufunua zaidi na zaidi kumhusu Mfalme na mipango yake kwa ajili ya wote wanaompenda.

Sasa hapa kuna sehemu iliyobaki ya habari zake.







# Tukio la 38
## Habari Za Mariamu

Wakati ulifika. Baada ya maelfu ya miaka ya maandalizi, Mungu alikuwa njiani kumtuma duniani Mwokozi-Masihi-Mfalme aliyeahidiwa. Lakini alikuwa nani na atakuja kwa hali gani?

> Zamani za Herode, mfalme wa Uyahudi … malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi: na jina lake bikira huyo ni Mariamu.
>
> Malaika akamwambia, "Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake Atamiliki … ufalme wake utakuwa hauna mwisho."
>
> Mariamu akamwambia malaika, "Litakuwaje neno hili, maana sijui mume?"
>
> Malaika akajibu akamwambia, "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu." (Luka 1:5,26-27,30-35)

Kwa nini Gabrieli alimwita Yesu "Mwana wa Mungu"?

Baadhi hufikiri msemo huu una maana kuwa Mungu alioa na kuzaa mwana. Si kweli. Kama unatoka bara la Afrika, baadhi wanaweza kukuita "mwana wa Afrika". Ina maana Afrika ilioa ikazaa mtoto? La! Ni kuwa unatoka Afrika.

Masihi anaitwa Mwana wa Mungu kwa sababu alitoka kwa Mungu. Aliingia kwenye familia ya Adamu iliyoharibiwa na dhambi lakini haikuwa asili yake. Yeye ndiye Neno lenyewe, nafsi, na Mwana wa Mungu.

> Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.
>
> Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli. (Yohana 1:1-3,14 )

Unakumbuka ahadi aliyoitoa Mungu siku ile Adamu alipokula tunda alilokatazwa? Mungu alitangazaa kuwa *uzao wa mwanamke utamponda nyoka kichwa*.

Uzao huo ulioahidiwa sasa ulikuwa tumboni mwa huyo msichana bikira.

Atakavyomponda nyoka kichwa lilibaki kuwa jambo la kusubiri aje lionekane.







## Tukio la 39
# Habari Za Yusufu

Mariamu alikuwa ameposwa na Yusufu, fundi seremala aliyeishi Nazareti, mji ulio mpakani huko Palestina ya kaskazini.

Mariamu na Yusufu wote walikuwa Wayahudi, wa uzao wa Daudi, na kurudi nyuma hadi kwa Ibrahimu. Yusufu angeweza kuwa wa ukoo wa kifalme, lakini nchi yake, ilitawaliwa na Rumi. Askari wa Kirumi waliifanyia doria mitaa. Wayahudi walioshukiwa walikamatwa na kusulibiwa. Watoza ushuru waliwaibia watu, maisha yalikuwa magumu.

Lakini Yusufu alikuwa na msisimko. Hivi karibuni atamwoa Mariamu. Alijitahidi apate mahali pa kuishi na mkewe baada ya kufunga ndoa. Kisha siku moja aligundua jambo la kushitusha: Mariamu alikuwa na mimba.

Unadhani Yusufu alijisikiaje? Ilionekana kuwa Mariamu hakuwa mwaminifu kwake.

Yusufu alivunjika moyo, lakini alitaka kufanya jambo sahihi. Hivyo aliamua kuuvunja uchumba kimya kimya, kwa sababu hakutaka kumwaibisha Mariamu.

> Basi alipokuwa akiyafikiri hayo tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto.
>
> "Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."
>
> Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema: "Tazama! Bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi."
>
> (Mathayo 1:20-23)

Uchungu wa Yusufu uligeuka ukawa furaha. *Heshima kubwa mno! Mariamu awe mama wa Masihi aliyeahidiwa! Na Yusufu awe mlezi halali wa huyo mtoto!*

Huyu Masihi mtakatifu atakuwa na mama mwanadamu, lakini bila baba mwanadamu. Jina lake ataitwa Yesu, yaani, *BWANA huokoa* au tu *Mwokozi*.

> Naye Yusufu alipoamka katika usingizi, alifanya kama malaika wa Bwana alivyomwagiza; akamchukua mkewe; asimjue kamwe hata alipomzaa mwanawe; akamwita jina lake YESU. (Mathayo 1:24-25)

Ulikuwa mkono wa Mungu.







# Tukio la 40
## Ujio

Miaka mia saba ya nyuma, nabii Mika alitabiri kuwa Masihi-Mfalme atazaliwa Bethlehemu, mji wa Daudi wa asili.

Lakini kulikuwa na tatizo. Mariamu na Yusufu walikuwa wakiishi Nazareti, mwendo wa siku tatu kuelekea kaskazini. Maandiko yangetimizwaje?

Mungu aliyasimamia yote.

Muda ulipokaribia wa Mariamu kujifungua, Mfalme wa Kirumi Kaisari Augusto alitoa agizo la kila mmoja kurudi alikotoka ili akaandikishwe kulipa kodi. Hivyo Yusufu na Mariamu na ujauzito wake wakalazimika kusafiri kutoka Nazareti hadi Bethlehemu.

> Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia, akamzaa mwanawe, kifungua mimba.
>
> Akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori la kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni. (Luka 2:6-7)

Kwenye mji huo wa Bethlehemu uliojaa wasafiri waliochoka wakija kujiandikisha kwa kulipa kodi, *Mzao wa mwanamke* aliyeahidiwa alizaliwa. Injili inaliandika tukio hilo kwa usahihi:

> Akamzaa mwanawe, kifungua mimba. (Luka 2:6)

Upande wa mama yake, mtoto huyu alikuwa kifungua mimba wa kiume wa Mariamu, lakini upande wa baba yake, alikuwa Mwana wa milele wa Mungu. Neno yule yule ambaye Mungu alimtumia kuuumba ulimwengu, Sauti ile ile iliyounguruma kwenye mlima Sinai uliowaka moto, sasa iliweza kusikika ndani ya kilio laini cha mtoto.

Na alizaliwa wapi?

Si kwenye makao ya mfalme, si hospitalini, wala si kwenye nyumba ya wageni ya pembeni mwa njia. Mfalme aliyetoka mbinguni alizaliwa wanamozaliwa wana-kondoo — kwenye nyasi za kulishia wanyama, na hori kikawa kitanda chake.

Yote yalikuwa sehemu ya mpango wa Mungu.

> Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake. (2 Wakorintho 8:9)

Lakini Mungu hakuweza kufanya namna fulani ya sherehe kuheshimu kuwasili kwa Mwanawe?

Alifanya.







## Tukio la 41
## Habari Za Wachungaji

Mungu aliwajulisha akina nani kwanza habari za ujio wa Masihi duniani? Mfalme? Matajiri na watu mashuhuri? Viongozi wa kidini?

La.

Wa kwanza kuzipokea habari hizo za kusisimua walikuwa wachungaji maskini, wanaume waliokuza wana-kondoo wa kutoa sadaka kwenye madhabahu ya hekaluni huko Yerusalemu.

> Na katika nchi ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu.
>
> Malaika akawaambia, "Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo[13] Bwana. Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe."
>
> Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia!"
>
> Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, "Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalione hilo lililofanyika, alilotujulisha Bwana."
>
> Wakaenda kwa haraka wakamkuta Mariamu na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini.
>
> Walipomwona wakatoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto. Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji.
>
> (Luka 2:8-18)

Habari waliyotoa wachungaji ilikuwa ya ajabu!

*Mwokozi amezaliwa! Tulimwona! Tulimgusa! Malaika alituambia ndiye Kristo BWANA! Kwaya ya wingi wa malaika ililijaza anga! Usiku ulikuwa kama mchana! Masihi amekuja! Yuko hapa! Yuko hapa!*

Baadhi ya watu waliuamini ujumbe wa wachungaji. Walio wengi hawakukubali.

Lakini amini usiamini, Mfalme, ambaye siku ya kuzaliwa kwake kuliigawa historia ya dunia sehemu mbili,[14] alijiunga na wanadamu.

> Hata zilipotimia siku nane za kumtahiri, aliitwa jina lake Yesu, kama alivyoitwa na malaika kabla hajachukuliwa mimba. (Luka 2:21)







## Tukio la 42
## Habari Za Mamajusi

Baada ya Yesu kuzaliwa kwenye zizi, Yusufu alipanga kuwa na mahali pazuri pa kupumzikia familia yake ndogo.

Siku moja Mamajusi (wenye hekima ya kusoma nyota) walioshtushwa walifika Yerusalemu. Wakiongozwa na nyota maalum, watu hawa walitoka mbali huko Uajemi wakimtafuta Mfalme aliyezaliwa.


Wenye hekima hawa walikuwa na swali moja na kusudi moja:

> "Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia."
>
> Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye. Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari kwao, Kristo azaliwa wapi?
>
> "Nao wakamwambia, katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii …"
>
> Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani … akasema, "Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto, na mkiisha kumwona, nileteeni habari ili mimi nami niende nimsujudie."
>
> Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia, na tazama, ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto.
>
> Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno.
>
> Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu, mamaye wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane.
>
> Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.
>
> Na hao walipokwisha kwenda zao, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto, akasema, "Ondoka, umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize." (Mathayo 2:2-13)

Herode alijaribu kumwua mtoto. Watu wa Yerusalemu walimpuuza. Lakini Mamajusi, waliovuka jangwa linalochoma wakimtafuta, walimwabudu na kumpa zawadi anazostahili mfalme: dhahabu na uvumba na manemane ya thamani, maalum kwa kuhifadhia maiti. Kwa nini walimtolea na hiyo dawa ya kuhifadhia maiti?

Hawa wenye hekima walijua kuwa Yesu alizaliwa ili afe?







TUKIO LA 43

## MTOTO MKAMILIFU

Baada ya onyo la malaika, Yusufu alimchukua Mariamu na mtoto Yesu hadi Misri, ambako waliishi kama wakimbizi hadi kifo cha mfalme katili Herode.

> Hata alipofariki Herode, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri, akasema, "Ondoka, umchukue mtoto na mamaye, ushike njia kwenda nchi ya Israeli; kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto." (Mathayo 2:19-20)

Hili lilitimiza unabii mwingine wa zamani uliotabiriwa na BWANA:

> Nikamwita mwanangu atoke Misri. (Hosea 11:1)

Hivyo Yusufu na Mariamu walimpeleka mtoto Nazareti, alikokulia pamoja na ndugu zake wa upande mmoja.[15]

Kwa njia nyingi mtoto Yesu alikuwa kama watoto wengine. Alikula, alilala, alicheza, alichunguza, na kujifunza shughuli, lakini kwa njia zingine Yesu alikuwa tofauti na watoto wengine. Kamwe hakuwa mchoyo. Aliwatii wazazi wake wakati wote. Hakusema uongo kamwe. Wakati wote alimpendeza Baba yake wa mbinguni.

> [Alikuwa] Mtakatifu, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lo lote, aliyetengwa na wakosaji. (Waebrania 7:26)

Yesu ndiye mtoto mkamilifu pekee katika historia. *Mkamilifu* haina maana hakuwa na tofauti yo yote, ina maana alikuwa na asili ya ukamilifu. Utakatifu na wema kamili. Alikuwa mkamilifu pia katika uwezo na hekima, lakini kabla ya kuingia kwenye tumbo la Mariamu alijiwekea vikomo fulani ili aweze kuishi kama mwanadamu kati ya wanadamu.

> Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu. (Luka 2:52)


Yesu alipokuwa na umri wa miaka 12 alisafiri na wazazi wake kutoka Nazareti hadi Yerusalemu kwenye sikukuu ya kila mwaka ya kutoa sadaka, iliyojulikana kama Pasaka.[16] Huku watoto wenzake wakilichunguza jiji, Yesu aliitumia wiki ile akiwa hekaluni na waandishi wa sheria, akiwasikiliza na kuwauliza maswali.

> Nao wote waliomsikia walistaajabia fahamu zake na majibu yake. (Luka 2:47)

Hekalu ilikuwa mahali ambapo wana-kondoo waliteketezwa madhabahuni kwa ajili ya dhambi za watu. Mtoto Yesu aliyajua ambayo Waalimu hawakuyajua.

Alikuja kumtoa Mwana-kondoo wa mwisho.







# Tukio la 44
# Mwana-Kondoo Wa Mungu

Ilikuwa imepita miaka 30 tangu Yesu azaliwe Bethlehemu. Kaisari Augusto alikuwa amekufa; mwanawe wa kambo Kaisari Tiberius aliitawala himaya ya Kirumi. Herode Antipa alitawala Galilaya. Pontio Pilato alitawala Uyahudi. Na nabii mpya alikuwa akihubiri nchini Palestina.

> Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi na kusema, "Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."
>
> Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema: "Sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake.'"
>
> Naye Yohana mwenyewe alikuwa na vazi lake la singa za ngamia na mshipi wa ngozi kiunoni mwake; na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu. (Mathayo 3:1-4)

Huku watu wengi wa wakati wake wakivaa hariri safi na kula vyakula vizuri sana, Yohana aliishi kwa hali ya chini. Alikuwa kwenye wito.

Yohana alikuwa mtangulizi wa Mfalme.

Mamia ya miaka kabla, manabii wawili, Isaya na Malaki, waliandika kuhusu nabii ajaye atakayetangaza ujio wa Masihi-Mfalme. Nabii huyo ndiye Yohana.

Huku manabii wa nyuma wakitabiri: *Wakati ukifika Mwokozi aliyeahidiwa atakuja duniani,* Yohana alihubiri, *Wakati huo umefika. Mwokozi yupo hapa!*

Makundi yalimiminika jangwani kumsikia Yohana. Waliokiri kuwa ni wenye dhambi wanaomhitaji Mwokozi walibatizwa kwenye Mto wa Yordani. Kwa njia hiyo walionyesha imani yao kwa Masihi, atakayeondoa deni lao kubwa la dhambi na kuwavika haki yake.

Siku baada ya siku na wiki baada ya wiki, Yohana aliwaambia watu kuhusu Mwokozi kutoka mbinguni aliyesubiriwa muda mrefu, "wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu" (Mathayo 3:11).

Na siku moja, Mwokozi alikuja — akitokea mlimani, akipita katikati ya umatii hadi mahali alipokuwa akibatiza Yohana.


Yohana alielekeza kwa Yesu na kusema,

> "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" (Yohana 1:29)

Kwa nini Yohana alimwita Yesu Mwana-kondoo wa Mungu?

Kama unajua ni kwa nini, basi unaujua wito wa Mfalme.







## Tukio la 45
# Mwana Mkamilifu

Yesu alitaka Yohana ambatize. Yohana alikataa kwa sababu Masihi-Mfalme hakuwa na haja ya kutubu.

> Yesu akajibu akamwambia, "Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote." (Mathayo 3:15)

Hivyo Yohana alimbatiza Yesu. Kwa kubatizwa, Yesu alionyesha alikuwa pamoja na familia ya watu aliokuja kuwaokoa.

> Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye!" (Mathayo 3:16-17)

Kama kwenye siku ya kwanza ya uumbaji, Umoja wa Mungu wenye maeneo matatu unafunuliwa tena. Hata Mungu, Roho wake, na Neno wake walivyofanya kazi kama mmoja kuuumba ulimwengu, na sasa walifanya kazi kama mmoja kuuokoa.[17]

Tunamwona *Roho wa Mungu* (ambaye mwanzoni alitulia juu ya uso wa maji) akimshukia Yesu. Tunamtazama *Mwana wa Mungu* (Neno aliyeuumba ulimwengu) akipanda kutoka mtoni. Tunamsikia *Baba* akizungumza kutoka mbinguni.

Miaka 30 nyuma yake Yesu aliishi bila kueleweka vizuri, bila kuonekana na wengi, lakini Baba yake wa mbinguni alifuatilia kila wazo, neno, na tendo lake. na uamuzi wa Baba yake juu ya maisha yake ulikuwaje?

> "Huyu ni Mwanangu … ninayependezwa naye!"

Kwenye historia yote ya wanadamu, Yesu ndiye pekee aliyefanya kila jambo analotaka Mungu. Kila jambo. Wakati wote. Kikamilifu.

Yesu alifanya alichoshindwa Adamu: kuuakisi mfano wa Mungu. Lakini Yesu alifanya zaidi ya kuakisi, alikuwa huo mfano.


> Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake … (Waebrania 1:1-3)

Si ajabu baadaye Yesu aliposema,

> "Mimi na Baba tu umoja." (Yohana 10:30)

Yesu ndiye Mwana mkamilifu.







## Tukio la 46
# Mwanadamu Wa Pili

Shetani hakufurahia Mwana huyu mkamilifu kuishi kwenye ufalme wake! Lakini Shetani alikuwa na mkakati. Kama alivyomjaribu mwanadamu wa kwanza akatenda dhambi, na sasa anataka amjaribu Yesu naye atende dhambi.

Shetani alitaka amlete Yesu chini ya utawala wake kama alivyofanya kwa Adamu. Mwana wa Mungu akishawishika kutenda dhambi, hatafaa kwa kuwaokoa watu wake watoke kwenye dhambi zao.

> Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate." (Mathayo 4:1-3)

Yesu alikuwa na njaa, lakini hakumtii Shetani. Hakutenda nje ya mapenzi ya Baba yake. Hakutumia mamlaka yake makuu kuridhisha matamanio yake ya mwili. Kumkabili Shetani, Yesu alinukuu kutoka kwenye Torati ya Musa:

> "Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." (Mathayo 4:4; Kumbukumbu 8:3)

Kwa kiburi chake cha kijinga, Shetani alimjaribu tena huyo Mtakatifu.

> Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha miliki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia." (Mathayo 4:8-9)

Adamu alipotenda dhambi, mwanadamu aliikosa haki ya kuitawala dunia. Shetani aliiiba miliki ya ulimwengu, akijifanya kuwa mfalme wake. Sasa Mfalme wa utukufu alikuwa duniani kuirudisha miliki hiyo, lakini hangeweza kwa kumwangukia ambaye amekuja kumwangamiza.

> Ndipo Yesu alipomwambia, "Nenda zako, Shetani; Kwa maana imeandikwa: 'msujudia Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake.'" (Mathayo 4:10)

Hatimaye, Shetani alimwacha Yesu. Shetani hakuwahi kumjaribu ye yote aliye kama Yesu, ambaye hakuwa na nia wala uwezo wa kutenda dhambi. Yesu hakuwa kama Adamu na uzao wake.


> Mtu wa kwanza atoka katika nchi, ni wa udongo. Mtu wa pili atoka mbinguni. (1 Wakorintho 15:47)

Adamu alikuwa mtu wa kwanza mkamilifu. Yesu alikuwa mtu wa pili mkamilifu.

Shetani alipomjaribu Adamu ili atende dhambi, Adamu alishindwa na Shetani akashinda. Shetani alipojaribu kumfanya Yesu atende dhambi, Shetani alishindwa, Yesu akashinda.

Mwanadamu wa kwanza alitupeleka kwenye ufalme wa Shetani wa dhambi na mauti. Mwanadamu wa pili alikuja kutuondoa huko.







## Tukio la 47

# Mfalme-Masihi

Baada ya jitihada za bure za Shetani za kumfanya Yesu atende dhambi, Yesu alirudi Nazareti, alikokulia na kufanya kazi ya useremala.

> Siku ya Sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake. (Luka 4:16)

Sinagogi ilikuwa nyumba ya kuabudia yalikosomwa na kufafanuliwa Maandiko kila Jumamosi. Jumamosi ile Yesu alikuwa na tangazo la kutoa.

> Alisimama ili asome.
>
> Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo akatafuta mahali palipoandikwa:
>
> "Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena …" (Luka 4:16-18)

Alichosoma Yesu kwenye Mandiko ni unabii wa kale kuhusu Mfalme-Masihi atakayeuonyesha ulimwengu Mungu alivyo na kuwaokoa wenye dhambi kutoka kwenye utawala wa Shetani, dhambi, kifo, na jehanamu.

> [Yesu] akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi;
>
> Na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, "Leo mandiko haya yametimia masikioni mwenu!" (Luka 4:20-21)


Majirani wa Yesu waliliitikiaje dai lake kuwa yeye ndiye Masihi aliyetoka mbinguni kuja kutimiza waliyoandika manabii kwenye Maandiko?

> Wakajaa ghadhabu wote waliokuwa katika sinagogi walipoyasikia hayo. wakaondoka wakamtoa nje ya mji, wakampeleka mpaka ukingo wa kilima ambacho mji wao umejengwa juu yake, wapate kumtupa chini.
>
> Lakini yeye alipita katikati yao akaenda zake. (Luka 4:28-30)

Yesu alikuwa mtawala. Tofauti na uzao wa Adamu ulioathiriwa na dhambi na kifo, Mfalme-Masihi aliyetiwa mafuta[18] na Mungu alikuwa na mamlaka kamili. Hakuna aliyeweza kumgusa bila ya ridhaa yake.

Lakini yeye aliwagusa.







## Tukio la 48
# Mamlaka Juu Ya Mapepo Na Magonjwa

Kwenye Maandiko ya manabii, moja la majina ya Masihi ni *Mkono wa BWANA* (Isaya 53:1). Miujiza ya Yesu ilimwonyesha Yeye kuwa ni Mkono wa Bwana duniani. Kwa mguso wa mkono wake au neno kutoka kinywani mwake, wagonjwa na waliokuwa katika hali ya kufa waliponywa hapo hapo.

> Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, mabubu, vilema, na wengine wengi wakawaweka miguuni pake; akawaponya.
> (Mathayo 15:30)

Maneno ya manabii yalikuwa yakitimia.

> Vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema. (Mathayo 11:5 [Isaya 35:4-6; 61:1])

Hakuna ugonjwa alioshindwa Yesu kuuponya.

> Akaja kwake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti, na kumwambia, "Ukitaka, waweza kunitakasa."
>
> Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, "Nataka, takasika."
>
> Na mara ukoma wake ukamtoka, akatakasika. (Marko 1:40-42)
>
> Na jua lilipokuwa likichwa, wote waliokuwa na wagonjwa wenye maradhi mbali mbali waliwaleta kwake, akaweka mikono yake juu ya kila mmoja, akawaponya. Pepo nao waliwatoka watu wengi, wakipiga kelele na kusema, "Wewe u Mwana wa Mungu!"
>
> Akawakemea, asiwaache kunena, kwa sababu walimjua kuwa ndiye Kristo.
> (Luka 4:40-41)


Yesu hakutaka mapepo yamshuhudie. Malaika hawa wovu walishuhudia mamlaka na uwezo wake alipozitamkia mbingu na nchi ziwe mahali pake. Waliogopa wakiikumbuka siku alipowatupa kutoka mbinguni. Na sasa alikuwa anaishi duniani kama mwanadamu! Utawala wa bwana wao ulikuwa ukivunjika. Mfalme wa utukufu alikuwa amevamia miliki yao.

Po pote alikokwenda Yesu, mamlaka ya Shetani yalikuwa yakidhoofishwa. Kila alikoenda Yesu, laana ya dhambi ilikuwa ikirudishwa nyuma.

Sambamba na miujiza, Yesu alikuwa na ujumbe:

> "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili!" (Marko 1:15)







## Tukio la 49
# Mamlaka Juu Ya Upepo Na Mawimbi

Yesu aliteua wanaume kumi na wawili wasafiri naye na wajifunze kwake. Pia wanawake wengi walimfuata. Walimhudumia Yesu na wanafunzi wake wakiwapa chakula na fedha.

Kwa kila aliyemfuata, mwito wa Yesu ulikuwa rahisi:

> "Nifuate." (Luka 5:27)

Lakini mwito wake pia ulikuwa na gharama:

> "Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili." (Mathayo 10:37)

Kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wake walikuwa wavuvi, mara nyingi Yesu aliitumia siku akiwa kando ya bahari ya Galilaya. Watu walimjia kutoka karibu na kutoka mbali.

> Akaanza kufundisha tena kando ya bahari. Wakamkusanyikia mkutano mkubwa mno, hata yeye akapanda chomboni, akakaa baharini. (Marko 4:1)

Akiisha kufundisha siku nzima, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Twendeni ng'ambo nyingine." Tayari alikuwa chomboni, hivyo wakaanza safari, wakiwaacha makutano.

> Ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji. Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu ya mto; wakamwamsha, wakamwambia, "Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia?"
>
> Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, "Nyamaza, utulie!"
>
> Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu.
>
> Akawaambia, "Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?"
>
> Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, "Ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii?" (Marko 4:37-41)


*Ni nani huyu?* Miaka elfu moja nyuma yake, nabii Daudi tayari alikuwa amelijibu swali lile:

> Wayumba-yumba, wapepesuka kama mlevi, Akili zao zote zawapotea. Wakamlilia BWANA katika dhiki zao, akawaponya na shida zao. Huituliza dhoruba, ikawa shwari, Mawimbi yake yakanyamaza. (Zaburi 107:27-29)

Ni nani awezaye kutuliza upepo na mawimbi kwa kuyatamkia tu?

Ni Sauti ile ile iliyoyaumba.







## TUKIO LA 50
# MAMLAKA JUU YA DHAMBI

Siku moja, wanaume wanne waliobeba machela ya mtu aliyepooza walikwenda kwenye nyumba alipokuwa Yesu.

Wanaume hao walijaribu kuingia ndani wasiweze kwa sababu ya wingi wa watu. Hivyo walipanda darini wakaitoboa wakaliteremsha godoro alipolazwa mwenye kupooza hadi mahali alipokuwa Yesu.

> Naye Yesu alipoiona imani yao, akamwambia yule aliyepooza, "Mwanangu, umesamehewa dhambi zako." (Marko 2:5)

Yesu alilijua kuwa hitaji kuu la aliyepooza si kutembea tena bali kusamehewa dhambi zake.

> Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi wakifikiri mioyoni mwao, Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?
>
> Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, "Mbona mnafikiri hivyo mioyoni mwenu? Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, 'Umesamehewa dhambi zako', au kusema, 'Ondoka, ujitwike godoro lako, uende?' Na nitakuhiridishia ya kwamba Mwana wa Mtu ana uwezo wa kusamehe dhambi," (hapo amwambia yule mwenye kupooza), Nakuambia, "Ondoka ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako."
>
> Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote.
>
> Hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, "Namna hii hatujapata kuiona kamwe!" (Marko 2:6-12)

Waalimu wa sheria walikuwa wamepofushwa na dini na majivuno yao. Mawazo yao yalikuwa hivi: *Yesu, wewe ni mjadhambi! Unamtukana Mungu kwa sababu unadai kusamehe dhambi, lakini ni Mungu pekee anayeweza kufanya hilo!*


Walikuwa sahihi kufikiri kuwa ni Mungu pekee anayeweza kusamehe dhambi, lakini walikuwa wamekosea kwenye maamuzi yao kuhusu Yesu ni nani.

Unafikiri Yesu ni nani? Unaikumbuka maana ya jina lake? Lina maana ya *BWANA huokoa*.

Kwenye mji mmoja wa Kipalestina alikofundisha Yesu, watu walifikia uamuzi huu:

> "Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu; maana sisi tumesikia wenyewe, tena twajua ya kuwa hakika huyu ndiye Mwokozi wa ulimwengu." (Yohana 4:42)







Tukio la 51

# Mamlaka Juu Ya Kifo

Yesu alikuwa na mamlaka juu ya kila sehemu ya uumbaji. Hata hivyo hakuzunguka akisema, "Niabuduni! Mimi ni Mungu! Mimi ni Mungu!" Alifanya tu mambo ambayo ni Mungu pekee awezaye kuyafanya na akawaacha watu waamue wenyewe.

Kwa kuangalia simulizi hizi mbili unafikiri Yesu ni nani?

> [Yesu] alikwenda mpaka mji mmoja uitwao Naini, na wanafunzi wake walifuatana naye pamoja na mkutano mkubwa. Na alipolikaribia lango la mji, hapo palikuwa na maiti anachukuliwa nje, ni mwana pekee wa mamaye ambaye ni mjane, na watu wa mjini wengi walikuwa pamoja naye.
>
> Bwana alipomwona alimwonea huruma, akamwambia, "Usilie."
>
> Akakaribia, akaligusa jeneza; wale waliokuwa wakilichukua wakasimama. Akasema, "Kijana, nakuambia, inuka."
>
> Yule maiti akainuka, akaketi akaanza kusema. Akampa mama yake. Hofu ikawashika wote, wakamtukuza Mungu. (Luka 7:11-16)

Siku nyingine, Yesu aliwatembelea dada wawili wenye huzuni, Martha na Mariamu. Kaka yao Lazaro alikufa zikapita siku nne.


> Basi Martha akamwambia Yesu, "Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa …"
>
> Yesu akamwambia, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini, hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?"
>
> Akamwambia, "Naam, Bwana, mimi nimesadiki ya kwamba wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, Yule ajaye ulimwenguni."
>
> Yesu … akafika kwenye kaburi. Nalo lilikuwa ni pango, na jiwe limewekwa juu yake. Yesu akasema, "Liondoeni jiwe."
>
> Martha, dada yake yule aliyefariki, akamwambia, "Bwana, ananuka sasa; maana amekuwa maiti siku nne."
>
> Yesu akamwambia, "Mimi sikukuambia ya kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?" Basi wakaliondoa lile jiwe. Yesu akalia kwa sauti kuu, "Lazaro, njoo huku nje." Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi … Yesu akawaambia, "Mfungueni, mkamwache aende zake."
> (Yohana 11:21, 25-27, 38-41, 43-44)

Bwana Yesu ndiye mwanadamu pekee katika historia aliyeweza kusema,

> "MIMI NDIMI huo ufufuo na uzima."

Kazi zake zilithibitisha kuwa maneno yake yalikuwa ya kweli.







## TUKIO LA 52
# MPAJI

Makundi makubwa ya watu hawakumwacha Yesu, wakati mwingine kwa siku kadhaa mfululizo. Mara nyingi walimwona kwenye maeneo yasiyokaliwa na watu akiwa na wanafunzi wake. Wakati mwingine umati ulipata njaa.

Hili lilitokea alasiri moja wakiwa wamekusanyika watu zaidi ya 5000 kando ya mlima mashariki mwa bahari ya Galilaya. Yesu akamwuliza Filipo, mmoja wa wanafunzi wake,

> “Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula?” Na hili alilinena ili kumjaribu; kwa maana alijua mwenyewe atakalotenda.
>
> Filipo akamjibu, “Mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi.”
>
> Andrea, nduguye Simoni Petro, akamwambia, “Yupo hapa mtoto, yuna mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa?”
>
> Yesu akasema, “Waketisheni watu.” Na mahali pale palikuwa na majani tele. Basi watu waume wakaketi, wapata elfu tano jumla yao.
>
> Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka.
>
> Nao waliposhiba, aliwaambia wanafunzi wake, “Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee cho chote.”
>
> Basi wakavikusanya, wakajaza vikapu kumi na viwili, vipande vya mikate mitano ya shayiri vilivyowabakia wale waliokula. (Yohana 6:5-13)


Siku iliyofuata baadhi ya makundi walikuja wakimtafuta Yesu. Walitaka wamfanye kuwa mfalme wao, lakini tu ili awaokoe kutoka kwa watesi wao wa Kirumi, na awape chakula zaidi. Yesu aliwaambia,

> “Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu[19] atawapa, kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu.
>
> “Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe.” (Yohana 6:27,35)

Chakula kitakufanya uishi kwa muda, lakini ni Bwana Yesu pekee anayeweza kukupa uzima wa kweli, sasa na milele. Ni Yesu tu anayeweza kusema,

> “MIMI NDIMI mkate wa uzima.”







## Tukio la 53
# Mwalimu

Yesu hakuwa kama wale walimu wa kidini waliosema maneno kama, “Fanya hili! Usifanye lile! Fuata sheria hizi! Hii ndiyo njia!” Yesu aliweza tu kusema,

> “MIMI NDIMI njia na kweli na uzima.” (Yohana 14:6)

Yesu pia alikuwa tofauti na manabii waliotoa sadaka kwa ajili ya dhambi zao na wakaandika kuhusu ujio wa Masihi. Yesu alisema,


> “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kuitangua, bali kuitimiliza.” (Mathayo 5:17)

Mara nyingi Yesu aliwafundisha wanafunzi wake wanavyopaswa kuishi raia wa ufalme ili waonyeshe tabia na utukufu wa Mfalme.

> “Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi.
>
> “Msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wanapenda kusali … waonekane na watu. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini. Basi ninyi salini hivi; ‘Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni, Utupe leo riziki yetu …’
>
> “Msisumbuke, basi, mkisema, ‘Tule nini?’ Au ‘Tunywe nini?’ Au ‘Tuvae nini?’ Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.
>
> “Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali.
>
> “Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba, mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba.
>
> “Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.” (Mathayo 5:43-44; 6:5-6, 9-11, 31-33; 7:15, 24-27)

Hakuna aliyewahi kusema kama yule Mwalimu aliyetoka mbinguni.





## Tukio la 54
# Fahari Yake

Walimu na makuhani wa Wayahudi hawakufurahi kuwaona makundi wakimsikiliza Yesu. Waliwataka watu wawasikilize wao, wasimsikilize yeye!

Siku moja makuhani wakuu waliwatuma watumishi wao wa hekalu wamkamate Yesu, lakini hawakumkamata. Waliporudi, makuhani waliwauliza, "Kwa nini hamkumleta?" Wale watumishi walijibu,

> "Hajanena kamwe mtu ye yote kama huyu anavyonena." (Yohana 7:46)

Hata manabii hawajanena kama Yesu. Manabii walikuwa kama mishumaa inayotoa miali ya mwangaza kwenye ulimwengu wa giza, lakini Masihi alikuwa "jua la haki" (Malaki 4:2). Ni nani anayehitaji mishumaa jua likiwa limechomoza?

Yesu alisema,

> "MIMI NDIMI nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." (Yohana 8:12)

Yesu ndiye Neno ambaye hapo mwanzo alisema, "Iwe nuru." Yeye ndiye Chanzo kikuu cha nuru inayoonekana, na ile ya kiroho.

Saa ilipokaribia ya Masihi kutimiza wito wake, Aliwatwaa watatu kati ya wanafunzi wake, Petro, Yakobo, na Yohana, akawaleta juu ya mlima mrefu.

> Akageuka sura yake mbele yao, uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru.
>
> Na tazama, wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye… Wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema,
>
> "Huyu ni Mwanangu, Mpendwa wangu; ninayependezwa naye; msikieni yeye!"
>
> Wale wanafunzi waliposikia, walianguka kifulifuli, wakaogopa sana. Yesu akaja, akawagusa, akasema, "Inukeni, wala msiogope."
>
> Wakainua macho yao, wasione mtu ila Yesu peke yake. (Mathayo 17:1-3, 5-8)

Wanafunzi hawakusahau kamwe walichokiona siku ile. Baadaye, Petro aliandika, "Tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake!" (2 Petro 1:16) na Yohana alisema, "Nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli" (Yohana 1:14).

Lakini wakati huo, utukufu wa Mwana ulibaki umefichwa kwenye mwili wake wa nyama.

Ulikuwa wakati wa Mfalme kutimiza wito wake.







## Tukio la 55
# Utume Wake

Kwa miaka mitatu, Bwana Yesu alikuwa akiizungukia Palestina “akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi” (Matendo 10:38). Watu wa kawaida walimpenda, lakini viongozi wa dini wa Yerusalemu walikuwa wakipanga kumwua — na Yesu alilijua hilo.

> Ikawa, siku za kupaa kwake zilipokuwa karibu kutimia, yeye aliukaza uso wake kwenda Yerusalemu. (Luka 9:51)

Ukijua kuwa genge la waovu kwenye mji ulio mbali wanapanga kukuteka, kukutesa, na kukuua, utakwenda huko?

Ndicho alichofanya Yesu.

> Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka. (Mathayo 16:21)

Hii haikuwa aina ya Mfalme waliyekuwa wakimtarajia wanafunzi. *Masihi aliyesulibiwa? Hakika Mungu hangeruhusu Mteule wake kupata mateso na aibu kama hiyo!* Hivyo Petro alimwambia Yesu,

> “Hasha, Bwana! Hayo hayatakupata!”

> [Yesu] akageuka, akamwambia Petro, nenda nyuma yangu, Shetani! U kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu. (Mathayo 16:22-23)

Wanafunzi walitaka Mfalme-Masihi atakaye waharibu walowezi wa Kirumi na kuweka utawala mpya Yerusalemu. Hata walipokuwa wakisafiri, wanafunzi walikuwa wakibishana kuhusu nani atakuwa mkubwa kwenye ufalme wa Mungu. Hivyo Yesu aliwaambia wanafunzi wake,

> “Mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; … Kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.” (Mathayo 20:26, 28)


Alipokuja duniani mara ya kwanza, Masihi hakuja kushinda falme za kisiasa na kutawala viti vya enzi vya duniani; Alikuja kumshinda Shetani na kutawala mioyo ya watu. Ndiyo sababu Yesu alifundisha,

> “Ufalme wa Mungu umo ndani yenu.” (Luka 17:21)

Lakini kabla ya Mfalme atokaye mbinguni kuweza kutawala mioyoni (na baadaye kuitawala dunia yote), ilibidi kwanza deni la ulimwengu la dhambi lilipwe, na kifo kishindwe.

Wito wake ulikuwa *huo*.





TUKIO LA 56

# MFALME ANAINGIA YERUSALEMU

Kila jambo lilikwenda lilivyopangwa. Bwana alipoikaribia Yerusalemu, Alituma wawili katika wale wanafunzi, akisema,

> "Nendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili, na mtakapoingia ndani mtaona mwana-punda, amefungwa, ambaye hajapandwa na mtu ye yote bado, mfungueni mkamlete hapa. Na kama mtu akiwauliza, Mbona mnamfungulia? Semeni hivi, Bwana anamhitaji.'"
>
> Na wale waliotumwa wakaenda wakaona kama alivyowaambia. Na walipokuwa wanamfungua mwana-punda, wenyewe waliwaambia, "Mbona mnamfungua mwana-punda?"
>
> Wakasema, "Bwana ana haja naye". Wakampeleka kwa Yesu, wakatandika nguo zao juu ya mwana-punda, wakampandisha Yesu.
>
> Na alipokuwa akienda walitandaza nguo zao njiani. Hata alipokuwa amekaribia matelemko ya mlima wa Mizeituni, kundi zima la wanafunzi wake walianza kufurahi na kumsifu Mungu kwa sauti kuu, kwa ajili ya matendo yote ya uwezo waliyoyaona, wakasema, "Ndiye mbarikiwa Mfalme ajaye kwa jina la Bwana; amani mbinguni, na utukufu huko juu!"
>
> Baadhi ya Mafarisayo[20] waliokuwa katika mkutano wakamwambia, "Mwalimu, uwakanye wanafunzi wako." Akajibu, akasema, "Nawaambia ninyi, wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele." (Luka 19:30-40)

Huyo ni Mfalme wa aina tofauti!

Huyo Mfalme-Masihi hakulifurikia jiji kwa matarumbeta na jeshi lenye nguvu. Hakuingia amepanda farasi wa kivita.


Aliingia amepanda punda wa hali ya chini — mwana-punda, punda mkaidia (kwa kawaida angeweza kupiga mateke na kuruka), mnyama mwenye alama ya msalaba mgongoni na mabegani mwake, na, muhimu zaidi, mnyama pekee aliyeweza kutimiza unabii alioandika nabii Zekaria miaka mia tano kabla:

> Piga kelele, Ee binti Yerusalemu; Tazama, mfalme wako anakuja kwako;
> Ni mwenye haki, naye ana wokovu; Ni mnyenyekevu, amepanda punda,
> Naamu, mwana-punda, mtoto wa punda. (Zekaria 9:9)

Kwa nini Mfalme-Masihi hakuingia Yerusalemu akipanda farasi mwenye nguvu wa kivita? Kwa sababu hakuja kuwaokoa watu kutoka kwa watesi wa Kirumi.

Alikuja kuwaokoa watu wake kutoka dhambini mwao.







## Tukio la 57
## Mfalme Anahojiwa

Siku chache baadaye, Yesu aliwafundisha watu hekaluni ambapo, akiwa kijana, aliwashangaza walimu kwa maswali yenye kina na majibu yenye hekima. Viongozi wa hekalu sasa wakawa na msimamo tofauti:

> "Hatumtaki huyu atutawale!" (Luka 19:14)

Hivyo walimvamia Yesu kwa maswali nyeti, wakitumaini watawageuza watu wa kawaida wampinge.

> Wakamvizia-vizia, wakatuma wapelelezi waliojifanya kuwa watu wa haki, ili wamnase katika maneno yake, wapate kumtia katika enzi na mamlaka ya liwali.
>
> Wakamwuliza, wakisema, "Mwalimu, twajua ya kwamba wasema na kufundisha yaliyo ya haki, wala hujali cheo cha mtu, bali unafundisha njia ya Mungu kwa kweli. Je! Ni halali tumpe Kaisari kodi, au sivyo?" (Luka 20:20-22)

Yesu angejibuje? Akisema, "Ndiyo, mpeni kodi Kaisari," umma wa Wayahudi ungemshitaki kwa kutotii kusudi lao. Kwa upande mwingine, Yesu akijibu, "La, msilipe kodi," mkuu wa Kirumi angesikia na kumshitaki kwa uasi.

> Lakini yeye alitambua hila yao, akawaambia, "Nionyesheni dinari. Ina sura na anwani ya nani?"
>
> Wakamjibu, "Ya Kaisari."
>
> Akawaambia, "Basi, vya Kaisari mpeni Kaisari, na vya Mungu mpeni Mungu."
>
> Wala hawakuweza kumshitaki kwa maneno yake mbele ya watu; wakastaajabia majibu yake, wakanyamaa. (Luka 20:23-26)


Tena na tena, makundi tofauti ya walimu wa dini walijaribu kumtega Yesu, lakini kila mara aliwajibu kwa hekima kamilifu.

> Hakuthubutu mtu ye yote tangu siku ile kumwuliza neno tena. (Mathayo 22:46)

Kwa aibu, hao waliondoka wakaenda kwa wakuu wa makuhani wakapange nao watakavyomkamata na kumwua Yesu. Upofu mkubwa mno! Makuhani hawa wenye wajibu wa kutoa sadaka madhabahuni, hawakutambua kuwa waliyetaka kumwua ndiye aliyetolewa mfano kwenye sadaka hizo.

Mpango wa Mungu wa siri ulikuwa karibu kutimia.







# Tukio la 58
## Mfalme Anakamatwa

Ilikuwa siku kabla ya sikukuu ya dhabihu ya kila mwaka iliyoitwa Pasaka.[16] Siku ile wachinjwe maelfu ya wana-kondoo.

Ingawa Yesu alijua kuwa naye atauawa siku hiyo, Aliitumia jioni ile kushiriki chakula cha mwisho na wanafunzi wake. Wakati wa chakula, Aliuchukua mkate, akaubariki, akaumega, akawapa wale. Alipitisha na kikombe. Aliwaambia kuwa wakiula mkate, waufikirie mwili wake, na kwa hiyo juisi nyekundu waifikirie damu yake itakayomwagika kuleta kwenye agano jipya msamaha wa dhambi.

Usiku wa manane, aliwaongoza hadi kwenye bustani iliyoitwa Gethsemane. Huko, akiyajua mateso yaliyomsubiri, Alimwomba Baba yake.

Kisha, kama vile walidokezwa, viongozi wa kidini walifika na kundi la watu wenye silaha. Yesu akawaambia,


> "Je, mmetoka kama kumkamata mnyang'anyi, wenye panga na marungu, ili kunishika? Kila siku naliketi hekaluni nikifundisha, msinikamate. Lakini haya yote yamekuwa, ili maandiko ya manabii yatimizwe."
>
> Ndipo wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia. (Mathayo 26:55-56)

Yesu aliruhusu wakamfuga na kumpeleka kwenye nyumba ya kuhani mkuu ambapo wakuu wa Wayahudi walikuwa wamekusanyika. Huko wanaume wengi walieleza uongo kuhusu Yesu.

> Kisha Kuhani Mkuu akasimama katikati, akamwuliza Yesu, akisema, "Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini?" Lakini akanyamaza, wala hakujibu neno. Kuhani Mkuu akamwuliza tena, akamwambia, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu?"
>
> Yesu akasema, "Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni."
>
> Kuhani Mkuu akararua nguo zake, akisema, "Tuna haja gani tena ya mashahidi? Mmesikia kufuru yake; mwaonaje ninyi?"
>
> Wote wakamhukumu kuwa imempasa kuuawa.
>
> Wengine wakaanza kumtemea mate, wakamfunika uso, na kumpiga makonde, na kumwambia, "tabiri." Hata watumishi nao wakampiga makofi. (Marko 14:56,60-65)

Mahakama ya Wayahudi ilipitisha hukumu ya kifo, lakini haikuwa na mamlaka ya kuitekeleza. Ni mahakama ya Kirumi tu iliyoweza kufanya hivyo.







## Tukio la 59
# Mfalme Anahukumiwa

Ilikuwa mapema asubuhi viongozi wa dini na genge kubwa walipomwondoa Yesu kwenye nyumba ya kuhani mkuu wakiipitia mitaa ya Yerusalemu hadi kwenye nyumba ya kiongozi wa Kirumi aliyeitwa Pontio Pilato.

Viongozi wa dini walitaka Pilato amuue Yesu.

> Wakaanza kumshitaki, wakisema, "Tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme."
>
> [Baada ya kumhoji Yesu] Pilato akawaambia wakuu wa makuhani na makutano, "Sioni neno lililo ovu katika mtu huyu!" (Luka 23:2,4)

Wakajibu, wakamwambia, "Kama huyu asingekuwa mtenda mabaya, tusingemleta kwako," …


> Basi Pilato akaingia tena ndani ya Praitorio, akamwita Yesu, akamwambia, "Je! Wewe ni Mfalme wa Wayahudi? … Umefanya nini?"
>
> Yesu akajibu, "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa." Basi Pilato akamwambia, "Wewe u mfalme basi?"
>
> Yesu akajibu, "Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu."
>
> Pilato akamwambia, "Kweli ni nini?"
>
> Naye akiisha kusema neno hilo akawatokea Wayahudi tena, akawaambia, "Mimi sioni hatia yo yote kwake." (Yohana 18:30,33,35-38)

Lakini wakapiga kelele, wakisema,

> "Msulibishe! Msulibishe!"
>
> Akawaambia mara ya tatu, "Kwa sababu gani? Huyu ametenda uovu gani? Sikuona kwake hata neno lipasalo kufa. Basi nikiisha kumrudi nitamfungua."
>
> Lakini wakatoa sauti zao kwa nguvu sana, wakitaka asulibiwe. Sauti zao zikashinda. (Luka 23:21-23)

Pilato alijua Yesu hakuwa na hatia, lakini kwa sababu aliwaogopa viongozi wa dini na genge lao, alimhukumu Yesu auawe.







## Tukio la 60
## Mfalme Anavikwa Taji

Pilato alimhukumu Yesu adhabu kali ya sheria ya Kirumi: kupigwa kikatili ndipo asulibiwe. Wahanga waliohukumiwa walipigwa mijeledi iliyowekewa vipande vya chuma vyenye ncha kali.

Miaka mia saba ya nyuma, Bwana alimwambia nabii Isaya aandike:

> "Naliwatolea wapigao mgongo wangu, na wang'oao ndevu mashavu yangu; sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate." (Isaya 50:6)

Injili inatueleza kilichotokea baada ya Bwana kupigwa.

> Ndipo askari wa liwali wakamchua Yesu ndani ya Praitorio, wakamkusanyikia kikosi kizima.
>
> Wakamvua nguo, wakamvika vazi jekundu.
>
> Wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake, na mwanzi katika mkono wake wa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki, wakisema, "Salamu, Mfalme wa Wayahudi!" Kisha wakamtemea mate, wakautwaa ule mwanzi, wakampiga-piga kichwani. (Mathayo 27:27-30)

Askari hao hawakuijua maana ya taji ya miiba waliyopigilia kwenye kichwa cha Yesu. Miiba ilikuwa sehemu ya laana iliyokuja juu ya nchi kwa sababu ya dhambi ya Adamu. Huyo Mfalme wa utukufu aliye mtakatifu alikuja kuchukua laana ya dhambi kwa ajili yetu.

> Walipokwisha kumdhihaki, wakalivua lile vazi, wakamvika mavazi yake, wakamchukua kumsulibisha. (Mathayo 27:31)


Wenye hatia wawili waliohukumiwa nao walipelekwa pamoja na Yesu. Kila mmoja alibebeshwa msalaba wake hadi mahali pa kusulibiwa.

Wakiwa njiani kwenye hilo gwaride katili, hao askari wa Kirumi walimlazimisha mwanaume kutoka Afrika ya kaskazini ambebee Yesu msalaba. Wakaendelea wakipitia kwenye mitaa ya Yerusalemu iliyojaa watu, nje ya kuta za jiji, na wakaupanda mlima ulioitwa Golgotha, sehemu ya kaskazini ya Mlima Moria ambapo, kama miaka 1900 nyuma yake, nabii Ibrahimu alisema,

> "Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu." (Mwanzo 22:8).

Ulikuwa wakati wa huyo Mwana-kondoo kufa.







## Tukio la 61
# Mfalme Anasulubiwa

Kusulibisha ni njia inayotisha zaidi ya uuaji kuwahi kuundwa na taifa. Wakiongezea kuaibisha hadharani kwenye mateso yenye maumivu makali, askari hao waliwavua nguo wahanga wakabaki uchi kabla ya kuwapigilia misumari mikono na miguu kwenye msalaba au mti.

> Na walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulibisha yeye, na wale wahalifu, mmoja upande wa kuume, na mmoja upande wa kushoto. Yesu akasema, “Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.”
>
> Wakagawa mavazi yake, wakipiga kura. Watu wakasimama wakitazama. Wale wakuu nao walikuwa wakimfanyia mzaha, wakisema, “aliokoa wengine; na ajiokoe mwenyewe, kama ndiye Kristo wa Mungu, mteule wake.”
>
> (Lk 23:33-35)

Yesu angejiokoa mwenyewe hangetuokoa sisi. Umati haukufikiria kuwa walikuwa wanatimiza alichosema Bwana kwa nabii Daudi:

> “Wamenizua mikono na miguu … Wao wananitazama na kunikodolea macho. Wanagawanya nguo zangu, Na vazi langu wanalipigia kura … Wote wanionao hunicheka sana, Hunifyonya, wakitikisa vichwa vyao; ‘… Umtegemee BWANA; Na amponye; … maana apendezwa naye!’”
>
> (Zaburi 22:16-18, 7-8)

Mpango wa Mungu wa kuokoa ulikuwa ukitimizwa kwenye kila kipengele.

Kwenye mlima ule ule[11] ambapo nabii Ibrahimu alisema, “Mungu atajipatia mwana-kondoo,” na “katika mlima wa BWANA itapatikana” (Mwanzo 22:8, 14), Mungu alimtoa Mwana-kondoo wake mwenyewe — Yesu.

Unakumbuka kondoo dume asiye na hatia alivyotolewa sadaka kwenye kuni madhabahuni kumkomboa mwana wa Ibrahimu aliyehukumiwa? Sasa Mwana wa Mungu asiye na dhambi alikuwa akitolewa sadaka kwenye msalaba wa mbao aukomboe uzao wa Ibrahimu uliohukumiwa. Mungu alimwachilia mwana wa Ibrahimu, lakini haku “mwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote” (Warumi 8:32).

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
>
> (Yoh 3:16)

> Mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo. (1 Petro 1:18-19)

Ndivyo ulivyo na thamani kwa Mungu.







# Tukio la 62
## Mfalme-Mwokozi

Ili autimize mpango wa Mungu wa wokovu, Bwana Yesu aliitambua aibu inayoletwa na dhambi. Alilaaniwa badala yetu. Aliichukua adhabu tunayostahili.

Siku Adamu alipoivunja sheria ya Mungu, Mungu alifanya ijulikane kuwa siku moja Masihi atamponda kichwa nyoka. Mungu alimwambia Shetani,

> "[uzao] huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino." (Mwanzo 3:15)

Unabii huu wa kale wa kimafumbo kuhusu Shetani kuponda kisigino cha Mwokozi kulitabiri aibu na maumivu atakayopata Mwana-kondoo wa Mungu msalabani maana "alijeruhiwa kwa makosa yetu" (Isaya 53:5).

Waliomsulibisha Yesu hawakuujua mpango wa siri wa Mungu.

> Wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja, maana kama wangalijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu.
>
> Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. (1 Wakorintho 2:8; 1:18)

Msalaba wa Yesu uliwekwa katikati ya wahalifu wawili.

> Na mmoja wa wale wahalifu waliotundikwa, alimtukana, akisema, "Je! Wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi!"
>
> Lakini Yule wa pili akamjibu akamkemea, akisema, "Wewe humwogopi hata Mungu, nawe uko katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyo hakutenda lo lote lisilofaa." Kisha akasema, "Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako."
>
> Yesu akamwambia, "Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi." (Luka 23:39-43)

Mhalifu wa kwanza alitaka tu kuokolewa na mateso ya mwili wake. Hakufikiria kuwa alihitaji Mwokozi wa kufa badala yake.


Mhalifu wa pili naye alimtukana Yesu, lakini alipokabili kifo, alikuwa na badiliko moyoni. Alimtaka Bwana amwokoe kutoka kwenye ufalme wa Shetani. Alitaka awe raia wa ufalme wa Mungu, Yesu alimthibitishia kuwa naye alipomwambia:

> "Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi." (Luka 23:43)

Baadaye jioni ile, wahalifu wote wawili walikufa. Mmoja alikwenda kuzimuni. Mwingine alikwenda peponi. Ni nini kilichotofautisha?

Mmoja hakumtumaini Mfalme-Mwokozi. Mwingine alimtumaini.







## Tukio la 63
## Sadaka Ya Mwisho

Ni adhuhuri. Yesu amekuwa msalabani kwa masaa matatu. Mawingu mazito yanaingia. Mchana unakuwa kama usiku. Waangaliaji wanatiwa hofu na kusambaa. Ukimya wenye hofu unaufunika mlima. Masaa matatu baadaye, Yesu analia,

> "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Mathayo 27:46)

Kwenye madhabahu ya msalaba, Mwana wa Mungu wa milele alikiona kitisho cha kutengwa na Mungu mbinguni. Kwenye hayo masaa ya giza, yaliyofichwa yasionekane na watu, Mungu alizibeba dhambi zetu zote na kumwekea Mwanawe aliye mtakatifu. Yesu anakuwa sadaka ya mwisho ya dhambi.

Dhambi zilizopita, za sasa, na zijazo zilipokuwa zikiwekwa kwa Yesu, Mungu huko mbinguni aliangalia kwingine kwa sababu "macho yake hayawezi kuangalia dhambi kwa kuwa ni matakatifu mno" (Habakuki 1:13). Kwa masaa matatu, Hasira ya Mungu juu ya dhambi iliwaka kwenye sadaka yake mwenyewe ya kuteketezwa. Kama mwana-kondoo aliyetolewa sadaka madhabahuni, Mwana-kondoo wa Mungu alitundikwa msalabani katikati ya mbingu na dunia, kati ya Mungu na mwanadamu. Asiye na ukomo aliikabili adhabu yetu kwa muda ili tusiikabili kwenye umilele.

Kisha ilikwisha.

Akijua kuwa ameizamisha adhabu iliyowastahili wenye dhambi na kuwa ameutimiza unabii wa Agano la Kale, Yesu alisema,

> "Imekwisha!"
>
> Akainama kichwa, akaisalimu roho yake. (Yohana 19:30)
>
> Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini, nchi ikatetemeka; miamba ikapasuka. (Mathayo 27:51)

Kwa karne nyingi, wana-kondoo walikuwa wakichinjwa na kuteketezwa kwenye madhabahu ya hekalu. Yesu alipokufa, Mungu alilipasua pazia lililokificha chumba maalumu ambapo damu ilinyunyizwa kila mwaka kufunika dhambi. Kwa kulipasua pazia, Mungu alikuwa akitangaza: *Imekwisha! Deni la dhambi limelipiwa kikamilifu! Mwana-kondoo wangu amemwaga damu yake takatifu kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu. Sitakubali tena damu ya wanyama kwa ajili ya dhambi. Mwanangu mpendwa ndiye sadaka ya mwisho. Kwa ajili ya wote wanaomwamini, mlango wa mbinguni uko wazi!* (Ona kitabu cha Waebrania kwenye Agano Jipya.)

Miaka mia saba kabla ya tukio hili, nabii Isaya aliandika,

> Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote. (Isaya 53:5-6)

Imekwisha.







## Tukio la 64
## Mfalme Amezikwa

Yesu wa Nazareti alikuwa amekufa. Ili kuthibitisha, askari alimchoma mkuki ubavuni. Damu na maji vilimwagika.

Matumaini ya wanafunzi nayo yalikuwa yamekufa. Wakidhani ilipasa Yesu awaharibu Warumi na kuanzisha ufalme wake duniani, wanafunzi walikuwa hawajaitambua ahadi yake ya kufufuka siku ya tatu.

Miili ya wahanga waliosulibiwa kwa kawaida ilikuwa ikitupwa jalalani nje ya jiji au kwenye kaburi la wengi. Haikuwa hivyo kwa mwili wa Yesu. Miaka mia saba kabla nabii Isaya aliandika,

> "Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; na pamoja na matajiri katika kufa kwake…" (Isaya 53:9)

Mungu alipanga Mwanawe azikwe kwenye kaburi la heshima.

> Hata ilipokuwa jioni akafika mtu tajiri wa Arimathaya, jina lake Yusufu, naye mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa Yesu; mtu huyu alimwendea Pilato akauomba mwili wa Yesu. Ndipo Pilato akaamuru apewe. (Mathayo 27:57-58)

Kabla ya kifo cha Yesu, Yusufu wa Arimathaya na rafiki yake Nikodemo walikuwa wanafunzi wa siri wa Yesu Masihi. Waliwaogopa viongozi wa dini. Lakini baada ya kumwona Yesu akiteseka msalabani, hawakuogopa tena. Hivyo waliuchukua mwili wa Yesu, wakauosha, na wakaufunga kwenye sanda ya kitani safi pamoja na kama kilo 35 za manemane, aina ile ile ya viungo vya thamani vya kuhifadhia maiti walivyompa mtoto Yesu wale Mamajusi. Kisha waliuweka mwili wake kwenye kaburi jipya la Yusufu mwenyewe. Baada ya kuvingirisha jiwe kubwa kufunika mlango wa kaburi, walikwenda nyumbani.

Yalikuwa mazishi ya kifalme, yanayostahili kwa mfalme.

Asubuhi iliyofuata viongozi wa dini walikwenda kwa Pilato.

> Wakasema, "Bwana, tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, baada ya siku tatu nitafufuka. Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi wake wakamwiba, na kuwaambia watu, Amefufuka katika wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita ule wa kwanza."
>
> Pilato akawaambia, "Mna askari; nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo." Wakaenda, wakalilinda kaburi salama, kwa kulitia lile jiwe muhuri, pamoja na wale askari walinzi. (Mathayo 27:63-66)

Wakati huo ndani ya kaburi nini kilikuwa kikitokea kwenye mwili wa Yesu?

Hakuna kilichotokea.







## Tukio la 65
# Kaburi Tupu

Tangu siku Adamu alipotenda dhambi, kifo kilitawala kama mfalme katili juu ya familia ya wanadamu. Kama Yesu aliwahi kutenda dhambi, kifo kingeufanya mwili wake nao uanze kuoza, kunuka, na kubadilika kuwa mavumbi taratibu. Lakini miaka 1000 ya nyuma, nabii Daudi aliandika,

> "Hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu." (Zaburi 16:10)

Kifo na kaburi havikuwa na mamlaka kwa Yule asiyewahi kutenda dhambi.

Siku ya tatu baada ya Yesu kuuawa na kuzikwa, Jumapili mapema asubuhi, wanawake kadhaa walikuja kwenye kaburi kutoa heshima zao. Ghafla, kukawako tetemeko kubwa malaika aliposhuka kutoka mbinguni, akaliondoa jiwe na kulikalia. Askari walizimia, lakini malaika aliwaambia wanawake,

> "Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu . . ."
>
> Wakaondoka upesi kutoka kaburini, kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari.
>
> Na tazama, Yesu akakutana nao, akasema, "Salamu!" Wakakaribia wakamshika miguu, wakamsujudia. (Mathayo 28:5-9)

Wakati huo huo wale askari walikuja mjini na kuwaambia wakuu wa dini kilichotokea. Hivyo viongozi waliwahonga fedha nyingi wakiwaambia,

> "Semeni, ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipokuwa tumelala." (Mathayo 28:13)

Lakini uongo wao haukuweza kuificha kweli. *Kaburi lilikuwa tupu!*


Kwa kifo chake, Yesu alilipa deni letu la dhambi. Kwa kuzikwa kwake, Yesu alitelemka kwenye shimo la kufa na kuoza. Kwa kufufuka kwake, Yesu alishinda mauti na sasa anasema,

> "Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu." (Ufunuo 1:17-18)

Kwa wote wanaoiamini habari hii njema, Kifo ni mlango tu wa kuuingilia uwepo wa Mfalme anayesema,

> "Kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai." (Yohana 14:19)







## Tukio la 66
# Ujumbe Wa Manabii

Siku ya kufufuka kwake, Yesu aliwatokea wengi kati ya wanafunzi wake: kwanza kwa wale wanawake, kisha kwa Petro, na kwa wale wasafiri wawili.

Siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili.

Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao. Macho yao yakafumbwa wasimtambue. Akawaambia, "Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea?"

Wakasimama wamekunja nyuso zao. Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, "Je! Wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo siku hizi?"

Akawauliza, "Mambo gani?" (Luka 24:13,15-19)

Wasafiri hao walieleza walivyotumaini Yesu wa Nazareti kuwa Masihi wa kuwashinda maadui zake. Lakini alisulibiwa! Na sasa kaburi lilikuwa tupu. *Hilo halikuwa na maana yo yote!*

Akawaambia, "Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?"

Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.

Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele. Wakamshawishi wakisema, "Kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha." Akaingia ndani kukaa nao.

Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua, kisha akatoweka mbele yao.

Wakaambiana, Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia Maandiko? (Luka 24:25-32)


Walirudi haraka hadi Yerusalemu wakawaambia wanafunzi: *Bwana yu hai! Ndiye Mwokozi aliyeahidiwa kwenye Maandiko! Ndiye Mwana-kondoo aliiyeonyeshwa mfano kwenye sadaka! Ndiye BWANA!*

Hatimaye ujumbe wa manabii ukawa na maana.

Maana thabiti.







Tukio la 67

# Mwili Wa Utukufu

Ilikuwa jumapili jioni. Wanafunzi walikuwa pamoja, milango imefungwa. Ghafla Yesu alitokea chumbani na kusema,

> "Amani iwe kwenu!"
>
> Naye akiisha kusema hayo, akawaonyesha mikono yake na ubavu wake. Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana. (Yohana 20:19-20)

Tomaso, mmoja wa wanafunzi 12 wa Yesu, hakuwapo jioni ile. Baadaye, wanafunzi walimwambia, "Tumemwona Bwana!"

> [Tomaso] akawaambia, "Mimi nisipoziona mikononi mwake kovu za misumari, na kutia mkono wangu katika ubavu wake, mimi sisadiki hata kidogo."
>
> Basi baada ya siku nane, wanafunzi wake walikuwamo ndani tena, na Tomaso pamoja nao. Akaja Yesu, na milango imefungwa, akasimama katikati, akasema, "Amani iwe kwenu."
>
> Kisha akamwambia Tomaso, "Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye."
>
> Tomaso akajibu, akamwambia, "Bwana wangu na Mungu wangu!"
>
> Yesu akamwambia, "Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki." (Yohana 20:24-29)


Siku arobaini zilizofuata, Bwana aliweza kutokea ghafla kwa wafuasi wake, akazungumza nao, kisha akatoweka. Mwili wa Yesu wa ufufuo haukuzuiwa na kuta wala kuhitaji muda na kasi kufika mahali atakako. Huku akiwa wa kwanza kuwa na mwili kama huo, hatakuwa wa mwisho.

> Na kama tulivyochukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutachukua sura yake yeye aliye wa mbinguni.
>
> Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. (1 Wakorintho 15:49,21-22)

Unaelewa kuwa wewe ni mwenye dhambi usiye na njia ya kutwaa haki ya kuishi kwenye ufalme wa Mungu? Unaamini kuwa Bwana Yesu Kristo alikufa badala *yako,* kwa ajili ya dhambi *zako,* na akawa hai tena, akikishinda kifo *kwa ajili yako?* Kama unaamini, Mungu anasema *haumo tena katika* Adamu. Mungu anakuona kama mwenye haki *ndani ya Kristo*. Siku moja na wewe utapokea mwili wa utukufu — kama wa Yesu.

Lakini bila makovu ya misumari.







# Tukio la 68
## Kuondoka

Utawala alionyang'anywa Adamu na Shetani, Yesu aliurudisha. Kwa mamlaka yake yaliyo kamili juu ya shetani na mapepo, upepo na mawimbi, magonjwa na njaa, dhambi na mauti — Yesu alionyesha kuwa na mamlaka kamili. Hata viongozi wa dini na askari walipomkamata, wakamtesa, na kumsulibisha, alikuwa amewaruhusu kufanya hivyo.

Ndiyo sababu, kabla ya kuinuliwa juu kwenye makao ya Baba yake, Bwana Yesu aliwaambia wanafunzi wake:

> "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,[21] mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." (Mathayo 28:18-20)

Yesu aliwaambia pia wafuasi wake,

> "Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." (Yohana 13:34-35)

Siku arobaini baada ya kufufuka kwake, Yesu aliwakusanya wanafunzi wake kwenye mlima wa mizeituni nje ya Yerusalemu. Wanafunzi walitaka kujua atarudi lini.

Yesu aliwajibu,

> "Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu;[22] nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."
>
> Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe.
>
> Wakasema, "Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."
>
> Kisha wakarudi kwenda Yerusalemu … (Matendo 1:7-12)

Huko mbinguni, ulikuwa wakati wa Mfalme kuvikwa "taji ya utukufu na heshima" (Zaburi 8:5; Waebrania 2:9).







## Tukio la 69
## Sherehe Ya Ushindi

Fikiria utukufu. Rangi. Muziki. Msisimko. Milioni mia za malaika wakihojiana: *Mfalme anakuja nyumbani! Lakini ataonekana tofauti. Aliyemuumba mwanadamu kwa mfano wa Mungu atakuwa na mfano wa mwanadamu daima!*

Kuna ukimya kwenye jiji la mbinguni.

Ghafla ukimya unavunjwa kwa pambio za kifahari za tarumbeta, zikifuatiwa na tangazo lenye mvumo:

Inukeni, enyi malango ya milele,

Mfalme wa utukufu apate kuingia.

Ni nani Mfalme wa utukufu?

BWANA mwenye nguvu, hodari, BWANA hodari wa vita!

Ni nani huyu Mfalme wa utukufu?

BWANA wa majeshi — Yeye ndiye Mfalme wa utukufu! (Zaburi 24:7-8,10)

Malango yanafunguka, na kwa shangwe ya mbinguni Shujaa anaingia, yule Mwana-kondoo, Mwana wa Adamu mwenye makovu ya vita — *Yesu!* Anavuka kwenye wingi wa wanaotukuza, hadi kwenye kiti cha enzi cha Baba yake. Akigeuka, Anautazama uzao wa Adamu uliokombolewa, na kuketi.

Utume umekamilishwa. Baadaye, raia wa mbinguni wanamwimbia Mfalme wao mpendwa huu wimbo mpya:

"Wastahili wewe … kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa." (Ufunuo 5:9)

Kisha malaika wanakizunguka kiti cha enzi, wakimsifu Mungu na kusema,

"Astahili Mwana-kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka." (Ufunuo 5:12)

Duniani leo, wingi wa uzao wa Adamu bado ni mateka kwenye ufalme wa shetani wa dhambi na mauti uliolaaniwa. Lakini uhuru unapatikana. Kwa kufa kwake, kuzikwa kwake, na kufufuka kwake, Bwana Yesu alivishinda vita vilivyoamuliwa. Kwa wote wanaomtumaini anasema,

"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia, maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo."

"Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi." (Yohana 14:1-3,6)







## Tukio la 70
## Mfalme Atakuja Tena

Siku moja kati ya hizi, ulimwengu ukiwa kwenye mahangaiko yake ya kipuuzi na dini za uongo, Mfalme wa utukufu atarudi duniani, lakini si juu ya punda kuonyesha hali ya chini, wala kuja kudhihakiwa na kuvikwa taji ya miiba.

Mfalme aliyefufuka alimpa Yohana onyesho la awali la hiyo siku ijayo:

> Kisha nikaona mbingu zimefunuka, na tazama, farasi mweupe, na yule aliyempanda, aitwaye Mwaminifu na wa kweli, na kwa haki ahukumu na kufanya vita. Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa chake vilemba vingi, naye ana jina lake lililoandikwa, asilolijua mtu ila yeye mwenyewe. Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake aitwa, Neno la Mungu. Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA. (Ufunuo 19:11-14,16)

Anaporudi Mfalme, sauti itaunguruma kutoka mbinguni:

> "Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki milele na milele!" (Ufunuo 11:15)

Maadui wa Mfalme watayeyuka mbele zake. Kisha atamfunga Shetani na kuuonyesha ulimwengu uliochakaa jinsi utawala wa haki ulivyo. Itakuwa saa nzuri kabisa duniani.

> Naye BWANA atakuwa Mfalme juu ya nchi yote; siku hiyo BWANA atakuwa mmoja, na jina lake moja. (Nabii Zekaria 14:9)

Siku ya hukumu, BWANA Yesu atakuwa ndiye Mhukumu.

> Kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa. (Nabii Danieli 7:9-10)

> Shetani na ufalme wake wa giza ata "tupwa katika ziwa la moto na kiberiti" (Ufunuo 20:10). Hatimaye, kichwa cha yule nyoka kitapondwa milele.

Kuhusu raia wa ufalme wa nuru, Mungu atawafanyia "mbingu mpya na nchi mpya … watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio" (Ufunuo 21:1,3-4).

Hatimaye, sala ya wote wanaompenda Mfalme itatambuliwa milele:

> "Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni." (Mathayo 6:10)

Hili ndilo ombi lako? Umemsujudia Mfalme wa utukufu?

Yeye ni Mfalme *wako?*





# Kufunga

Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.

— Yesu, Mfalme wa Utukufu (Yohana 5:24)

Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua. … Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.

— Injili (Yohana 1:10,12)

Ujumbe Kwenye Habari • 1

# Kwa Furaha Milele Baadaye?

Watu wa vizazi vyote wanapenda hadithi za kufikiria au za mapenzi na kuokolewa, simulizi zenye mwisho mzuri. Watu husimulia simulizi kama hizo kwa sababu yule Mungu mmoja wa kweli amejenga kwenye moyo wa mtu shauku ya kukombolewa kutoka kwenye uovu aishi kwa furaha milele hapo baadaye. Lakini habari za Mfalme wa Utukufu si hadithi ya kubuni.




Habari za kumfanya mtu aamini hazikuandikwa na manabii 40 kwa zaidi ya miaka 1500, lakini ni hivyo kwa kitabu cha Mungu. Habari za kubuni hazikuthibitishwa kwa mamia ya unabii na uvumbuzi wa wachimbuaji wa mambo ya kale, lakini ni hivyo kwa habari za Mungu.



Shujaa wa kuvutia si eneo la historia kugawanyika, lakini kwa Yesu ni hivyo. Ubunifu hauwezi kuiondoa dhambi na aibu yetu, kutuleta kwa Mungu, na kutupa moyo mpya uliojaa upendo wake, furaha, na amani yake, lakini Yesu anaweza.

Kwa kuyatimiza Maandiko ya manabii, Yesu Masihi amewezesha uzao wa Adamu kuishi milele na Mfalme-Muumbaji wao. Lakini si wote watakaoishi kwenye ufalme wake.



Kama Mungu alivyolielewesha agizo lake moja kwa Adamu kuhusu kuishi kwenye bustani ya duniani, kadhalika Mungu amelifanya agizo lake moja likawa wazi kwa uzao wa Adamu kuhusu kuishi kwenye jiji la mbinguni:

> Hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo. (Ufunuo 21:27)



Kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo ndio usajili wa mbinguni pamoja na jina la kila mtu ambaye, tangu wakati wa Adamu, ameiamini njia ya Mungu ya wokovu. Mfalme wa utukufu hatakulazimisha wewe au familia yako kumwamini yeye na alichokifanya kukuokoa kutoka kwa Shetani, dhambi, kifo na jahanamu.

Hakutakuwa na raia wasiofurahia kwenye ufalme wake. Lakini kwa kuwa Mfalme hapendi ye yote apotee, anakifunga kitabu chake kwa karibisho, onyo na ahadi:

"Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure. Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki: Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki … Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, 'Naam, naja upesi.'"

> "Amina; na uje, Bwana Yesu." (Ufunuo 22:17-20)



Baada ya Adamu kutenda dhambi, alisema nini kwa Mungu, Mungu alipokuja bustanini akimwita? Adamu alijibu kwa aibu,

> "Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa." (Mwanzo 3:10)

Lakini sasa, baadhi ya uzao wa Adamu huijibuje ahadi ya Bwana ya kuja duniani kwa ajili yao? Huiitikia kwa furaha,

> "Amina, na uje, Bwana Yesu!" (Ufunuo 22:20)


Ni nini kilicholeta badiliko hilo? Kwa nini baadhi ya watu hawaogopi tena kusimama mbele ya Mhukumu wa dunia? Kwa nini wanachochewa sana kuhusu kumwona Mfalme uso kwa uso?

Ni kwa sababu wanaamini habari na ujumbe wake.

Nabii Isaya aliandika,

> Ni nani aliyesadiki habari mliyoileta? … Sisi sote kama kondoo tumepotea. Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe. Na BWANA ameyaweka juu yake maovu yetu sisi sote. (Isaya 53:1,6)

Isaya alijumuisha habari na ujumbe wa Mfalme kwenye kauli tatu:




**1. Tuna tatizo.**

"Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe."



**2. Mungu ana ufumbuzi.**

"BWANA ameyaweka juu ya [Mwanawe] maovu yetu sisi sote."



**3. Tuna uchaguzi.**

"Ni nani aliyesadiki habari mliyoileta?"

Unamwamini Mfalme?

> Tukiupokea ushuhuda wa wanadamu, ushuhuda wa Mungu ni mkuu zaidi, kwa maana ushuhuda wa Mungu ndio huu, kwamba amemshuhudia Mwanawe …
>
> Asiyemwamini Mungu amemfanya mwongo, kwa kuwa hakuuamini huo ushuhuda ambao Mungu amemshuhudia Mwanawe. Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele, na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima, asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.
>
> Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu. (1 Yohana 5:9-13)

Ndiyo, unaweza *kujua*. Mfalme hataki uendelee kubahatisha.

Umeipa mgongo dini ya wanadamu na kuuamini ushuhuda wa Mungu? Kama ni hivyo, basi utakuwa na Mfalme milele …

kwa furaha milele baadaye.

## Ujumbe Kwenye Habari • 2

# Habari Mbaya

Kama tulivyosoma mwanzoni mwa kitabu chake, Mfalme wa ulimwengu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake na kwa sura yake. Aliwafanya wanadamu kwa utukufu wake. Watu wawe tunu yake maalumu, marafiki wa karibu, na raia watakatifu kwenye ufalme wake wa nuru. Lakini kwanza lazima uwepo muda wa kujaribiwa.

BWANA alimpa Adamu jaribio dogo lenye madhara makubwa. Mungu alimwambia kuwa alikuwa huru kula matunda ya miti yote isipokuwa mmoja. Mungu alisema litamtokea jambo gani Adamu akilivunja agizo hili moja?



Mungu alimwambia Adamu kuwa lazima kukariri sala, kufunga, na kufanya matendo mema ya kutosha kuwianisha na matendo yake mabaya? *La!* Mungu alisema, "Utakapokula matunda ya mti huo *utakufa hakika*." (Mwanzo 2:17).



Tunajua kilichotokea. Mwanadamu alichagua kumwasi Mfalme-Muumbaji wake Adamu na Hawa walitenda dhambi. Lakini walikufa siku ile ile? Hapana. Basi Mungu alikuwa na maana gani aliposema, "Utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika"?

Ni nini maana ya kifo kulingana na Maandiko?



Iangalie picha. Linatokea jambo gani kwenye tawi? Tawi litakuwaje likiondolewa kwenye mti? Litakuwa hai? Au litakufa?

Tawi linaweza kuonekana kama liko hai bado, lakini litakufa kwa sababu limetengwa na chanzo chake cha uhai.

Kifo maana yake ni *kutengwa*. Hizi ni habari mbaya.

Adamu na Hawa walipochagua kwenda njia yao wenyewe badala ya njia ya Mungu walipoteza muungano wao na Mungu, kama tawi lililoondolewa kwenye mti. Uhusiano wao na Mungu ulikufa. Hawakutaka tena kuwa naye. Walijaribu kujificha. Adamu na Hawa walikuwa wamekufa kiroho.

> Maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia. (Isaya 59:2)



Adamu na Hawa pia walianza kufa kimwili. Kama majani kwenye tawi lililovunjika ambayo hayakauki hapo hapo, na miili yao haikurudi kwenye udongo siku waliyotenda dhambi. Lakini hatua ya kuzeeka ilikuwa imeanza. Kifo alikuwa adui ambaye hawangeweza kumwepuka.

Lakini hizo habari mbaya zinakuwa mbaya zaidi. Bila ya Mungu kutoa wokovu, Adamu na Hawa walikabiliwa na kutengwa na Mungu milele kwenye "moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake" (Mathayo 25:41).



Watu wengine hulidhihaki wazo la jahanamu — ziwa la moto ambamo nafsi zilizoathiriwa na dhambi zitawekwa kizuizini milele yote. Lakini




ni busara kudhihaki kile tusichokielewa? Kama wanadamu, hatuwezi kuielewa dhana ya umilele. Ni eneo jingine lililo tofauti.[8] Watu pia walimdhihaki nabii Nuhu alipokuwa akijenga safina na kuwaonya kuhusu ujio wa gharika, lakini mlango wa safina ulipofungwa na gharika likaja, waliuelewa ukweli walioudhihaki. Na watu wakiingia jahanamu watauelewa uzito wa hoja yake.

> Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake. (2 Wathesalonike 1:9)

Mfalme hataruhusu dhambi iuchafue ulimwengu wake milele.

Dhambi ndiyo nguvu haribifu na yenye majanga yenye madhara zaidi kwenye sayari yetu. Dhambi ni chanzo cha uovu wote.



Kama ugonjwa wa kuambukiza, dhambi ya Adamu imetuambukiza wote. Kama kila kijiti na jani kwenye tawi lililovunjika vilivyokufa, kadhalika sisi tumeathiriwa na dhambi ya Adamu. Sisi wote ni sehemu ya tawi la Adamu.




> Kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi. (Warumi 5:12)



Wakati wa Musa, watu walikuwa na dhana ile ile potovu waliyo nayo watu leo. Walitumaini kuwa wakitenda mema mengi kuliko mabaya, Mungu atawahurumia siku ya hukumu. Ili aisahihishe dhana yao hiyo, Mungu alikuja kwenye mlima wa Sinai kwenye moto uwakao na akawapa watu amri kumi wazitii. Ye yote asiyezitii kikamilifu amri zote kumi alihesabiwa kuwa na hatia na kustahili kifo.





Amri hizo kumi ni kama kioo. Uso wako ukiwa mchafu, kioo hukusaidia kuuona uchafu, lakini hakiwezi kuuondoa. Kadhalika na amri hizo hazikukusudiwa kutupatanisha na Mungu. Badala yake, zinatuonyesha kuwa sisi ni wenye dhambi tulio na hatia mbele ya Mungu aliye mtakatifu. Hatufai kuishi kwenye ufalme wake wa haki. Sisi ni wenye dhambi tusio na msaada, tunaohitaji Mwokozi aliye mkamilifu.

> Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. (Warumi 3:23)

Habari mbaya ni kuwa hatukifikii kiwango cha Mungu cha wema mkamilifu. Habari njema ni kuwa kuna mtu mmoja kwenye historia aliyekifikia.

Jina lake ni Yesu.

## Ujumbe Kwenye Habari • 3

# Habari Njema

BWANA ni mkamilifu katika haki na huruma. Haki ina maana kuwa adhabu kamili ya sheria imetekelezwa kulipia dhambi zangu. Huruma ina maana kuwa adhabu ya sheria haikutekelezwa dhidi yangu.

Mungu angewezaje kuiadhibu dhambi yetu bila ya kutuadhibu sisi?

Jibu linapatikana katika Bwana Yesu Kristo, aliyekuja kutuokoa.





Katika nyakati za Agano la Kale, kabla ya Yesu kuja, Mungu aliweka sheria ya sadaka ya dhambi ili kuwaokoa wenye dhambi kutoka kwa sheria ya dhambi na mauti. Alikubali damu ya wanyama wasio na hatia kama malipo kwa ajili ya dhambi. Ndivyo alivyoiadhibu dhambi bila ya kumwadhibu mwenye dhambi.

Lakini mwana-kondoo alitosha badala ya mwanadamu? La. Damu ya wanyama ilikuwa tu kielelezo cha nini hasa haki ilichodai.






Ni damu ya aina gani iliyoweza kukubaliwa kulipa deni la dhambi ya mwanadamu? Ni damu ya mwanadamu mkamilifu asiye na ukomo. Neno-Muumbaji mwenyewe ndiye mwanadamu aliyefaa.

> Hapo mwanzo kulikuwako Neno … Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli. (Yohana 1:1,14)




Damu ya wana-kondoo iliweza tu *kufunika* dhambi. Yesu ndiye "Mwana-kondoo wa Mungu *aichukuaye dhambi* ya ulimwengu" (Yohana 1:29)

Unamkumbuka Habili? Mungu aliziweka dhambi za Habili juu ya mwana-kondoo. Mwana-kondoo alikuwa mbebaji wa muda wa dhambi za Habili. Yesu ni mbebaji wa kudumu wa dhambi zetu. Mungu alimbebesha yeye dhambi zetu zote.

Mwana-kondoo aliyechinjwa na kuteketezwa akawa majivu mahali pa Habili alikuwa kielelezo cha Yesu aliyelipa adhabu kamili kwa ajili ya dhambi zetu. Ndiyo sababu kabla tu ya kufa kwake Yesu alitamka kwa sauti ya ushindi "Imekwisha!" (Yohana 19:30)

Haki imeridhishwa. Huruma ipo.

> Na kwa hiyo [Injili au Habari Njema] mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno … Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo Maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo Maandiko. (1 Wakorintho15:2-4)











Mfikirie Ibrahimu na mwanawe. Kwa nini Mungu aliwatuma kwenda kwenye mlima wa mbali kwa ajili ya sadaka?

Mungu alikuwa anaonyesha mahali ambapo Mwanawe mwenyewe atakwenda afe kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

Kwa nini Ibrahimu aliuita mlima huo "BWANA atajipatia"? Kwa sababu mahali hapo ndipo Mungu alipoitoa sadaka kamilifu na ya mwisho.




Mungu alitoa nini kwa ajili ya mwana wa Ibrahimu? Kondoo dume. Mungu ametoa nini kukuokoa kutoka hukumuni? Yesu, Mwana-kondoo wa Mungu.




Unaogopa kifo na hukumu? Ukiweka imani yako kamili kwa Yesu kama Mwokozi huna haja ya kuogopa, kwa sababu Mungu amepokea malipo kamili kutoka kwake kwa ajili ya dhambi zako na akamfufua tena.

Sasa mfikirie Adamu na Hawa. Dhambi na aibu yao iliwafanya wajifunike kwa majani ya mtini na watake kujificha Mungu asiwaone. Kwenye haki na huruma yake, Mungu aliifunua dhambi yao na kuwavika ngozi za wanyama waliotolewa sadaka. Damu ya wanyama iliyomwagika ilitoa kielelezo cha kilichohitajika kufunika dhambi yao, na ngozi za hao wanyama zilikuwa kielelezo cha kilichohitajika kufunika aibu yao.

Wote tunashiriki dhambi na aibu ya babu zetu. Tunapungukiwa na haki ya Mungu. Hatufai kuishi naye. Habari njema ni kuwa msalabani Yesu Kristo alichukua dhambi na aibu yetu. Kwenye masaa yale ya giza, Alionja kutengwa na Mungu tunakostahili. Kisha alikufa. Lakini kwa kuwa hakuwa na dhambi yeye mwenyewe, kaburi halikuweza kumshikilia.

Kwa kufa na kufufuka kwa Yesu, Mungu anakusafisha na kukuvika: kubadilishana dhambi zako kwa haki yake.




> Sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu [kwa dhambi]. Na matendo yetu ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi. (Isaya 64:6)




> Nitafurahi sana katika BWANA, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki. (Isaya 61:10)

> Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye. (2 Wakorintho 5:21)

Siku ya hukumu, utakuja mbele za Mungu na matambara ya juhudi zako za kidini?

Au utasimama mbele zake umevikwa haki timilifu ya Kristo?

## Ujumbe Kwenye Habari • 4

# Mwitikio Wako Kwa Mfalme

Jifikirie unatembea peke yako kwenye pori lisilo na watu. Unapenda ukutane na nini —mwana-kondoo, au simba?



Alipokuja mwanzoni, Mfalme wa utukufu aliitwa *Mwana-kondoo*. Alikuja akiwa mnyenyekevu awaokoe wenye dhambi. Mfalme atakaporudi, Ataitwa *Simba*. Atakuja kwa fahari kuwahukumu wenye dhambi wasiotubu.



Yesu akirudi, utafurahia kwenye uwepo wa Mfalme-Mwokozi wako au utatetemeka mbele ya Mfalme-Mhukumu wako? Yote yanategemea mwitikio wako kwenye ujumbe wa Mungu.

Yesu alipoanza kusafiri na kufundisha, baadhi ya maneno yake ya mwanzo yalikuwa,

> "Tubuni, na kuiamini Injili!" (Marko 1:15)

"Tubu" ina maana ya *badili mawazo yako* kuhusu unachoamini ili uwe na haki ya kuishi kwenye ufalme wa Mungu. Ina maana ya kuacha kuamini njia yako mwenyewe na kuanza kuamini na kufuata njia ya Mungu.

"Iamini Injili" ina maana ya *weka imani yako kwa Neno la Mwokozi* aliyekufa kwa ajili ya dhambi zako na kufufuka tena akupe uzima mpya. Lakini maana yake ni nini kuweka imani yako kwa fulani?

Naelezea kwa kutimia habari za kweli kutoka Afrika ya Magharibi. Ni kuhusu wanawake wawili, Fatu na Bintu.

Wote walikuwa na ugonjwa kwenye macho yao. Fatu alikwenda kwenye hospitali. Daktari alimpa dawa za matone za kuua wadudu. Macho yake yalipona. Bintu alikwenda kwa mganga wa kienyeji. Alisugua "tiba" yake kwenye macho ya Bintu. Macho yake yakawa meupe akawa kipofu.

Fatu na Bintu wote walikuwa na iamini. Wote waliitendea kazi imani yao wakienda kwa tibabu waliyemwamini — lakini matokeo yalikuwa tofauti mno.

Tukija kwenye umilele, kila mmoja anaamini kitu au mtu fulani. Wengi huning'iniza tumaini lao kwenye dini ya wazazi wao. Baadhi hukubaliana na wanaoamini kuwa maisha huishia kwenye kaburi. Wengine wana maoni yao wenyewe kuhusu uzima, kifo, na umilele. Hatimaye, swali moja tu ni muhimu: Uliyochagua ndiyo kweli yenyewe?

Kwa upande wangu, nimefanya uchaguzi wangu. Ninamwamini Mfalme, aliyesema,

> "Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu." (Yohana 18:37)

Ndiye ninayetaka niishi naye milele. Ndiye "ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).

Yeye si tu mfalme. Ni Mfalme *wangu!*





Mwanadamu wa kwanza aliumbwa auakisi mfano wa Mungu. Mfano huo uliharibiwa na dhambi. Yesu Kristo, aliye "mfano wa Mungu asiyeonekana" (Wakolosai 1:15), alikuja kukupa uzima mpya na kuurudisha mfano wa Mungu ndani yako.



Kama umeweka imani yako ndani ya Yesu Kristo aliye Mfalme wa utukufu, basi, machoni pa Mungu, hauko tena *ndani ya Adamu*. Wewe umo *ndani ya Kristo*. Wewe ni raia wa mbinguni na mtoto mpendwa wa Mungu uliyependelewa. Wewe ni tunu ya Mungu mwenyewe, aliyoikomboa kwa damu ya Mwanawe mwenyewe.

Kama kiungo kipya cha familia ya Mungu sasa unaweza kumwita Mungu *Baba*. Lakini kwenye faida kubwa huja wajibu mkubwa.

> Kama watoto wa kutii msijifananishe na tamaa zenu za kwanza, za ujinga wenu; bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote. (1 Petro 1:14-15)

Kama mfuasi wa Kristo, umeagizwa kusamehe, kuwapenda na kuwaombea watu wote, hata adui zako. Yesu anasema,

> "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." (Yohana 13:35)

Unaponyenyekea kwake, Roho wa Bwana Yesu, aliyeingia moyoni mwako ulipoiamini Injili, atakusaidia kushinda dhambi na kuiakisi tabia yake takatifu.

> Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi. (Wagalatia 5:22-23)

Kama mtoto wa Mfalme, una kusudi jipya katika maisha: Kumheshimu Yeye. Wewe ni balozi wake kwenye ulimwengu uliopotea. Mwakilishe vema. Siku moja utamwona uso kwa uso, na hapo "utafanana naye" (1 Yohana 3:2). Hadi wakati huo, zungumza naye wakati wo wote. Mtukuze katika hali yo yote. Mwabudu na kumtumikia pamoja na wanaompenda na kulipenda Neno Lake. Yachunguze Maandiko kila siku (ukianza na *Luka, Yohana,* Matendo, na *Warumi)*. Roho Mtakatifu ni mwalimu wako. Biblia ni chakula na silaha yako ya kiroho dhidi ya Shetani, asiyependa ufikiri, uzungumze, na utende kama Yesu. Kadiri unavyoyatafakari Maandiko ndivyo unavyokuwa na nguvu zaidi kiroho.



Naupenda mfano huu wa neno kutoka kwenye Zaburi:

> Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu. (Zaburi 42:1)

Unaweza kusema hivyo?

Uamuzi ni wako.

*Paul D. Bramsen*
resources@rockintl.org

# Mambo Ya Ziada

Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.

Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo tunasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu.

—Kutoka kwenye Agano Jipya
(Waefeso 2:8-10; Warumi 5:1-2)

## Mfalme Wa Utukufu:

# Maswali Ya Mapitio • Sehemu ya 1 • Agano La Kale

Orodha hii hutoa swali moja au mawili kwa kila tukio kati ya hayo 70. Majibu yamo kwenye kila kifungu kinachoambatana na tukio husika. Uko huru kunakili kurasa hizi kwa kujifunzia kwenye kundi.

Kwa maelezo zaidi tembelea: **www.one-god-one-message.com**.

*Namba ya tukio • Swali(au maswali)*

1 • Mfalme wa utukufu alitumia maelfu ya miaka kuiendeleza mipango yake. Hili linakueleza nini kuhusu Mfalme huyu?

2 • Sehemu kuu mbili za Biblia ni zipi? Kuna tofauti gani kati ya sehemu hizi mbili?

3 • Unayaamini maneno ya mwanzo ya Andiko (Mwanzo 1:1)? Kwa nini unayaamini au huyaamini?

4 • Hata kama ni Mungu pekee aliyekuwako, kamwe hakuwa peke yake. Unaelewa nini kuhusu kauli hii?

5 • Tunaweza kujifunza nini kuhusu Mungu kutokana na vitu alivyoviumba?

6 • Taja njia kadhaa ambapo Mungu alimwumba mwanadamu tofauti na wanyama.

7 • Kwa nini Mungu hakumwuliza Adamu kama alitaka kuishi katika Edeni?

8 • Dhambi ni nini? Mungu alisema nini kitatokea kwa Adamu asipotii agizo la Mungu? Ni neno gani lingine lenye maana ya kifo?

9 • Kama Adamu, Hawa aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Hili lina maana gani?

10 • Kivutio bora zaidi mbinguni ni nini?

11 • Dhambi iliingiaje ulimwenguni?

12 • BWANA alisema nini kitatokea mwanadamu akila tunda la ujuzi wa mema na mabaya? Shetani alisema nini kitatokea?

13 • Dhambi iliingiaje kwenye familia ya wanadamu?

14 • Matokeo ya kwanza ya dhambi yalikuwa nini? Ni kwa njia gani Adamu na Hawa walikuwa na aibu badala ya heshima?

15 • Ni kwa njia gani Adamu na Hawa walikufa siku ile ile waliyotenda dhambi? Ni vipi walikuwa kama tawi lililovunjika? (Ona pia ukurasa wa 160.)

16 • Taja njia kadhaa ambapo laana ya dhambi imeuharibu uumbaji wa asili.

17 • Unadhani kwa nini mpango wa siri wa Mungu ulijumuisha Mwokozi atakayekuwa wa uzao wa mwanamke (aliye na mama mwanadamu, lakini bila baba mwanadamu)?

18 • Mungu alifanya nini kufunika dhambi na aibu ya Adamu na Hawa? Mungu aliwaonyeshaje kuwa yeye ni Mungu wa haki, huruma na neema?

19 • Kwa nini Mungu aliwafukuza Adamu na Hawa kutoka kwenye bustani ya Edeni?

20 • Dhambi ya Adamu na Hawa iliwaathirije watoto wao? Inatuathirije sisi na familia zetu? (Ona pia ukurasa wa 161.)

21 • Mungu alikubali mwana-kondoo wa aina gani kufa badala ya mwenye dhambi?

22 • Nini maana ya *ondoleo?* Kwa nini Mungu alitaka malipo ya kifo?

23 • Mungu alifanya nini na dhambi ya Habili? Sadaka ya Kaini ilikuwa na tatizo gani?

24 • Nini maana ya kutubu? Mungu alitaka Kaini afanye nini? Kaini alifanya nini?

25 • Gharika ya dunia nzima ya wakati wa Nuhu hutufundisha nini kuhusu uvumilivu wa Mungu na hukumu yake?

26 • Kitu cha kwanza kufanya Nuhu na familia yake walipotoka kwenye safina kilikuwa kitu gani?

27 • Mnara wa Babeli hutoa kwa njia gani kielelezo cha dini ya uongo?

28 • Ni zipi ahadi mbili kuu ambazo BWANA alimpa Ibrahimu kama atamwamini na kumfuata BWANA?

29 • Kwa nini Mungu aliwasamehe Ibrahimu na Sara dhambi yao na kuwahesabu kuwa ni wenye haki?

30 • Mwana wa Ibrahimu alimwuliza baba yake swali lipi walipokuwa wakiupanda mlima wa kutoea sadaka?

31 • Mungu aliahidi kumfanya Isaka awe baba wa taifa jipya. Kwa kuwa Ibrahimu alijua kuwa Mungu hawezi kusema uongo, Ibrahimu alifikiri Mungu atafanyaje baada ya Ibrahimu kumtoa sadaka Isaka madhabahuni?

32 • Kwa nini Ibrahimu aliupa mlima ule jina la *BWANA atajipatia? Mwana-kondoo* alikufa siku ile badala ya mwana wa Ibrahimu?

33 • BWANA alizitimizaje ahadi kuu mbili alizompa Ibrahimu?

34 • Tukijaribu sana kutii maagizo ya Mungu, tunaweza kuwa wema wa kutosha kuwa na sifa ya kuishi na Mungu mbinguni? Hizo Amri Kumi zinafananaje na kioo? Amri hizo zinatuonyesha kwa njia gani kuwa tunahitaji Mwokozi?

35 • Kwa nini sadaka za wanyama hazikuweza kuondoa deni la dhambi ya ulimwengu?

36 • Chagua unabii mmoja kutoka kwenye gombo na ueleze lilivyomlenga Mwokozi atakayekuja.

## Mfalme Wa Utukufu:
# Maswali Ya Mapitio • Sehemu ya 2 • Agano Jipya

37 • Kwa nini Mungu alitumia watu wanne (badala ya mtu mmoja tu) kuziandika habari za Injili inayomhusu Yesu?

38 • Kwa nini malaika Gabrieli alimwita Yesu *Mwana wa Mungu?*

39 • Jina *Yesu* lina maana gani?

40 • Ni nini unachokifurahia zaidi kuhusu habari za kuzaliwa kwa Yesu?

41 • Malaika aliwaambia wachungaji, "amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana." Kwa nini wachungaji walisisimka kusikia habari hizi?

42 • Ilikuwa haki Mamajusi kumwabudu mtoto Yesu? Kwa nini ilikuwa au haikuwa haki?

43 • Yesu alikuwa tofauti na watoto wengine kwa namna gani?

44 • Ni kwa vipi ujumbe wa nabii Yohana ulikuwa tofauti na ujumbe wa manabii wote waliotangulia? Unadhani kwa nini Yohana alimlenga Yesu na kusema, "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu"?

45 • Litazame tena tukio hili na ueleze jambo unalojua kutoka kwenye Maandiko kuhusu Roho wa Mungu, Mwana wa Mungu, na Baba wa mbinguni.

46 • Kwa nini Shetani alijaribu kumfanya Yesu atende dhambi?

47 • Baada ya Yesu kulisoma gombo la nabii Isaya, alisema, "Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu!" Unadhani kwa nini hili liliwakasirisha majirani zake?

48 • Yesu alikuwaje *Mkono wa Mungu* duniani? Kwa nini mapepo yalimwogopa Yesu?

49 • Baada ya Yesu kuiamuru dhoruba, "Nyamaza! Utulie!" wanafunzi walisema, "Ni nani huyu? Hata upepo na mawimbi vyamtii!" Unafikiri Yesu ni nani?

50 • Kwa nini wakuu wa dini walimshitaki Yesu kuwa amekufuru?

51 • Yesu alisema, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima, Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi." Tunajuaje kuwa alisema kweli?

52 • Yesu aliwaambia nini watu waliorudi kesho yake wakitafuta chakula kingine?

53 • Lipitie tukio hili na ueleze jambo moja alilosema Yesu likakushangaza.

54 • Manabii walimwita Masihi "jua la haki." Yesu alijiita mwenyewe "nuru ya ulimwengu." Yesu Masihi ni tofauti na manabii kwa vipi?

55 • Wanafunzi walidhani Masihi alipaswa kufanya nini? Masihi alikuja kufanya nini?



56 • Kwa nini Bwana Yesu akielekea Yerusalemu alipanda mwana-punda mnyama wa hali ya chini badala ya farasi wa kivita mwenye nguvu?

57 • Kwa nini wakuu wa dini hawakufanikiwa kumtega aweze kutamka makosa?

58 • Kwa nini kuhani mkuu na wakuu wa Wayahudi walisema kuwa inampasa Yesu kuuawa?

59 • Kwa nini Pilato alimhukumu Yesu kifo?

60 • Askari walimshindilia kofia ya miiba Yesu kichwani. Miiba inatukumbusha nini?

61 • Unabii wa Ibrahimu ulitimizwaje na Yesu? Una thamani gani kwa Mungu?

62 • Wahalifu wawili walisulibiwa karibu na Yesu. Leo mmoja yuko jahanamu (ametengwa milele na Bwana) na mwingine yuko mbinguni (milele na Bwana). Tofautiililetwa na nini?

63 • Bwana Yesu alipokuwa msalabani gizani,<br>Baba wa mbinguni alimwekea Yesu mzigo gani?<br>Kwa nini Yesu alisema, "Imekwisha"?<br>Kwa nini Mungu alilipasua pazia la hekalu?

64 • Wanafunzi walikumbuka ahadi ya Yesu ya kufufuka tena? Viongozi waovu wa dini waliikumbuka ahadi yake?

65 • Wanawake walikuta nini walipokuja kaburini jumapili asubuhi? Viongozi wa dini walifanya nini kuhusu kaburi lililo tupu? Nikimtumaini kikamilifu Mwana-kondoo wa Mungu aliyekufa kwa ajili ya dhambi zangu na kufufuka tena, kwa nini sina haja ya kuogopa kifo?

66 • Kwa nini Bwana Yesu aliwaambia wawili waliokuwa wakisafiri kwenda Emau kuwa walikuwa wazito kufahamu?

67 • Mwokozi aliyefufuka alipowatokea kwenye chumba, Tomaso alimwambia, "Bwana wangu na Mungu wangu!" Tomaso alikuwa sahihi au alikosea kumwita Yesu Bwana wake na Mungu wake? Kwa nini?

68 • Yesu aliwaambia wanafunzi wafanye nini yeye akiisha kurudi mbinguni?

69 • Mfalme wa utukufu ni nani? Unafikiri nini juu yake?

70 • Mfalme akirudi utafurahi au utaogopa? Kwa nini?

## Ukumbusho Wa Mwisho

1 **Nyuma ya Matukio:** Wakati *Alice in Wonderland* ikitafsiriwa katika lugha karibu 200, *Bibliia Takatifu*, nzima au sehemu yake, iko katika lugha zaidi ya 2500.

2 Biblia imethibitishwa na wachunguzi wa mambo ya kale, historia ya kidunia, unabii uliotimia, na msimamo thabiti wa habari zenye mambo mengi yaliyoandikwa kwa muda wa karibu miaka 2000.

3 **Tukio la 2:** Mfalme si tu Muumbaji na mtunzaji wa ulimwengu wake, yeye pia ndiye Mwandishi na Kiongozi wa kitabu chake. Magombo ya karibu na Bahari ya chumvi (The Dead Sea Scrolls) huthibitisha Maandiko ya Agano la Kale tuliyo nayo leo kuwa ndiyo yaliyokuwako kabla ya wakati wa Kristo. Maandiko ya Agano Jipya huthibitishwa na maelfu ya maandishi ya kale, mengi yakiwa ya karne za mwanzo baada ya Kristo. Dai lililoenea kuwa maandiko ya asili yaligeuzwa na kuvurugwa na watu hayana msingi wa kweli. Ona kitabu kiitwacho *One God One Message*, sura ya 3. www.one-god-one-message.com

4 **Tukio la 5:** Kwa mtazamo wenye kina kwenye sifa za Mungu kama zinavyoonekana kwenye siku sita za uumbaji, ona kitabu cha *One God One Message*, sura ya 8.

5 **Tukio la 6:** Kwa kuwa Mungu ni MMOJA, kwa nini anasema, "na TUmfanye mtu kwa mfano WETU…"? Jibu limo kwenye umoja wake wenye sehemu nyingi. Kwenye Maandiko, neno la Kiebrania kwa maana ya "Mungu" ini *Elohim*, ambalo ni nomino yenye wingi. Neno linaloonyesha "mmoja" kwenye maneno "Mungu ni mmoja" ni *echad*, ambalo linaweza kumaanisha umoja mchanganyiko. Kwenye umilele, kabla ya kuumba malaika au wanadamu, Mungu alifurahia ushirika ndani yake mwenyewe—na Neno lake/Mwana na Roho Mtakatifu. "Mungu ni mkuu—nasi hatumjui!" (nabii Ayubu 36:26)

6 **Tukio la 6 & 7:** Viini vinavyouumba mwili vimo kwenye vumbi la dunia. Ukweli huu haukutambuliwa na wanasayansi hadi nyakati za karibuni. Huku msingi wa ufahamu wa wanasayansi wengi ukiwa kwenye uchunguzi na *nadharia*, (hoja za wanadamu), msingi wa ufahamu wa wanaoamini Biblia ni uchunguzi na *ufunuo* (Neno la Mungu).

7 **Tukio la 11:** Zaidi kuhusu asili ya Shetani, ona *One God One Message*, sura ya 11.

8 **Tukio la 16:** Kama ziwa la moto, kwenye adhabu ya milele, linaonekana kutotenda haki au kutokuwa na sababu kwenye akili zetu, huenda hatujauelewa bado utakatifu kamili wa Mungu, asili ya milele ya mwanadamu, uovu wa dhambi, na dhana ya umilele. Neno lenyewe *umilele* huuzidi uwezo wa akili zetu, kwa kuwa muundo wetu wa rejea ni wakati. Umilele hauna wakati. Mungu aliyeumba wakati hawekewi ukomo na huo (2 Petro 3:8-9). Umilele hautokani na miaka. Uufikirie kama *sasa ya milele*. Wenye dhambi wakiiingia dola hiyo isiyoepukika, watatambua uzito wa hoja yake.

9 **Tukio la 17:** Kufidia (au kukomboa) ni *kurudisha kwa kulipa gharama inayotakiwa*. Kwenye sura ya 18 ya *One God One Message* mwandishi analifafanua hili habari za wakati wa utoto wake:

> Kama kijana nikikulia huko California, nilikuwa na mbwa mdogo. Nilimlisha, nilimtunza, na kucheza naye. Alikuwa akinifuata na nikirudi kutoka shule alisisimka. Lakini alikuwa na tatizo. Wakati mwingine alizurura kwa majirani, ingawa alikuwa akirudi kila mara. Hadi siku moja.
>
> Nilikuja nyumbani kutoka shuleni, lakini mbwa wangu hakuonekana anikaribishe. Hadi wakati wa kulala alikuwa hajaonekana. Siku iliyofuata baba yangu aliona niulizie kwenye kituo cha wanyama cha eneo letu, wanaposhikiliwa kwa muda paka na mbwa wazururaji. Wanyama wasiofuatiliwa waliuawa.
>
> Nilifika kwenye kituo hicho. Ndiyo, walikuwa na mbwa mdogo wa kufanana na maelezo yangu. Mkamataji wa mbwa jijini alikuwa amemwokota. Mbwa wangu hakuwa na uwezo wa kujiokoa. Bila ya mtu wa kuja kumwokoa angeuawa.
>
> Nilikwenda kwenye zizi lile. Nilitaka kumrudisha nyumbani mbwa wangu! Lakini mhusika kwenye dawati la mbele aliniambia kuwa kama ninataka kumchukua lazima nilipe adhabu. Ilikuwa kinyume cha sheria mbwa kuachwa azurure mtaani.
>
> Nililipa gharama iliyotakiwa na mbwa wangu alikuwa huru. Alifurahi sana kutoka kwenye pango lile la kutisha akarudi pamoja na yule aliyemtunza! Alikombolewa.
>
> Uzoefu wa ujana wangu katika kumrudisha kwa gharama mbwa wangu mpotevu hutupa wazo fulani kuhusu hali yetu. Kama wenye dhambi tulioasi tukahukumiwa, hatuna njia ya kujiokoa kutoka kwenye adhabu ya dhambi yetu, kutoka kwenye sheria ya dhambi na mauti.
>
> Tunahitaji Mwokozi wa kulipa gharama ya ukombozi.

10 **Tukio la 23:** Huenda Mungu alionyesha kuikubali sadaka ya Habili kwa kufanya kama alivyofanya kwenye siku za nabii Musa, Sulemani, na Eliya: "Moto ukatoka hapo mbele za BWANA, na kuiteketeza sadaka ya kuteketezwa, na yale mafuta juu ya madhabahu." (Walawi 9:24; 2 Mambo ya Nyakati 7:1; 1 Wafalme 18:38).

11 **Tukio la 30 & 61:** Maana ya Moria ni *Mteule wa BWANA*. Ni eneo ambapo Yerusalemu ilijengwa baadaye. Leo, Mlima wa Moria ndilo eneo liliposimama hekalu la Sulemani hapo mwanzo (2 Mambo ya Nyakati 3:1). Si mbali sana, kwenye safu ile ile ya milima kuna "mahali paitwapo Fuvu la Kichwa" (Luka 23:33).

12 **Tukio la 36:** Unabii uliotimia huitenga Biblia na vitabu vingine vyote duniani. Unabii wa manabii wa matukio yajayo, ukifuatiwa na kutimia kwake kwenye historia, ni njia moja ya Mungu kuhalalisha ujumbe wake. Ni Mungu pekee anayeweza na kutamka "nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado" (Isaya 46:10). Yesu Masihi alisema, "Tangu sasa nawaambia kabla hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini ya kuwa mimi ndiye" (Yohana 13:19). Ona *One God One Message*, sura ya 5.

13 **Tukio la 41:** Kristo ni neno la Kigiriki kwa neno la Kiebrania *Masihi* lenye maana ya *Mteule*.

14 **Tukio la 41:** Msingi wa kuweka tarehe kwenye matukio ni kwenye mwaka aliozaliwa Yesu Kristo. Kwa mfano, nabii Ibrahimu alizaliwa kama mwaka wa 2000k.K. (miaka 2,000 *kabla ya Kristo kuzaliwa*). Kitabu hiki *(Mfalme wa Utukufu)* kiliandikwa mwaka wa 2011b.K. (zaidi ya miaka 2,000 *baada ya Kristo kuzaliwa*). bK ni kifupi cha baada ya Kristo (AD ni kifupi cha Kilatini *Anno Domini*, yaani *kwenye Mwaka wa Bwana wetu*. Wengi leo hutumia BCE (Before Common Era yaani Kabla ya Enzi ya Wote) na CE (Common Era yaani Enzi ya Wote) kumwondoa Kristo kwenye ufupisho huo, lakini eneo la mgawanyiko wa historia linabaki kuwa kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

15 **Tukio la 43:** "'Huyu si Yule seremala, mwana wa Mariamu na ndugu yao Yakobo, na Yose, na Yuda, na Simoni? Na maumbu yake hawapo hapa petu?' Wakajikwaa kwake." (Marko 6:3). Kwa kuwa Yusufu hakuwa baba yake wa kumzaa, Yesu alihusiana na ndugu zake tu upande wa mama yake. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na Mwana wa Adamu. Ona ukumbusho wa mwisho 19 (Tukio la 52).

16 **Tukio la 43 & 58:** Kila mwaka kwenye sikukuu ya Pasaka Wayahudi walikumbuka tukio lililotokea wakati wa Musa walipokuwa watumwa huko Misri. Wahenga wao walichinja wana-kondoo na damu kuipaka kwenye mihimili ya milango ya nyumba zao kwa sababu Mungu alisema, "nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu" (Kutoka 12:13). Usiku wa manane BWANA alimuua mzaliwa wa kwanza wa kiume wa kila nyumba isiyo na damu kwenye mihimili ya milango yake. Mungu alitumia tukio hili kuwaokoa watu wake kutoka kwenye miaka 400 ya utumwa.

17 **Tukio la 45:** Upande huu wa mbingu kamwe hatutauelewa kikamilifu umoja wa Mungu katika utatu. Hata hivyo yeye ni MUNGU. Hata hivyo jambo moja tunalojua wote, ni ile dhana ya kitu kimoja kuwa vitatu, huku kikiwa kimoja. Ulimwengu wetu umejaa umoja wa vitatu: WAKATI: ni uliopita, uliopo, na ujao. NAFASI: urefu, upana, kimo. MWANADAMU: roho, nafsi,

mwili. ATOMU: electroni, protoni, nutroni. JUA letu nalo lina umoja wenye tatu. Hilo kuu la angani tunaliita *jua,* mwangawake, *jua,* na joto lake *jua,* lakini jua ni moja. Kadhalika na BWANA ambaye ni Baba wa Milele, Mwana wa Milele, na Roho Mtakatifu wa Milele. Kama nuru na joto vinavyotoka kwenye jua, kadhalika na Mwana (Neno) la Mungu na Roho wa Mungu hutoka kwa Mungu, lakini "BWANA ndiye mmoja" (Kumbukumbu 6:4). Ona pia Tukio la 4 na ukumbusho wa mwisho 5 (Tukio la 6). Kupata zaidi kuhusu umoja wa Mungu wenye wingi na asili ya Yesu ya kibinadamu na kimungu, soma *One God One Message*, sura ya 9 na ya 17. Na bora zaidi soma Injili ya Yohana.

18 **Tukio la 47:** Masihi ina maana ya *Mteule* au hasa *Mpakwa mafuta*. Nyakati za kale huko Mashariki, mfalme mpya anapotawazwa, kuhani au nabii alimimina mafuta maalumu ya upako kichwani kwake kuonyesha ndiye kiongozi mpya wa ufalme. Yesu hakumwagiwa mafuta na mwanadamu, bali na Roho Mtakatifu mwenyewe (ona Tukio la 45).

19 **Tukio la 52:** Mara nyingi Yesu alijiita Mwana wa Adamu. Wakati wote yeye ni Mwana wa Mungu, lakini alikuja awe Mwana wa Adamu. Kama Mwana wa Mungu, ndiye Neno aliyekuwako kwa Mungu hapo mwanzo (Yohana 1:2; Mwanzo 1:3), lakini kama Mwana wa Adamu, ndiye Neno aliyefanyika mwili, aliyeteuliwa na Mungu awe Mwokozi-Mhukumu-Mfalme wa ulimwengu (Yohana 1:14; Danieli 7:13-14).

20 **Tukio la 56:** Mafarisayo walikuwa waumini wa sekta kali ya Kiyahudi. Baadhi yao waliomba mara sita kila siku, walifunga miezi mitatu kwa mwaka, na kutoa asilimia 10 ya mapato yao kwa maskini (Luka 18:9-14). Lakini yote yalikuwa desturi tupu. Walikuwa watu wa dini, lakini hawakumjua na kumpenda Mungu.

21 **Tukio la 68:** Kwa wanaomwamini Bwana Yesu Kristo ubatizo ni njia ya kutangaza uamuzi wao wa kumfuata. Kuzamishwa kwenye maji hakuondoi dhambi. Kunaashiria utambulisho wa mtu na Yesu katika kufa, kuzikwa, na kufufuka kwake. Ubatizo wa maji pia huonyesha mwisho wa maisha ya kale na mwanzo wa maisha mapya ndani ya Kristo.

22 **Tukio la 68:** Si siku nyingi baada ya Mwana wa Mungu kupaa mbinguni, Roho wa Mungu alishuka ili aishi kwenye moyo wa kila mwanaume, mwanamke, na mtoto anayeiamini Injili. Kitabu cha Matendo kwenye Agano Jipya kina habari za kusisimua kuhusu Roho Mtakatifu alivyowapa wanafunzi uwezo wa kuionyesha tabia ya Yesu na kuujulisha ujumbe wake kwa mataifa. Njia ya Mungu ya wokovu haijabadilika. Ukiamua kuuamini ujumbe wake — kuwa wewe ni mwenye dhambi uliyetengwa na Mungu aliye mtakatifu na usiyeweza kujiokoa mwenyewe kutoka kwenye adhabu ya dhambi na kuwa Yesu Kristo alichukua adhabu yako msalabani, akazikwa, na kufufuka kutoka kwa wafu — basi na wewe utaipokea karama ya Roho Mtakatifu. Hii ina maana kuwa Mfalme wa ulimwengu mwenyewe atakuja aishi moyoni mwako. Atakuwa Bwana, Baba, na Rafiki wako mpya. Andiko linasema, "Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake" (Waefeso 1:13-14). Mungu ni Mfalme mkubwa wa ajabu, na atakuwa na familia kubwa ya ajabu pamoja naye milele yote. Utakuwako?



## One God One Message:
## Kwenda Ndani Zaidi

Kama *Mfalme Wa Utukufu*, *One God One Message* hukusafirisha hadi kwenye Maandiko ya manabii, lakini kwa kina zaidi kwa kuwa kinaulinganisha ujumbe wa Biblia na mitazamo mingine ya ulimwengu. Maswali ambayo hayakujibiwa kwenye Mfalme wa Utukufu yamejibiwa kwenye kitabu hiki cha *One God One Message*.

Huku *Mfalme Wa Utukufu* kikichukua chini ya masaa matatu kukisoma kwa sauti, *One God One Message* huchukua kama masaa kumi na mawili.

Kikiwa na ufumaji pamoja wa uzoefu binafsi, barua pepe za wenye kushuku, na simulizi jipya la habari zinazosimuliwa zaidi katika historia, kitabu hiki hutoa mfumo wa kuyafikiria upya maswali makubwa ya maisha.




- Mwandishi: P. D. Bramsen
- Mtoa Vielelezo: D. C. Bramsen
- Mchapishaji: ROCK International
- Vielelezo zaidi ya 30.
- Mwongozo wa majadiliano wenye maswali 150.
- Kumbukumbu za mwisho 270.
- Unapata bure kwenye internet kwa Kiarabu, Kialbania, Kichina, Kiingereza, Kifarsi, Kifaransa, Kirusi, Kihispania, Kituruki, Kiurdu, Kiindonesia …

**www.one-god-one-message.com**

*Kitabu hiki ni hazina ya kweli; mtindo wa uandishi ni wa kipekee; kimejaa shauku ya mwanadamu.*

—William MacDonald, mwandishi wa *Believer's Bible Commentary* na vitabu vingine 80

*Dondoo za barua pepe humthibitishia msomaji kuwa mwandishi hakwepi maswali magumu.*

—Vaughan, Premed Grad kutoka Afrika ya kusini

*Kinasomeka kama simulizi la mpelelezi, ndivyo kilivyo kwa namna fulani.*

—Theo, msomaji wa Canada

*Baada ya kusoma kitabu hiki hoja ya Biblia inaleta maana na kugonga akilini mwangu. Kimeniumbia hamu ya kuisoma Biblia.*

—Mohammed, Mwandishi kutoka Mashariki ya Kati

ROCK INTERNATIONAL INATOA

# MFALME wa UTUKUFU

## FILAMU

Uwasilishaji wa neno kwa neno wa kitabu cha MFALME wa UTUKUFU

**HADITHI 1 KATIKA SEHEMU 2. MILANGO 70 KATIKA MATUKIO 15.**

| | | |
|---|---|---|
| **SEHEMU YA 1: AGANO LA KALE: MFALME ANAELEZA MPANGO WAKE** | saa 1 dakika 47 | |
| 1. Utangulizi | *Milango 1-3* | ~ 10:40 |
| 2. Muumba na Uumbaji Wake | *Milango 4-9* | ~ 19:04 |
| 3. Kuingia kwa Uovu | *Milango 10-15* | ~ 15:10 |
| 4. Laana ya Dhambi na Ahadi ya Mungu | *Milango 16-19* | ~ 11:57 |
| 5. Njia ya Sadaka | *Milango 20-24* | ~ 14:58 |
| 6. Uasi wa Mwanadamu na Uaminifu wa Mungu | *Milango 25-27* | ~ 9:05 |
| 7. Mpango wa Mungu Unaendelea | *Milango 28-32* | ~ 14:04 |
| 8. Sheria na Manabii | *Milango 33-36* | ~ 12:20 |
| **SEHEMU YA 2: AGANO JIPYA: MFALME ATIMIZA MPANGO WAKE** | saa 1 dakika 55 | |
| 9. Ujio wa Mfalme | *Milango 37-42* | ~ 20:16 |
| 10. Tabia ya mfalme | *Milango 43-47* | ~ 15:32 |
| 11. Enzi ya Mfalme | *Milango 48-51* | ~ 14:02 |
| 12. Utume wa Mfalme | *Milango 52-56* | ~ 15:24 |
| 13. Ujitiisho wa Mfalme | *Milango 57-61* | ~ 14:50 |
| 14. Sadaka ya Mfalme na Ushindi | *Milango 62-65* | ~ 13:53 |
| 15. Injili ya Mfalme na Utukufu | *Milango 66-70* | ~ 18:26 |
| *Mungu Wetu ni Mkuu* (ulioimbwa kwa Kiarabu) | *Washiriki* | ~ 2:45 |

*"Filamu hiyo ilieleza mambo kwa njia ningeyoweza kuelewa." — Eli, 7*

*"Nilipitia hadithi hiyo kwa hisia zangu zote kana kwamba nilikuwa pale." — Lydia, 21*

*"Inaeleza baadhi ya maonyesho makubwa zaidi katika ulimwengu kwa njia rahisi lakini yenye nguvu!" — Dick, 74*

MTAALA WA

**MFALME WA UTUKUFU**




KITABU CHA KUCHOREA | MWONGOZO WA MASOMO ULIOONYESHWA | FILAMU YA LUGHA NYINGI | KITABU CHA PICHA

**www.king-of-glory.com**